

UTANGULIZI WA ELIMU YA KUITETEA IMANI



Shepherds Global Classroom ipo kwa ajili ya kuujenga mwili wa Kristo kwa kutoa mtaala kwa ajili ya kuwaendeleza viongozi wa Kikristo duniani kote. Tunalenga kuongeza programu za mafunzo ya asili kwa kuweka chombo cha mtaala wa kozi 20 mikononi mwa viongozi wa kiroho wanaotoa mafunzo katika kila nchi duniani.

Kitabu hiki kinapatikana bure kwa njia ya kupakua kutoka katika <https://www.shepherdsglobal.org/courses>

Mwandishi Mkuu: Dr. Mark Bird

Hakimiliki © 2019 Shepherds Global Classroom
Ilitafsiriwa kutoka Toleo la Pili Kiingereza.

Haki zote zimehifadhiwa.

Nyenko za wahusika wengine zilizotumika ni hakimiliki ya wamiliki husika ambazo zimeshirikishwa na kutumika humu chini ya leseni mbalimbali.

Tafsiri ya Maandiko “yalionukuliwa” kutoka chapisho la Kiingereza kwa ajili ya chapisho hili la Kiswahili yanatoka katika Biblia Takatifu ya Kiswahili, “Swahili Union Version Bible” (SUVB®).” Yametumika kwa kibali. Haki zote zimehifadhiwa.

Taarifa kuhusu vibali:

Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa na kutawanywa bure kikiwa kimechapishwa na katika mifumo ya kidigitali chini ya miongozo ifuatayo: (1) Maudhui yaliyoko kwenye kitabu hiki hayawezi kubadilishwa kwa namna yeoyote ile; (2) Nakala zinazopatikana haziwezi zikauzwa kwa ajili ya kupata faida; (3) Taasisi za elimu zina uhuru wa kutumia na kukinakili kitabu hiki, hata kama wanalipisha ada za masomo ya ziada; na (4) Kitabu hiki hakiwezi kufanyiwa tafsiri pasipokuwepo na kibali na usimamizi wa Shepherds Global Classroom.

Tafsiri ya chapisho la Kiingereza kwenda katika Kiswahili imefanywa na:

Askofu Wilbert Alfayo Ngowi,
Arusha, Tanzania, East Africa.
E-mail: revwangowi@gmail.com

Yaliyomo

Mtazamo wa Mafunzo	5
1. Utangulizi wa Elimu ya Kuitetea Imani	7
2. Dhana potofu dhidi ya Elimu ya Kuitetea Imani	21
3. Je, Mungu Yupo?.....	35
4. Elimu ya Kuitetea Imani ya Uumbaji.....	47
5. Hoja za Ujumla kuhusu Imani ya Kikristo	59
6. Kuaminika kwa Agano Jipya	65
7. Unabii wa Masihi na Ufufuo	81
8. Madai ya Yesu kuwa Yeye ni Mungu	95
9. Upekee wa Ukristo katika Dini Nyingi.....	107
Vianzo Vilivyopendekezwa.....	122
Kumbukumbu ya Kazi Zilizofanywa	124

Yaliyomo katika kozi hii yameandikwa na Dr. Mark Bird, Profesa wa Theolojia katika Chuo cha Biblia cha God's Bible School and College, Cincinnati, Ohio. Mengi ya mafundisho haya yamechapishwa kama *Kuitetea Imani yako* (*Defending Your Faith*), (Kentucky: Answers in Genesis, 2007) na yanatumika kwa kibali kutoka kwa mchapishaji. Mafundisho haya ya *Kuitetea Imani yako* (*Defending Your Faith*) yanapatikana kutoka: Answers in Genesis, P.O. Box 510, Hebron, Kentucky,

41048. Yanaweza kuagizwa kupitia katika mtandao wa intaneti:

<https://answersingenesis.org/store/product/defending-your-faith-leaders-guide/?sku=10-2-263>.

Mtazamo wa Mafunzo

Malengo ya Kozi

- (1) Kuelewa uhusiano uliopo kati ya Elimu ya Kuitetea imani na Injili. (Somo la 1)
- (2) Kujibu hoja potofu zinazohusiana na Elimu ya Kuitetea imani. (Somo la 2)
- (3) Kuelewa ushahidi uliopo kuhusiana na uwepo wa Mungu (Somo la 3)
- (4) Kuthamini ushahidi wa uumbaji (Somo la 4)
- (5) Kukariri hoja za ujumla kuhusiana na ukweli wa Ukristo (Somo la 5)
- (6) Kutambua ushahidi wa kuaminika kwa Agano Jipya (Somo la 6)
- (7) Kuthamini umuhimu wa kutimia kwa unabii kuhusiana na Uungu wa Yesu (Somo la 7)
- (8) Kutathmini ushahidi wa ufufuo wa Yesu Kristo (Somo la 7)
- (9) Kuyaewa madai ya Yesu ya Uungu, na mwitikio unaofaa kwa madai hayo (Somo la 8)
- (10) Kujibu maswali yanayohusu upekee wa imani ya Kikristo, imani ya Utatu Mtakatifu, imani kuwa vitu vyote (miti, mawe upepo n.k.) vina roho, na hatima ya wale ambao hawajawahi kuisikia Injili (Somo la 9)

Maelezo na maelekezo kwa viongozi wa madarasa.

Kozi hii inatambulisha kanuni ya msingi ya elimu ya kuitetea imani. Unapaswa uratibu dakika 90-120 kwa kila mnapokutana darasani. Na muda zaidi wa kufanya kazi za nyumbani nje ya darasa.

Alama ► inaashiria **swali linalopaswa kujadiliwa**. Wakati wowote unapokuja katika hayo, uliza hayo maswali yanayokuja mbele yake, na uwaachie wanafunzi wajadili jibu lake. Jitahidi kuhakikisha kwamba wanafunzi wote darasani wanahusika katika majadiliano. Ikiwa ni lazima, waite wanafunzi kwa majina yao.

Kila tanbihi chini ya ukurasa inarejea **Andiko** la Biblia. Kama aya haijatolewa au hazijatolewa kutoka kwenye fungu, tafadhali wafanye wanafunzi waziangalie na wazisome wakati wa kipindi darasani. Labda iwe imeelekezwa vinginevyo, nukuu ya maandiko yanatoka katika *Biblia Takatifu ya Kiswahili*, (SUV®).

Kila somo lina **kazi tatu za kufanya**. Kazi za kufanya zinatakiwa zimalizike na kuwakilishwa kabla ya muda wa kipindi kingine.

1. Kazi ya kwanza itaelekezwa kwenye **kichwa**. Hii itakuwa ni jaribio linalotakiwa lifanyike kila mwanzo wa kipindi kingine cha darasa baada ya somo kumalizika. Majaribio yote yafanyike bila ya kutazama kutoka kwenye daftari la somo, vidokezo

vilivyoandikwa au kwa mwanafunzi mwengine. Kitabu chenye majibu ya majaribio yote kinaweza kupatikana kwa kupakua kwenye tovuti ya ShepherdsGlobal.org

2. Kazi ya pili itaelekezwa kwenye **moyo**. Hizi kazi fupi fupi zinakusudiwa kuwakumbusha wanafunzi elimu ya kuitetea imani ya kweli inazungumza kuliko akili. Kazi hizi mara nyingine zinakuwa ni ushuhuda wa mtu binafsi. Chukua muda darasani wa kushirikishana shuhuda hizi.
3. Kazi ya tatu itaelekezwa kwenye **mikono**. Hii ni nafasi ya wanafunzi kuyaweka kwenye matendo yale yote waliyojifunza. Kwa njia nyingi, hii ni sehemu muhimu sana katika kozi. Kama wanafunzi hawatazifanya mazoezi kanuni walizofundishwa kwenye kozi, wanaweza wasiweze kuzikumbuka au kuzitumia kanuni hizo baadaye. Chukua muda kuzijadili kanuni hizi kila wiki.

Kwenye kila mwanzo wa kipindi cha darasa, kiongozi anapaswa kutoa **jaribio** dogo linalohusiana na somo lililopita. Uchambuzi wa somo la 7 ni kwa ajili ya mjadala wa darasa, unaofanyika kabla ya somo la 8. Kama kiongozi wa darasa, wajibu wako katika mjadala ni kuwakilisha kila hoja dhidi ya Ufufuo zitokanazo na Somo la 7. Hakikisha kwamba kila mwanafunzi anapata nafasi ya kushiriki angalau katika mojawapo ya hoja husika.

Pia katika kila mwanzo wa kipindi cha darasa, kila mwanafunzi atapaswa kutoa muhtasari wa mjadala wao na kazi ya kufanya kuhusu "Elimu ya kuitetea Imani na Mikono" kwa ajili ya somo lililopita.

Kama mwanafunzi atataka apewe cheti cha kuhitimu **Shepherds Global Classroom**, ni lazima ahudhurie vipindi vyote na akamilishe kazi zote za kufanya. Fomu itatolewa kila mwisho wa kozi kwa ajili ya kuweka kumbukumbu ya kazi zote zilizomalizika.

Somo la 1

Utangulizi wa Elimu ya Kuitetea Imani

Utangulizi

Jia ni Mkristo mchanga wa Taipei. Amekuwa Mkristo kwa mwaka mmoja. Kwa miezi michache iliyopita, amekuwa akijaribu kushiriki katika Injili na Lee, aliye jirani yake. Lee siyo mwamini na anapenda kumwuliza Jia maswali magumu sana. Mara nyingine Jia anafikiri kwamba Lee ana mashaka ya kweli na anatafuta ukweli; wakati mwingine anafikiri kwamba anataka tu kubishana. Hata hivyo, pamoja na kusudio lake hilo, Jia hujaribu kuwa na heshima na kuonyesha upendo wa Kikristo. Hata akiwa mwamini mchanga, anatambua kwamba siyo tu akili yake, bali hata roho yake, vinavyopaswa kumdhahirisha Kristo kwa jirani yake.

Wiki hii, Lee kwa msisimko alikuja kwa Jia. Kutoka kwenye mtandao, alikuwa amepata orodha ya mambo kumi ya "kuwachanganya Wakristo." Mtandao unasema, "Hakuna Mkristo atakayeweza kujibu maswali haya. Maswali haya yatadhihirisha kwamba Biblia haiwezi kuaminika."

Lee akasema, "Jia, nina swalii la kukuuliza. Unasema kwamba Biblia ni neno la Mungu na haliwezi kuwa na makosa. Katika Marko 15:25 panasema kwamba Yesu alisulibiwa kwenye muda wa saa tatu, yaani 03:00 asubuhi. Yohana 19:14 anaelezea kwamba Pilato hakuwahi kuitoa hukumu yake hadi ilipofika saa sita, yaani 06:00 mchana. Kama Biblia ni Neno la Mungu, kwa nini aya hizi zinapingana?

► Kama Jia atakuja kwako kwa msaada, utamjibuje? Utakuwa na wasiwasi kwamba Lee amepata kosa katika Biblia? Je, unafikiri kwamba ni muhimu kuwa na uwezo wa kuitetea imani yako?

Elimu ya Kuitetea Imani ni nini?

Kariri ufanuzi huu wa Elimu ya kuitetea imani ya Kikristo: **Elimu ya kuitetea imani ya Kikristo ni kuwasilisha ushahidi unaothibitisha ukweli wa Imani ya Kikristo.**

D. James Kennedy alishawishika kuandika kitabu kinachohusiana na elimu ya kuitetea imani baada ya kusikia mahojiano kwenye radio. Mtayarishaji wa kipindi alikuwa anamhoji mtu asiyeamini kwamba Mungu yupo. Kennedy anashuhudia:

Wakati nikiwa na hofu nikawa najaribu kupiga simu kwenda katika kituo kile, nilisikia zaidi ya watu Wakristo waliokuwa wakipiga simu wakitaka kuzungumza na huyu mtu. Ilionekana kwamba kila Mkristo aliye kujibu akipiga simu alikuwa hana uwezo wa kutoa sababu za kwa nini ana imani aliyo nayo. Kila aliye piga simu alikuwa anaanza na, "Biblia inasema..." Yule kafiri akawa anajibu, "Kwanini unai amini Biblia?" Kila mmoja alijikuta anakwama akisema maneno kama, "Sawa, nimeiweka moyoni mwangu."

Yule kafiri naye akawajibu, "Sawa, kwangu mimi haikuwa ndani ya moyo wangu, kwa hiyo siwezi kuiamini."¹

► Utamjibuje huyu kafiri?

Katika kozi hii, utajifunza majibu ya maswali kama yafuatayo:

- Je, tunaweza kujua kama Mungu yupo?
- Vipi kuhusu tatizo la kuteseka na uovu vilivyopo katika dunia?
- Uumbaji unatufundisha nini kuhusiana na Mungu?
- Je, Agano Jipya ni la kuaminika?
- Je, unabii kuhusiana na Masihi katika Agano la kale umetimia katika Yesu?
- Je, ni kweli kwamba Yesu alifufuka katika wafu?
- Je, Ukristo ndio njia pekee ya kwenda mbinguni?
- Utatu Mtakatifu ni nini?
- Wakristo wataitikaje kuhusu imani ya kwamba vitu vyote (miti, mawe upemo n.k.) vina roho?
- Ni nini kinaenda kutokea kwa wale watu ambao hawajawahi kabisa kuisikia Injili?

Kwa nini tujifunze Elimu ya kuitetea Imani?

Elimu ya kuitetea imani ni muhimu wakati tunafanya *Uinjilisti* na baada ya *kufanya Uinjilisti*. Wakati tunafanya *Uinjilisti* ni pale tunapomsaidia mtu kuja karibu na kutaka kumpa Kristo maisha yake. Mkristo anaweza kutumia elimu ya kuitetea imani katika kuondoa vizuizi vyote vya ujuzi na elimu vilivyoko kwenye njia ya mtu ambaye anataka kuipokea imani. *Baada ya Uinjilisti* ni yale yanayofanyika katika kuwasaidia Wakristo kuwa na nguvu katika imani yao baada ya kuwa wameokoka na kuipokea imani.

Kwa nini elimu ya kuitetea imani ni muhimu *tunapofanya uinjilisti?* **Ni kwa sababu watu wengi huja kwa Kristo baada ya kujifunza ushahidi wa ukweli uliopo kuhusiana na Ukristo.**

C.S. Lewis hakuamini kwamba Mungu yupo, alikuja kugeuka kuwa Mkristo baada ya kugundua kwamba Ukristo ni wa kweli. Akizungumzia maisha yake kama kafiri, C.S. Lewis alisema, "Nilikuwa najidhania nimewamaliza Wakristo kabisa." Lakini "kwa kijana anayetaka kubakia kweye ukafiri kikamilifu hawezi kuwa makini vya kutosha katika kusoma kwake. Kuna mitego mingi kila mahali...."

¹ D. James Kennedy. *Why I Believe*. (Nashville: Thomas Nelson, 1999), 13

Ushahidi kuhusiana na Ukristo ulikuwa wa kuvutia sana kiasi kwamba Lewis hakuweza kuukwepa. Alisema kwamba alifikishwa mahali pa kuamini kwamba Mungu yupo, "akijaribu kupuuzia, kushindana, kukasirika na akipepesa macho yake huku na kule ili apate mahali pa kutorokea." Mungu alipofanya kazi katika maisha ya Lewis, akawa Mkristo aliyejitoa kabisa na akaiita historia yake ya kuokoka kama ni *Surprised by Joy ("Kushangazwa kwa furaha."*)

Josh McDowell naye alikuwa ni mtu aliyekuwa na mashaka mengi akiukanusha sana Ukristo. Alikuja kugundua kwamba ushahidi unaelemea upande wa ukweli wa Ukristo. McDowell alibadili imani yake potofu na kuwa Mkristo, na aliandika kitabu, *Ushahidi ambao Unahitaji Uamuzi*, kwa lengo la kuthibitisha ukweli wa imani ya Kikristo.

Lee Strobel, mwandishi wa kitabu kiitwacho *The Case for Christ (Shauri la Kristo)*, alikuwa kafiri aliyekuja kuwa Mkristo baada ya kujifunza ushahidi wa Ukristo. Mojawapo ya vitabu alivuosoma ni kile kilichokuwa kimeandikwa *Evidence that Demands a Verdict ("Ushahidi ambao Unahitaji Uamuzi")*.

Elimu ya kuitetea imani ni chombo muhimu sana kwa matokea makubwa katika Uinjilisti wa wakati uliopo. Tunapowakilisha elimu ya kuitetea imani kwa mtu ambaye haamini kabisa kwamba Ukristo ni wa kweli, tunaweza kuondoa vizuizi vya ufahamu na ujuzi vinavyomzua katika kuiamini Injili. Kwa njia hii, elimu ya kuitetea imani inaweza kukusaidia katika kuishirikisha imani yako.

Elimu ya kuitetea imani pia inasaidia baada ya Uinjilisti. Elimu ya kuitetea imani haitakusaidia tu katika kuishirikisha imani yako kwa watu wengine, lakini pia itaimarisha imani yako na imani ya watu wengine. Hii ndio inayomaanisha, 'baada ya Uinjilisti.' Kwa nini elimu ya kuitetea imani ni muhimu kwenye wakati wa 'baada ya Uinjilisti'? **Kujua ni kwa nini umeamini kutakufanya uwe na nguvu katika imani ya Kikristo.**

Hata watu wengi wanaojitambulisha kuwa wamezaliwa mara ya pili hujikuta wakifiri kwamba haijalishi mtu yuko katika dini gani kwa sababu imani zote zinafundisha masomo yale yale yanayohusiana na maisha. Wakristo wengi hawajajua ni kwa nini wanaamini kile wanachokiamini. Wako wazi kudhuriwa na mashambulizi ya kuharibu imani kutoka kwa watu waliojaa mashaka na wasiwasi. Kujifunza elimu ya kuitetea imani kutakuandaa kujibu maswali ya watu wenye mashaka wanaojaribu kuivuruga na kuisambaratisha imani yako.

Je, uelewa wa elimu ya kuitetea imani ni lazima kwa mtu ili aweze kuamini katika Kristo? Hapana. Wako Wakristo wengi ambao walimwamini Kristo hata kabla hawajajua historia na ushahidi wa kisayansi unaounga mkono usahihi wa Biblia. Pia bado inawezekana watu hawa hawa wakachanganyikiwa na uongo wa Shetani anaowaambia baadaye kuhusiana na Yesu. Shetani anataka awapokonye imani wale ambao wameweka tumaini lao kwa Kristo. Hiyo ndiyo sababu mojawapo ya kwa nini ni muhimu sana kujifunza sababu thabiti zenye akili kuhusiana na imani.

Ni mahali gani kwenye Maandiko imeamriwa kwamba tutumie Elimu ya kuitetea Imani?

Sababu kubwa inayotufanya tujifunze elimu ya kuitetea imani ni kwamba Biblia ianatureleza kuwa ni lazima wakati wote tayari kuitetea imani yetu. Mtume, Petro aliandika:

Bali mtakaseni Kristo Bwana moyoni mwenu, mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu.²

Jina la Kigiriki linalohusiana na "kutetea" ni *apologia*. Katika Ugiriki ya zamani, neno *apologia* limehusishwa katika kumtetea mtu aliyeshitakiwa mahakamani. Mlalamikaji atawakilisha malalamiko yake (*categoria*). Kisha mlalamikiwa atawakilisha utetezi wake (*apologia*).

Katika 1 Petro 3:15 panajibu maswali matatu kuhusiana na elimu ya kuitetea imani.

1. Kuna haja yejote ya kutumia elimu ya kuitetea imani? **Ndiyo, Wakristo wanapaswa wakati wote wawe tayari kutoa utetezi na maelezo yeny sababu za sisi kuwa na imani ya Kikristo.**
2. Tuwafikie nani kwa elimu ya kuitetea imani? **Mtu yejote anayehoji sababu za sisi kuwa na imani ya Kikristo.**
3. Tuiwasilisheje elimu ya kuitetea imani? **Kwa upole na heshima.**

Mbali na maagizo haya, je, Biblia yenyewe inatoa mwongozo wowote kuhusiana na matumizi ya elimu ya kuitetea imani? Ndiyo. Kwa mfano, Luka anerejea "shahidi nyingi zisizokuwa na shaka" ambazo Yesu alizitumia kuthibitisha kwamba angekuwa hai baada ya kufufuka (Matendo 1:3). Pia katika kitabu cha Matendo 17 kinatuambia kwamba Paulo, wakati akiwa Athene, alizungumza kupitia madhabahu za Wagiriki za "miungu isiyojulikana" katika kuwakilisha suala la Ukristo, Waandishi wa Biblia walihakikisha wasomaji wao wanaelewa kwamba madai yao waliyokuwa wanayatoa yanashikamana kabisa na ukweli.

Ni wakati gani tunapaswa kuwakilisha elimu ya kuitetea imani?

► Ni wakati gani tunapaswa kuwakilisha elimu ya kuitetea imani? Tuiwakilishe kabla au baada ya kuwakilisha Injili?

Sheria ya ujumla ni hii: Wakati unaposhirikisha imani yako kwa mtu mwingine, **wakilisha injili kwanza**. Kisha, kama itahitajika, **tumia elimu ya kuitetea imani kuunga mkono** injili iliyowakilishwa.

Kuna mambo ya pekee ya kuangaliwa katika sheria hii. Kwa mfano, mara nyingine unaweza kuwa unahitajika kutumia mada yeny elimu ya kuitetea imani katika kuwakilisha ujumbe wa Biblia. Kumbuka kwamba Injili ndiyo muhimu kwanza. Tumia elimu ya kuitetea imani

² 1 Petro 3:14-15

kama watu wataleta upinzani au kama endapo kwa kuitumia elimu ya kuitetea imani kutatoa nafasi nzuri ya kuwakilisha Injili.

Injili ni nini?

Kwa kuwa Injili ndio msingi mkuu wetu wa ujumbe, ni muhimu kuwa na uelewa mzuri wa Injili. Kitabu cha 1 Wakorintho 15:1-4 kinatoa muhtasari wa "habari njema."

- Kristo alikuwa kwa ajili ya dhambi zetu.
- Alizikwa.
- Alifufuka na akajionyesha tena kwa watu wengi akiwa hai.

Maandiko mengine yanaonyesha matokeo ya kifo na ufufuko wa mwili wa Kristo:

- Tunaweza kuwa na msamaha na utakaso wa dhambi.³
- Tunaweza kuchukuliwa kama watoto wa familia ya Mungu na kukaa na Roho wa Mungu.⁴
- Tunao uwezo wa kuishi maisha ya utakatifu na kumpendeza Mungu.⁵
- Tutakuwa na mwili mpya wa ufufuo wa kuishi milele pamoja na Kristo katika mbingu mpya na nchi mpya.⁶

Huu hapa ni muhtasari wa habari njema: Injili ni habari njema ambazo tunaweza kuokolewa kwa imani kupitia kwa mwanadamu Kristo aliyekufa na kufufuka. Kuuelezea ujumbe huu wa Injili kwa mtu mwingine, hapa kuna mbinu iliyofanyiwa majaribio kwa muda:

Msingi mkuu wa ujumbe wa Biblia⁷

Anza kwa kuwa uliza watu ni nini msingi mkuu wa Biblia. Thibitisha majibu yao, kisha useme, "Je ninaweza kuwaonyesha picha ya mchoro inayoonyesha kile ninachokiona mimi kuwa ni msingi wa ujumbe wa Biblia?"

Kama watakuruhusu, sema yafuatayo wakati ukiwa unachora mchoro, (ongeza takwimu, maumbo, na maneno unapokuwa kwanza ukielezea maana zinazoambatana nazo).

³ Waebrania 9:22

⁴ Wagalatia 4:4-6

⁵ Waebrania 13:12, 20-21

⁶ Wafilipi 3:20-21.

⁷ Unaweza kupakua program ya bure ya uwakilishaji wa injili kutoka www.answersingenesis.org/go/defending-your-faith. Bofya kwenye kiungo "Kwa ujumbe wa Msingi wa Biblia" kupakua uwakilishwaji huu.

Msingi wa kwanza wa Biblia ni huu: **Mungu** alituumba **sisi**, kama familia ya kibinadamu, tuwe na uhusiano wa **upendo** mtakatifu na yeye. Lakini **tumetenda dhambi**, na dhambi yetu ikatupekeea ufa mkubwa kati yetu na Mungu. Biblia inauita utengano huo kama **kifo**. Kwa ukweli, kama tukifa kifo cha kawaida wakati huo huo tukiwa tumekufa kiroho, tutatengwa milele na Mungu mahali panapoitwa **Kuzimu**. Hizi ndizo habari mbaya za Biblia.

Habari njema ni kwamba Mungu anatupenda na hapendi tuende Jehanamu. (Yohana 3:16). Mungu Baba alimtuma Mungu Mwana, Yesu, duniani kuja kufa msalabani, na afufuke kutoka kwa wafu, ili ushirika wetu na Mungu uweze kurejeshwa.

Sasa kama **tutatubu** – kama tutageuka kabisa katika dhambi zetu (Matendo 3:19) – na kama **tutampokea** Kristo katika miyo na maisha yetu – tukimwamini yeye atatusamehe sisi (Yohana 1:12) – ndipo mara moja tunatoka mautini kuingia uzimani, (tutakuwa tumelivuka daraja). Tutaingia kwenye uhusiano na Mungu, na kufanyika kuwa uzao mpya. Mwisho wa yote, wale wote wanaomwamini Kristo pekee yake kwa ukombozi wake wataingia **mbinguni** kwa ajili ya kuishi kwenye maisha ya umilele ya ushirika wa furaha na Mungu pamoja na wale wote watakaokuwa wanamjua Mungu kwa usahihi.

Huo ndio msingi mkuu wa Biblia. Naweza kukuuliza...

- Wewe unajiona uko wapi katika mchoro huu?
- Unataka uwe wapi?
- Kuna kizuizi chochote kinachokuzuia usiweze kuchukua hatua sasa hivi?

Nani anayehitaji elimu ya kuitetea Injili?


Kila Mkristo anatakiwa kujua ni kwa nini ameamin. Kila Mkristo anahitaji kufahamu misingi ya imani yake.

Vipi kuhusiana na wasioamini? Ni nini jukumu la msingi la elimu ya kuitetea imani kwa wasioamini? Kwa mujibu wa Josh McDowell, kuna sababu tatu za watu kumkataa Kristo:

- Ujinga (mara nyingi huu ni ujinga wa kujitakia)
- Kiburi
- Matatizo ya maadili.

"Katika vita, kusudi kubwa ni kumshinda mpinzani wako. Katika uinjilisti, kusudi kubwa ni kuwashawishi wengine." -Ravi Zakaria

Kuna watu wengi ambao wana mashaka ya akili kuhusiana na ukweli wa Ukristo. Tatizo la hawa watu ni ujinga wao katika kuijua imani ya Kikristo. Watu hawa wanahitaji elimu ya kuitetea imani.



Watu hawa wanaleta upinzani wa kiakili kama udhuru wa kuepuka kukubali sababu zinazowafanya wasikubali kuamini. Watu hawa wanaweza kuwa ni wenye kiburi au wana dhambi ambazo hawataki kuachana nazo. Tunapaswa tutambue ni sababu gani za msingi zinazowafanya watu hawa wamkatae Kristo na kukabiliana nao katika hali yao ya ukweli wa dhambi zao na kiburi chao. Hata hivyo, tunapaswa kushughulikia upinzani wao wa kiakili. Mara nyingi watu hawa wanahitaji majibu ya upinzani wao wa kiakili kabla hawajatambua sababu zao za kumkataa Kristo. Kwa sababu ya hili, kila mtu anayeanzisha upinzani wa kiakili anahitaji elimu ya kuitetea imani, bila kujali uzito wowote wa sababu zake alizo nazo za upinzani.

Elimu ya kuitetea Imani katika vitendo – Kuongoka kwa C.S. Lewis (1898-1963)

C.S. Lewis alizaliwa kwenye familia ya Kikristo nchini Ireland. Babu wa baba yake alikuwa mtumishi katika dhehebu la Wamethodisti, na babu yake alikuwa mwamini wa dhehebu la Anglikana. Hata hivyo, baada ya mama yake kufa kwa ugonjwa wa saratani, Lewis alifikia uamuzi kwamba Mungu alikuwa Mungu mkatili sana. Akiwa katika umri wa miaka kumi na tatu, Lewis alijiamulia kuwa mtu asiyeamini kwamba Mungu yupo (kafiri).

Lewis alikuwa mwanafunzi mwenye akili sana katika fani ya fasihi kwenye Chuo kikuu cha Oxford. Baada ya kuhitimu mafunzo yake, alikuja kuwa mmoja katika wakufunzi maarufu sana wa fasihi katika Chuo cha Magdalena, Oxford. Watu wawili maarufu sana waliokuwa marafiki wa Lewis katika kitivo cha Kiingereza, Hugo Dyson na J.R.R. Tolkien, walikuwa Wakristo. Kupitia majadiliano kati ya watu hawa na masomo yake mwenyewe, Lewis aligundua ukosefu wa akili uliokuweko katika kuamini kwamba hakuna Mungu.

Mwaka 1929, Lewis aliweza kukiri ukweli kuhusu uwepo wa Mungu, na akawa "mtu anayesita kuokoka katika Uingereza yote." Katika eneo hili, ndipo Lewis alipokiri hadharani kuhusu ukweli kwamba "kuna Mungu," lakini bado alikuwa hajageuka kuwa Mkristo. Elimu ya kuitetea imani iliishawishi akili ya Lewis kuhusu uwepo wa Mungu; lakini injili ilikuwa bado haijafanikiwa kuubadilisha moyo wake.

Miaka miwili baadaye, C.S. Lewis alijisalimisha kwa Kristo. Wakati huu, Lewis alikuwa na mabadiliko ya kweli ya moyo wake, siyo tu kwa akili zake kukubali kwamba Mungu yupo, bali hata kwa moyo wake. Lewis hakuwa tena "mtu wa kusita." Sasa alikuwa "aliyeshangazwa kwa furaha," na aliyemfuata Yesu Kristo kwa hiari yake mwenyewe.

Lewis alitokea kuwa mmoja wa waandishi maarufu sana wa Kikristo wa karne ya ishirini. Aliandika vitabu ishirini na tano akigusia mambo mengi sana yanayohusiana na imani ya Kikristo. Katika kipindi cha kuongezeka kwa maoni kwamba dini isiwe msingi wa elimu na maadili, Lewis alikuwa mtetezi aliyebobeaa wa imani ya Kikristo.

Kuongoka kwa Lewis kunadhihirisha uhusiano mkubwa uliopo kati ya elimu ya kuitetea imani na uinjilisti. Baada ya kifo cha mama yake, alikuwa na maswali ya kiakili kuhusiana na uwepo wa Mungu. Lewis hakuwa na uwezo wa kuoanisha Mungu wa upendo na mateso

ya dunia hii. Kabla ya masikio yake kufunguka kwa ajili ya injili, Lewis alihitajika apate majibu ya maswali na hoja zake.

Elimu ya kuitetea imani ilimleta Lewis kwenye mahali kamili pa kuamini kwamba Mungu yupo; Injili ilimleta kwenye furaha ya uhusiano na Mungu. Ingawaje kimsingi Injili inapaswa ihubiriwe kwanza, kuongoka kwa C.S.Lewis kunaonyesha kwamba elimu ya kuitetea imani, mara nyingine ni muhimu itumike kwanza kwa ajili ya kuandaa upenyo kwa ajili ya Injili.

Je, elimu ya kuitetea Imani ina upungufu gani?

Elimu ya kuitetea imani yenye haiwezi kumleta mtu yeote kwa Kristo. Mungu huyafungua macho ya wale amba ni vipofu wa kiroho. Hata hivyo, Roho Mtakatifu huitumia elimu ya kuitetea imani kama njia ya kuwasaidia watu wengine kumtafuta Yesu. Tunapaswa tuombe kwamba Mungu atumie maelezo tunayoshirikishana na watu wengine yasaidie katika kuwafungua macho yao ya kiroho.

Kwa maana ni Neno la Mungu tu (lenye ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili) linaloweza kupenyeza ndani ya moyo wa mtu mpotevu likamwamsha hata kumfanya amhitaji Kristo.⁸ Ndiyo, hatuhitaji hatuwezi kusema tu kuwa Maandiko kuwasaidia watu wawe na imani kubwa na kwamba wanaweza kuamini kile wanachokisoma katika Biblia, lakini pia ni lazima tuweke akilini kwamba Biblia yenye inajithibitisha.

Inamaanisha nini kusema “Biblia yenye inajithibitisha?” Kwa kuwa Biblia ni Neno la Mungu, linaishi na lina nguvu. Biblia yenye inasema na mioyo yetu kuhusu ukweli wake. Miyo yetu inatambua ukweli wa Neno la Mungu.

Kwa kuwa Neno la Mungu linajithibitisha lenyewe, watu wengi wanakuja kwa Kristo bila hata ya kujua hoja za ushindani kuhusiana na Ukristo. Wanakuwa wameshautambua ukweli wa Biblia mapema kabisa kabla ya kukutana na sababu za kiakili zinazotaka kupenyeza kwenye imani yao.

Kwa kipindi chote cha historia, Wakristo katika maeneo yote ya kijamii, kwa hiari yao wenye weamekuwa tayari kufa kwa ajili ya injili. Mionganini mwa hawa ni wasomi wa viwango vya juu sana; na wengine hawajui hata kusoma. Lakini imani yao haikuwahi kutikisika. Uhakika na ujasiri wao ulitoka wapi? Haukuja tu kwa uwezo wa asili au kwa hoja za kiakili bali kwa mafunuo ya Roho Mtakatifu “kwenye macho ya moyo.”⁹

Kuna njia mbili za kuona. Tunaona kwa macho ya mwili, na tunaona kwa macho ya kiroho. Watu wengi huwa kwanza wanafahamu kwamba Biblia ni Neno la Mungu kwa sababu wakati wanapolisoma au wanaposikia likisomwa, Mungu huudhihirisha utukufu wake ndani ya mioyo yao.

⁸ Waebrania 4:12

⁹ 1 Wakorintho 2:14; Waefeso 1:19

Ushuhuda wa Mchungaji wa Kifilipino

Mchungaji mmoja katika nyanda za juu za nchi ya Ufilipino alizaliwa katika kabila la wapagani. Baba yake alikuwa "kuhani" aliyeendesha ibada za mizimu za kikabila. Siku moja, huyu kijana alipewa kitabu cha Agano jipya kilichokuwa kimeandikwa kwa lugha yao ya asili. Alianza kusoma – na hakuacha kuendelea kusoma!

Alijua kwamba kitabu hiki kilikuwa cha kweli ingawaje hakuweza kuelezea ni kwa namna gani. Alipokuja kwenye maelezo ya kusulubiwa, alianza kulia. Alikuwa amesoma habari za kifo cha Yesu kwa mara ya kwanza. Akasema, "Nilipokuwa nikisoma, nilijisikia kana kwamba moyo wangu umekuwa wazi, na nikalia kumwambia Mungu aniomkoe! Baada ya hapo nilijisikia nimekuwa msafi!"

Ni kwa jinsi gani Mungu huudhihirisha Utukufu wake?

Yohana Piper anaorodhesha njia ambazo Mungu huwapa watu wake macho ya kiroho.¹⁰

Mungu huudhihirisha Utukufu wake kupitia Uumbaji

Mtume Paulo aliandika kwamba, "uweza wake wa milele na tabia ya Uungu ulionekana wazi tangu kuumbwa kwa ulimwengu, kwa mambo ambayo yanaonekana." Wanadamu wote wamepewa macho ya kiroho ya kuuona utukufu wa Mungu kupitia ulimwengu aliouumba, hata wasiwe na udhuru.¹¹ Kuwaelekeza watu jinsi uumbaji unavyodhihirisha kazi njema ya mikono ya Mungu ni aina ya elimu ya kuitetea imani.

Mungu huudhihirisha Utukufu wake katika Ubinadamu na Kujitoa Sadaka kwa Yesu Kristo

Kwa wale wanaojitoa kwa hiari yao wenyewe kumpokea Kristo, Mungu kwa njia isiyokuwa ya kawaida hufungua macho ya miyo yao kwa ajili ya kuuona utukufu wake na kuwa na uhakika kwamba yeche ndiye anayetaka wawe kama atakavyo.¹²

Mungu amejidhihirisha mwenyewe kwa watu wake. "Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa."¹³ Kwa masikitiko, watu wengi huikataa neema yake na kuendelea kubakia vipofu. Wanaume kwa wanawake wanaokataa kuona huendelea kubakia vipofu hadi mwisho. Lakini kwa wale ambao kwa hiari yao wenyewe wako tayari kuona, Mungu huudhihirisha zaidi na zaidi utukufu wake na neema yake ya ukombozi.

► Soma Mathayo 13:13 na Yohana 9:39. Ni kwa jinsi gani inawezekana kuona au kutokuona, na kusikia au kutokusikia? Jadilianeni majibu yenu katika kikundi.

¹⁰ Nyenzo hii imechukuliwa kutoka katika mahubiri ya John Piper, "God's Peculiar Glory: How We Know the Bible Is True" (Houston, Texas, April 28, 2016). Imenyonywa kutoka: <http://www.desiringgod.org/messages/gods-peculiar-glory> April 11, 2020.

¹¹ Zaburi 19; Warumi 1:19-21

¹² Waefeso 1:19

¹³ Tito 2:11

Mungu huudhihirisha Utukufu wake kupitia Injili.

Katika kitabu cha 2 Wakorintho 4:6, Paulo anatoa kauli hii ya kushangaza!

Kwa kuwa Mungu, aliyesema, Nuru itang'aa toka gizani, ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo.

Kama vile Mungu alivyo sema, "Iwe nuru" wakati wa uumbaji, anaagiza nuru ya kiroho iangaze kwa kila moyo ulio tayari kupokea ili tujuue kwamba Yesu na Injili ni dhahiri. Mungu huzungumza kupitia katika Injili ili kujidhihirisha mwenyewe kwa kila mtu anayetaka kuona.

Mungu huudhihirisha Utukufu wake kupitia Maisha na Shuhuda za Walioamini.

Tumesoma hapo juu kwamba, "neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa." Hata kabla ya hapo, Paulo anatoa kauli nyingine tata. Paulo anamwandikia Tito, mchungaji kijana katika kisiwa cha Krete. Paulo anasema kwamba Tito ni lazima afundishe Wakristo jinsi ya kuishi maisha ya kimungu "ili wayapambe mafundisho ya Mwokozi wetu Mungu katika mambo yote."¹⁴ Maisha na Shuhuda za walioamini huifanya Injili iwe kivutio. Mungu huzungumza na mioyo ya watu wasioamini kupitia maisha ya Wakristo walioamini na ambao ni waaminifu. *Maisha matakatifu ya Wakristo ni tunu muhimu sana ya elimu ya kuitetea imani.*

Ushuhuda wa Mchina aliye kuwa ame amini

Daudi alishakusudia tangu mwanzo katika maisha yake kuwa mtu anaye amini kwamba hakuna Mungu. Lakini kama kijana mdogo aliye kuwa bado anatafuta maisha, alianza kujifanya majaribio kwa kushiriki katika dini mbalimbali. Alijiunga na dini ya wabudha, akona hakufai. Baadaye akaanza kujifundisha maandiko ya Wakonfishasi, lakini hakuweza kupata amani ya ndani.

Wakati mmoja, Daudi alijaribu kuanza kuisoma Biblia. Lakini alipofikia kwenye maelezo yaliyohusu gharika, aliifunga Biblia kwa hasira. Wazo la Mungu kuingamiza dunia kwa gharika lilimuudhi sana. Daudi akasema, "Nilishakusudia tangu mwanzo kutokuwa Mkristo. Singeweza kamwe kumwamini mungu wa visasi ambaye amekusudia kuleta vifo na maafa makubwa hivyo kwa wanadamu!"

Miaka michache baadaye, Daudi akajiunga katika darasa la kusoma Kiingereza katika Chuo Kikuu kimoja cha Wachina. Mwalimu wake alikuwa profesa kijana wa Kikristo kutoka Marekani.

"Huyu profesa kijana alikuwa na tahadhari sana katika kushirikisha Injili yake," Daudi alisema. "Alijua kwamba alikuwa anachunguzwa kwa umakini mkubwa na mamlaka za utawala, kwa hiyo hakuwahi kushuhudia darasani, ingawaje alimjua kwamba ni Mkristo." Lakini ilikuwa ni furaha iliyoniibua mimi. Sijawahi kukutana na mtu aliye kuwa na furaha

¹⁴ Tito 2:10

kama huyo! Tutamkuta maeneo ya chuo akipiga gitaa na kuimba, na akifanya hivyo kwa Amani. Ilibidi nitafute kufahamu furaha yake yote hiyo inatoka wapi.

"Kwa kutumia lugha ya Kichina iliyovunjika sana, alinishirikisha mpango wa ukombozi. Mara nyingine alipokuwa akisoma, nilikuwa tu nauamini ujumbe, na alijua mara moja kwamba jambo fulani la muujiza na la ajabu limetokea kwangu! Nilijisikia kana kwamba dunia yote imebadilika! Niliangalia nje ya dirisha la makazi yake niakona maua kana kwamba ndioya nayaona kwa mara ya kwanza. Yalionekana yanayong'ara sana. Ndipo nilipotambua kwamba siyo dunia iliyokuwa imebadilika. Mabadiliko yalikuwa yametokea ndani ya moyo wangu!"

Mungu aliyatumia maisha ya Mkristo kuudhihirisha utukufu wake kwa moyo wa Daudi uliokuwa na njaa. Kijana mdogo profesa Mkristo "alipambwa na mafundisho ya Mungu" kuititia maisha yake ya furaha ya Ukristo.

Hitimisho

Jia alimsimamisha Lee na kusema, "Je, ninaweza kuzungumza nawe kwa dakika chache? Ninaweza nikawa na jibu la swali lako kuhusiana na tofauti ya muda wa kusulubiwa kati ya Marko na Yohana."

Lee alishangaa. "Unategemea kabisa kujaminisha katika kitabu chako hicho cha dini kwa ajili ya kujibu swali langu? Sikuwa nimefikiria kwamba Wakristo wanapenda maswali! Nilifikiria kwamba Wakristo huwa wanafunga akili na macho yao kwenye ukweli. Lakini sasa endelea kuniambia; umegundua nini?"

Jia alimwonyesha Lee alichokipata kutoka katika mafafanuzi ya Biblia. Swali la Lee, kama yalivyo maswali mengi kuhusiana na Biblia, yanaweza kujibiwa kwa kuzingatia mazingira ya kihistoria. Jia akasema, "Injili ya Marko iliandikwa kati ya mwaka 45 na 65 B.K. Kwenye miaka hiyo, Wayahudi walikuwa na utaratibu wao wenyewe wa kuhesabu muda. Waliianza siku majira ya saa 12 asubuhi. Bila shaka Marko alitumia utaratibu wa muda wa Wayahudi katika Injili yake. Wakati katika Marko 15:25 panasema kwamba Yesu alisulubishwa saa ya tatu katika siku, ikimaanisha alisulubishwa saa 3 asubuhi.

"Hilo ndilo nililolisema," Lee aliingilia, akasema, "Marko anasema saa 3 asubuhi, lakini Yohana anasema saa 6 mchana. Mmojawapo ana makosa!

Jia alicheka na polepole akasema, "Yohana kwa uhakika hajasema Yesu alikuwa mbele ya Pilato saa 6 mchana. Alisema ni katika saa ya sita ya siku. Yohana aliandika kitabu chake cha Injili baadaye kuliko Marko. Alikuwa anaandika yumkini kutoka Efeso, iliyokuwa koloni la Kirumi. Ushawishi wa Warumi ulikuwa mkubwa sana wakati huo, katika ulimwengu wa Mataifa. Warumi waliianza siku yao mpya saa sita za usiku wa manane. Kwa hiyo kama Yohana alikuwa anatumia utaratibu wa saa za Kirumi, katika Yohana 19:14, saa ya sita itakuwa ni saa 12 asubuhi.

"Kwa pamoja, Injili hizi mbili zinatuonyesha taarifa kuhusu kuhukumiwa kwa Yesu na kusulubiwa. Yohana anatuonyesha kwamba Yesu alihukumiwa na Pilato saa 12 asubuhi (saa ya sita ya siku) baada ya uendeshwaji wa mashitaka na kuhukumiwa wakati huo wa usiku. Hukumu hiyo ya usiku wala haikuwa ya kisheria! Yesu alihukumiwa pasipo kuzingatia haki. Kisha Marko akaonyesha kwamba, masaa matatu baadaye, hukumu ya Pilato ilitekelezwa. Yesu alisulubiwa saa 3 asubuhi. Na, Lee, Yesu alisulubiwa kwa kutokuwa na kosa lolote. Hata Pilato alisema, "Sioni kosa lolote juu ya mtu huyu." Yesu alisulubiwa kwa ajili ya dhambi zako na zangu. Alikufa ili wewe na mimi tuweze kuishi milele."

Kazi za kufanya Somo la 1

(1) Elimu ya kuitetea imani na kichwa: Utaanza kipindi kinachofuata kwa kufanya mtihani kutoka katika tafakuri za Somo la 1. Yasome maswali haya kwa makini sana kwa ajili ya maandalizi ya mtihani.

(2) Elimu ya kuitetea imani na Moyo: Mshukuru Mungu kwa kujidhihirisha mwenyewe kwako. Mshukuru kwa kukuondolea vizuizi vilivyokuwa vimefunga akili yako ili usiujue ukweli. Fikiri juu ya mtu ambaye kuitia maisha yake aliudhihirisha Ukristo wa kweli kwako. Mwandikie au umwite mtu huyo ili uonyeshe shukrani zako kwake.

(3) Elimu ya kuitetea imani na Mikono: Uliza watu wasioamini (angalau mmoja) kama unaweza kuwahoji kuhusiana na mtazamo wao wa kidunia au mfumo wa imani. Kama watakuwa wako tayari, unaweza ukauliza, "Mnawenza kujibu maswali matatu muhimu ya falsafa ya maisha? Maswali haya matatu ni: Mimi nimetoka wapi? Kwa nini niko hapa? Ninaelekea wapi? Haya ni maswali yanayohusiana na asili ya maisha, kusudi la kuwepo kwetu, na kutatokea nini tukisha kufa. Waulize ni kwa nini wanaamini na wanaamini nini. Waulize kama watakuwa tayari kuendelea na mazungumzo na wewe tena utakapokuwa unaendelea na kozi hii. Nukuu mahali yale unayohojiana nao kwa ajili ya kulishirikisha darasa kwenye kipindi cha darasa kinachofuata.

Mtihani wa Somo la 1

- (1) Je, ni nini ufanuzi wa Elimu ya kuitetea imani ya Kikristo?
- (2) Kwa nini tunasema elimu ya kuitetea Injili ni muhimu wakati wa kufanya Uinjilisti?
- (3) Kwa nini tunasema elimu ya kuitetea imani ni muhimu baada ya Uinjilisti?
- (4) Ni aya gani katika Agano Jipya inayoonyesha kwamba kuna hitaji la kutumia elimu ya kuitetea imani? Inukuu aya hiyo.
- (5) Kuna maswali mangapi yanayoulizwa kuhusu elimu ya kuitetea imani katika 1 Petro 3:15?
- (6) Unapokuwa unashirikisha wengine imani yako, ni kipi kianze kwanza, injili au elimu ya kuitetea imani? Kwa nini?
- (7) Kuna sababu ngapi tatu za watu kuukataa Ukristo?
- (8) Kwa nini ni lazima tujibu upinzani wa kiakili hata kwa watu ambao wana sababu za ndani kabisa za kutoamini?
- (9) Ni mtu gani anayefungua macho ya wale ambao kiroho ni vipofu?
- (10) Ni kwa jinsi gani Roho Mtakatifu anaitumia elimu ya kuitetea imani kuwaleta watu kwenye imani katika Kristo?
- (11) Inamaanisha nini kwa kusema kwamba maandiko yanajithibitisha yenyewe?
- (12) Orodhesha mambo manne ambayo Mungu huyatumia kuudhirisha utukufu wake kwenye macho ya kiroho ya moyo.

Somo la 2

Dhana potofu dhidi ya Elimu ya Kuitetea Imani

Utangulizi

"Jia, nina swalii la kukuuliza wewe!" Msichana Jia aligeuka na kumkuta kijana Lee akipunga mkono kutoka kwenye makazi yake anayoishi. Msichana akaanza kuwa na mashaka, "Je, ninaweza kujibu swalii la huyu kijana.? Mwenyewe nimekuwa Mkristo muda siyo mrefu uliopita. Itakuwaje kama atanisababisha nianze kuwa na mashaka na imani yangu mpya?

Lakini Jia anaamini linalopaswa kuwa kwa Wakristo, "Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu."¹⁵ Kwa hiyo alicheka na kusema, "Lee, swalii lako ni nini?"

"Wiki lililopita, ulinieleza kuhusu tofauti kati ya Marko a Yohana. Ninakiri kwamba jibu lako lilikuwa zuri sana! Sikuwa nimejua kabisa kuhusu tofauti iliyokuwepo katika kuhesabu muda. Lakini, unawezaje kuthibitisha kwamba maelezo kuhusu Yesu ni ya kweli? Inawezekana mambo yote yamebuniwa tu. Mimi ni mtu wa kisasa. Ninatafuta kwanza uthibitisho wa kisayansi kabla sijaamini chochote. Thibitisha kisayansi kwamba Yesu alisulubiwa, alizikwa, na akafufuka kutoka kaburini ndipo ninaweza kuwa mwamini!"

Katika somo hili, tutajifunza kuhusu dhana nne potofu za kawaida kuhusiana na Ukristo zinazochangiwa na watu wengi. Watu wengi wasiokuwa Wakristo, na hata baadhi ya Wakristo, wanaamini katika mambo manne tunayokwenda kujadili hapa. Lakini dhana hizi ni za uongo zinazoweza kumzuia mtu asiye Mkristo anayejitahidi kuilewa Injili. Tunapaswa kujibu haya maswali yote kama yanamzuia mtu ye yeyote kuwa Mkristo.

Dhana potofu ya 1: Ukristo ni lazima uthibitishwe kwa njia ya Kisayansi

Baadhi ya watu wasioamini husema, "Siwezi ikaumini Ukristo ila tu kama unaweza kuthibitisha kwanjia ya kisayansi."

Kuelewa tatizo lililoko katika kauli hii, ni lazima uelewe kwanza maana ya "njia ya kisayansi." Njia ya kisayansi huthibitisha kitu *kwa kukifanyia majaribio ya kurudiarudia tena na tena katika mazingira yaliyodhibitiwa wakati huo huo matokeo yake yakiwekwa katika kumbukumbu.*" Njia ya kisayansi inahitaji majaribio ya kurudiwarudiwa.

Je, tunaweza kuthibitisha kwa njia ya kisayansi kwamba nguvu ya uvutano ipo? Ndio! Tunaweza kuangusha jiwe mara ishirini na kuweka kumbukumbu, "mara ishirini kwa jiwe kuanguka kwenye ardhi." Nguvu ya uvutano ipo.

¹⁵ 1 Petro 3:15

Je, tunaweza kuthibitisha kwa njia ya kisayansi kwamba Yesu alisulubiwa msalabani, akazikwa na akafufuka kutoka kaburini? Hapana! Hili ni tukio la kihistoria ambalo haliwezi kujirudia. Hatuwezi tukamwua tena Yesu mara ishirini, tukamzika, na tukangojea kufufuka tena!

Wale watu wanaosadiki kuwa hatuna habari za Mungu wala hatuwezi kuzijua wanaodai kwamba matukio ya kihistoria ni lazima yathibitishwe kwa njia za kisayansi wanajichanganya katika aina mbili za uthibitisho. Kuthibitisha matukio ya kihistoria, hatuwezi kutumia njia ya kisayansi, kwa sababu hutuwezi kuyarudia tena hayo matukio. Ili kuweza kuthibitisha matukio ya kihistoria, ni lazima tutumie njia ya uthibitisho ya *sheria-ya kihistoria*.

Njia ya sheria-historia hutafuta ushahidi kamili wa kuthibitisha tukio. Huangalia katika:

- Ushahidi ulioandikwa
- Ushahidi wa kusimuliwa kwa mdomo
- Ushahidi halisi wa kuona kwa macho

Jaribu kufikiria kwamba tunataka tutambue, "Je, Julius Nyerere wa Tanzania alikuwa hai mwaka 1972?" Hili siyo swalii la kisayansi; ni swalii la historia. Kutaka kuthibisha kuwepo kwa Nyerere, tutapaswa kutumia njia ya sheria-historia ya kuthibisha. Tutatafuta kuangalia:

Ushahidi ulioandikwa:

- Je, tunaweza kupata nyaraka zilizoandikwa kuanzia mwaka 1972 zinazomhusu Nyerere?
- Je, wasifu zilizoandikwa na watu mbalimbali kuhusiana na Nyerere zina maelezo yake kuanzia mwaka 1972?

Ushahidi wa kusimuliwa kwa mdomo:

- Je, tunaweza kumpata mtu yejote anayesema kwamba, "alikutana na Nyerere mwaka 1972"?
- Je, tunaweza kuzipata hotuba mbalimbali zilizotolewa na Nyerere mwaka wa 1972?

Ushahidi halisi wa kuona kwa macho:

- Je, zipo picha zozote za Nyerere za kuanzia mwaka 1972?

► Kabla ya kuendelea kusoma maandiko yanayofuata, jadili njia za sheria-ya kihistoria za kuthibisha unazoweza kuzipata kuhusiana na maisha ya Yesu wa Nazarethi.

Tumweke Yesu kwenye kipimo tulichokitumia kwa Nyerere.

Ushahidi ulioandikwa:

- Je, tunaweza kupata nyaraka zilizoandikwa zinazomhusu Yesu?

Josephus, mwana historia wa Kiyahudi, aliandika kuhusu Yesu katika hifadhi yake ya *mambo ya kale* (*Antiquities*), historia iliyoandikwa kwenye karne ya kwanza.

- Je, zipo wasifu zozote zilizoandikwa kutoka kwa watu mbalimbali waliomfahamu?

Kwenye vitabu vyote vya Injili, kila kimoja ni wasifu wa kihistoria. Injili ya Mathayo na Yohana ziliandikwa na wafuasi wake wa karibu sana. Marko alinukuu kumbukumbu za Simoni Petro. Luka alikuwa msomi makini sana, aliyechunguza kila historia katika Injili yake aliyoandika.¹⁶

Ushahidi wa kusimuliwa kwa mdomo:

Mlinzi wa dola ya Kirumi alishuhudia, "Hakika mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu!"¹⁷

Injili zimekusanya taarifa za kina za kumbukumbu za maneno ya Yesu mwenyewe. Baadhi ya hizi, kama ile ya Hotuba ya Mlimani, ni ndefu. Ushuhuda huu wa mdomo ulikuja kuchukuliwa pia kama ushuhuda ulioandikwa katika Injili zote.

Ushahidi halisi wa kuona kwa macho:

Tomaso, mtu ambaye hakuweza kukubaliana na ushuhuda wa wanafunzi wenzake, aligusa mikono ya Yesu na akasema, "Bwana wangu na Mungu wangu!"¹⁸

Yakobo, ndugu yake Yesu, ambaye hakuyaamini maneno ya Yesu kwenye siku za awali za utumishi wake hapa duniani, alikuja kuwa mwamini alipomwona Bwana amefufuka.¹⁹

Ukristo ni dini ya pekee sana mionganini mwa dini zote za dunia. Kuna ushahidi mdogo sana kuhusu maisha ya Muhammadi au Buddha. Dini hizi haziwezi kuthibishwa kama ni za kweli au uongo kwa kutumia njia hii ya sheria-ya historia. Ukristo unaweza kuthibitishwa kuwa ni wa kweli kwa kutumia ushahidi huu huu ambao tunautumia kuthibitisha maisha ya mtu ye yeyote maarufu katika historia.

Je, sayansi ni muhimu katika elimu ya Kikristo ya kuitetea imani? Ndiyo! Kweli za kisayansi zinathibitisha ukweli wa Biblia. Baadhi ya kweli za kisayansi zinasaidia sana kuunga mkono ukweli wa Biblia.; lakini maisha, kifo na kufufuka kwa Yesu ni lazima kupimwe kwa kutumia njia hii ya sheria na historia.

Kama mtu asiye Mkristo akisema, "Ni lazima uuthibitishe Ukristo kwa njia ya kisayansi," mwonyeshe kwamba matukio yasiyoweza kujirudia kama kuzaliwa na kufa kwa mtu, hakuthibitishwi kwa njia za kisayansi bali kwa njia ya sheria-ya kihistoria. Onyesha ushahidi

¹⁶ Luka 1:1-4

¹⁷ Marko 15:39

¹⁸ Yohana 20:28

¹⁹ 1 Wakorintho 15:7

wa sheria-ya kihistoria katika kutoa ushahidi wa maisha ya Yesu Kristo. Hali hii inaweza kuondoa kizuizi kimojawapo katika vizuizi vinavyozuia njia ya kuuenda msalaba.

Dhana Potofu ya 2: Ukristo ni lazima Uthibitishwe kwa asilimia 100% ya Uhakika

Dhana potofu ya pili kuhusiana na elimu ya kuitetea imani inasema. "Siwezi nikauamini Ukristo kama hakuna ushahidi thabiti kwamba Ukristo ni wa kweli."

► Kabla kusoma andiko linalofuata, ni kwa jinsi gani utajibu kuhusiana na dhana hii potofu? Je, kauli hii ina mantiki yeyote?

Kwenye majadiliano yenu kuhusiana na swali hili, je, yuko yeyote aliyesema, "Huwezi ukathibitisha tukio lolote la kihistoria kwa uhakika wa asilimia 100%"? Haya ni majibu mazuri. Kwa sababu tukio lililotokea zamani sisi hatukuwepo, kwa hiyo, hatuwezi kuthibitisha kwa ushahidi thabiti wa asilimia 100%.

Tuangalie mifano hii inayotokana na historia:

- Katika mwaka 49 K.K. Julius Kaisari alivuka kijito cha Rubicon akiwa njiani kwenda Roma. Je, yuko mtu yeyote anayeweza kuthibitisha jambo hilo kwa uhakikia wa asilimia 100%? Hapana; hatuwezi kutembelea siku hiyo ya historia ili kutoa ushahidi wa kumchunguza Kaisari. Lakini hakuna mwana-historia yeyote anayeweza kupinga jambo hili. Wana historia wanaamini kwamba Julius Kaisari alivuka kijito cha Rubicon kwa sababu kuna ushahidi wa sheria-historia wa kuunga mkono tukio hilo.
- Mwaka 1789, George Washington alikuwa raisi wa Amerika. Je, kuna njia yeyote ya kuthibitisha hili kwa uhakika kwa asilimia 100%? Hakuna; hatuwezi kuwepo siku hiyo ya historia ili kutoa ushahidi kushuhudia George Washington akiapishwa. Lakini hakuna mwana-historia anayelikataa tukio hili.
- Mwaka 1917, Nicholao wa II aliachia kitie cha kifalme cha ufalme wa Urusi. Je, Kuna njia yeyote ya kuthibitisha hili kwa asilimia 100% ya uhakika? Hakuna; hatuwezi kuwepo siku hiyo ya historia ili kutoa ushahidi wa mfalme Nicholao wa II kukataa kuendelea kuwa mtawala. Lakini hakuna mwana-historia anayekataa kuwepo kwa tukio hilo.

Hatuwezi kuthibitisha matukio ya historia kwa asilimia 100% ya uhakika. Badala yake, tunakusanya vielelezo hadi tutakopojiridhisha kwamba tuna ushahidi wa kutosha kufanya uamuzi kuhusiana na kilichotokea. Hata mahakamani, mwendesha mashitaka hahitajiki kutoa ushahidi thabiti. Kinachotakiwa ni Baraza linalosikiliza shauri kuthibitishiwa bila ya kuwepo na shaka yeyote kwamba uhalifu ulifanyika.

Ni kwa jinsi hii tunavyoishi kila siku. Tunafanya maamuzi yanayotokana na ushahidi wenyе vielelezo vilivyojitosheleza, na siyo ushahidi thabiti.

Kama Wakristo wenyе eimu ya kuitetea imani, hatuhitajiki "kuuthibitisha Ukristo kwa asilimia 100% ya ushahidi thabiti." Badala yake, tunawajibika kuonyesha kwamba kuna ushahidi wa kutosha katika kuamini ukweli wa imani ya Kikristo. Ushahidi wa kihistoria kwa ajili ya Ukristo sio ule thabiti, bali unajitosheleza

► Kama hatuwezi kuthibitisha kwa uhakika wa asilimia 100% kwamba Ukristo ni wa kweli, je, inamaanisha kwamba kamwe hatuwezi kujua kwa uhakika kuwa Ukristo ni wa kweli?

Usifikirie kuwa hili linamaanisha kwamba hatuwezi kujua kama Ukristo ni wa kweli! Kuna tofauti kati ya *kujua* kitu kwa uhakika na *kuthibitisha* kitu kwa uhakika.

Nataka niwape kielelezo rahisi kuhusiana na hili. Leo ni tarehe 15 Septemba, 2016. Ninajua kwa uhakika nilichokula leo kwa ajili ya kifungua kinywa. Nilikula stroberi na bakuli la uji, nikanywa na kikombe cha kahawa. Ninajua hili, lakini siwezi nikakuthibitishia wewe. Ulikuwa hauko pale; sikuchukua picha kwa ajili ya ushahidi. Ninajua hilo; lakini siwezi kulithibitisha.

Unawewza ukajua kwa uhakika kwamba Ukristo ni wa kweli. Ukiifunza ushahidi wa ukweli wa Ukristo na ukachukua hatua ya imani ambayo ni muhimu katika kumwamini Kristo, Roho Mtakatifu atakuthibitishia ndani ya moyo wako kwamba kile unachokiamini kwa uhakika ni cha kweli. Utaishi na kutenda kana kwamba una uthibitisho wa uhakika kwa sababu unazo sababu za kutosheleza kuweza kuzifanya ziwe asilimia 100%. Hii inaitwa *uhakika wa maadili*. Unaweza ukajua kwa uhakika kwamba imani ya Kikristo ni ya kweli ingawaje huwezi kuthibitisha kwa asilimia 100%.

Dhana potofu ya 3: kila mtu ana ukweli wake binafsi

Wakati wa leo, ni jambo la kawaida kusema, "Ukweli siyo lazima uwe kweli." Kwa maneno mengine, kama unaamini kitu, kwako wewe ni cha ukweli – na kwa mtu mwingine kinaweza kisiwe cha ukweli.

Jaribu kufikiria kwamba bilauri iliyojaa sumu ilikuwa kwenye dawati katika chumba hiki. Fikiria kwamba uliingia chumbani ukiwa na kiu na ukaichukua ile bilauri ukayanywa kile unachodhani ni maji, ukiamini kwamba kilichokuwemo ndani ya ile bilauri ni maji. Utakuwa mgonjwa, hata kama ulijiaminsha kabisa kwamba bilauri ilikuwa imejaa maji.

Kuamini kitu hakifanyi kiwe ni cha ukweli. Ukweli ni ukweli bila kujali imani yetu. Kuamini kwamba sumu ni maji haiwezi kuubadili ukweli. Kila mtu hana ukweli wake.

"Kuna ushahidi wa kutosha kwa imani ya Kikristo kumshawishi mtu ye yote ambaye bado hajajipanga kuwa kinyume chake.
Lakini hakuna ushahidi unaotosheleza wa kumleta mtu kwenye ufalme wa Mungu kwa mtu anayekataa kuingia."
- Blaise Paschali,
Mwanafalsafa na mwanasayansi
wa kifaransa

Kauli ya "kila ukweli siyo lazima uwe kweli" *inajichanganya yenyewe*. Kauli hii ni kamilifu, lakini inadai kwamba hakuna kauli zilizo kamilifu. Kama kila ukweli siyo lazima uwe kweli, kauli ya "kila ukweli siyo lazima uwe kweli" siyo ya ukweli!

Tafakari mzungumzo haya kati ya Mkristo (Thomasi) na mtu mwingine agnostiki (Aldous)- (*asadikiye kuwa hatuna habari za Mungu wala hatuwezi kuzijua.*)

Aldous: "Injili inaweza kuwa kweli kwako; siyo kweli kwangu."

Thomasi: "Kwa hiyo kila mtu ana ukweli wake?"

Aldous: "Ndiyo! Hivyo ni sahihi."

Thomasi: "Unasema kwamba hakuna kilicho kamilifu? Hakuna kilicho kweli katika hali zote?"

Aldous: "Hivyo ni sahihi! Ukristo unaweza kuwa kweli kwako, lakini siyo kweli kwangu."

Thomasi: "Hilo linavutia sana! Unaniambia kwa uhakika kabisa kwamba hakuna chochote kiicho cha uhakika? Kama kwako ni sahihi, umekosea!"

Je, unaelewa? Namna hii ni kujichanganya binafsi. Haiwezekani iwe kweli katika mambo yote na kwamba hakuna kweli katika mambo yote. "Kauli kwamba, "Hakuna mambo makamilifu kabisa" inawakilishwa kama kauli iliyokamilika. Hii haiwezekani ikawa kweli.

Tumwone tena Aldous na Thomasi wakiendelea na mazungumzo yao. Thomasi atamwongoza Aldous kwenye maamuzi mazuri kuhusiana na asili ya ukweli. Unaweza ukahifadhi mazungumzo yanayofanana na haya kama anavyofanya Thomasi. Fanya kuigiza mazungumzo haya na mwanafunzi mwenzako kabla ya kukutana na mtu wako:

Thomasi: "Kwa hiyo, Aldous, unaufafanuaje ukweli?"

Aldous: "Ukweli ni kile unachokiamini."

Thomasi: "Sawa. Vyema. Je, unaweza kuamini kitu ambacho ni cha uongo?"

Aldous: "Ndio."

Thomasi: "Kwa hiyo basi ukweli sio kile unachoamini, au siyo?"

Aldous: "Nafikiri hapana."

Thomasi: "Kama ningekuambia kwamba huko nje ya darasa kwa sasa hivi mvua inanyesha, hayo yatakuwa ni madai ya ukweli au madai ya uongo?" [Siyo kwamba kuna mvua ya ukweli inanyesha nje wakati wa mazungumzo haya ya Thomasi na Aldous.]

Aldous: "Hayo yatakuwa madai ya uongo."

Thomasi: "Kwa nini yawe madai ya uongo?"

Aldous: "Kwa sababu hakuna mvua ya ukweli inayonyesha."

Thomasi: "Hivyo ni sawa. Madai yangu hayafanani na ukweli. Ili madai au kauli viwe kweli, ni lazima viambatane na uhakika. Madai huwa ya uongo kama hayaendani na ukweli. Tafsiri nzuri ya ukweli ni hii: Ukweli ni wazo au maelezo yanayoendana na uhalisia. Kama ndivyo ilivyo, je, ukweli ni kitu tunachokigundua au ukweli ni kitu tunachounda?"

Aldous: "Kitu tunachogundua."

Thomasi: "Hivyo ni sawa. Ni kitu tunachogundua, au kinachofunuliwa kwetu. Hii inamaanisha kwamba ukweli upo nje yetu wenyewe; sio sula la kibnafsi. Siyo kitu tunachokitengeneza, lakini ni kitu tunachokikuta. Kwa hali hiyo, tunapaswa kuwa watafutaji wa ukweli. Kuna majibu halisi yasiyo ya kibnafsi katika maswali makubwa ya kifalsafa (mf sisi tumetoka wapi, kwanini tupo hapa, na tunakwenda wapi), na ni nia yetu kubwa ya kutaka kugundua majibu ya maswali hayo."

Dhana potofu ya 4: Uaminifu ni Muhimu kuliko Ukweli

Dhana hii inahusiana na Dhana potofu ya 3. Inasema, "Haijalishi unaamini nini ili mradi unakuwa mwaminifu katika imani yako. Haijalishi unaiweka kwa nani au unaiweka imani yako katika nini. Jambo muhimu ni kwamba unaamini kitu fulani."

► Unawezaje kujibu dhana hii potofu?

Watu wanaoamini katika Dhana potofu ya 3 ("kila mtu ana ukweli wake binafsi") mara nyingi huiamini dhana potofu ya 4. Hata hivyo, tumeshaona kwamba kuamini sumu ni maji haileti kuwa kweli. Kuamini kitu hakukifanyi kuwa cha ukweli. Hii ni muhimu sana hasa katika suala la wokovu. Kuamini tu kwamba nimekombolewa hakutoshi. Haijalishi mimi ni mwaminifu kiasi gani. Ni muhimu kwamba tunaamini katika kitu gani. Kitu kinachotufanya tuwe katika kuamini, ndicho kinachoitwa *kitu cha kuamini*.

Kitu cha kuamini ni muhimu. Kwa mara nyingine tena, tuelezee jambo hii kwa mfano halisi wa maisha. Fikiria watu wawili wamesimama ukingoni mwa mteremko mkali wa ghafla. Thomasi anasema, "Nitatafuta daraja lenye nguvu ninaloliamini kwamba linaweza kunivusha kwenye korongo." Aldous anasema, "Haijalishi kama daraja lina nguvu, ili mradi ninaamini kwa dhati." Ni yupi atakayeweza kuvuka hilo korongo kwa usalama?

Kuna mtu mmoja tu anayeweza kutuokoa – Yesu Kristo. Ni lazima tuiweke imani yetu kwake. Haitatusaidia kwa namna yejote ile kuiweka imani yetu kwa mtu au kitu ambacho hakiwezi kutuokoa, haijalishi tutakuwa waaminifu kwa kiasi gani.

Hatuokolewi kwa imani yetu; tunaokolewa na Kristo wakati tunapoiweka imani yetu kwake. Tunaokolewa kwa neema ya Kristo, *kwa njia ya imani*.²⁰ Ni Kristo peke yake anayeweza kuleta ukombozi.

Wala siyo kwa *nguvu* ya imani yetu inayoweza kutuokoa; ni shabaha ya imani yetu. Fikiria juu ya watu wawili. Abdala ambaye ni Muislamu mwenye imani ya nguvu katika mafundisho ya Muhammadi; Nabeli ambaye ni Mkristo mwenye imani dhaifu. Imani ya Nabeli ni ya uhakika, lakini ni dhaifu.

► Nani mwenye ukombozi? Abdala na imani yake ya nguvu katika Muhammadi au Nabli na imani yake dhaifu (lakini ya uhakika) katika Kristo?

Mkristo ndiye peke yake aliyekombolewa ingawaje ana imani iliyo dhaifu. Kwa nini? Kwa sababu ana imani katika mtu aliye sahihi.

Watu wengi husema kwamba mtu aliye katika dini yeote ataokolewa ili mradi awe waaminifu. Ili mradi wanaamini wako kwenye barabara sahihi, watakuwa sawa. Tuone jinsi hiyo inavyofanya kazi.

► Angalia ramani hii ya jimbo la Iowa.²¹ Ni barabara ipi inaenda kutokea Des Moines (1) hadi Davenport (2)?



²⁰ Soma Waefeso 2:8-9

²¹ "Iowa" was created by SGC with open data from NED and Wiki Commons, available from <https://www.flickr.com/photos/sgc-library/52344115203>, public domain (CC0).

Jibu ni Interstate 80. Nikiendesha gari katika barabara ya Interstate 35 kutokea Des Moines na nikaamini kwa uaminifu kabisa kwamba inakwenda Davenport, je, itanifikisha Davenport? Hapana!

Kuamini kwamba barabara fulani itanifikisha mahali fulani haimaniishi kwamba itanifikisha mahali pale. Ni lazima niwe kwenye barabara iliyo sahihi. Vivyo hivyo, kuamini kwamba niko njiani kuelekeea Mbinguni haimaanishi kwamba njia hiyo itanifikisha pale. Inanibidi kwa vyovyote niwe katika njia sahihi. Mwandishi wa kitabu cha Mithali alisema, "Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, Lakini mwisho wake ni njia za mauti."²² Yesu alisema, "Mimi ndimi njia ... mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi." (Yohana 14:6). Njia nyingine yejete kama siyo kupitia kwa Yesu haitaweza kutufikisha Mbinguni.

Elimu ya Kuitetea Imani katika Vitendo – Kuokoka kwa Josh McDowell

Kama kijana aliyejekulia Michigan, Josh McDowell (mzaliwa wa 1939)²³ alitafuta majibu katika maswali makubwa matatu: *Mimi ni nani? Kwaninii mimi niko hapa? Mimi ninakwenda wapi?*

Josh alitafuta majibu ya maswali haya kanisani, lakini hakupata majibu ya maswali haya katika kanisa alilohudhuria. Josh alitafuta majibu katika elimu, lakini aligundua kwamba aidha waalimu wake au wanafunzi wenzake hawakuwa na majibu ya maswali haya makubwa. Josh akafikiria kwamba majibu ya maswali haya yanaweza kupatikana kwenye vyama, lakini akagundua kwamba msisimuko wa vyama umeshaisha – akabakia amechanganyikiwa kuhusu kusudi lake la maisha na hatima yake.

Watu waliokuwa wanamzunguka McDowell walidhania kwamba alikuwa na furaha, lakini ndani alikuwa mtupu. Wakati huo, aliona kundi la wanafunzi na walimu waliokuwa na furaha na walioonekana kuwa na amani ya ndani.

Siku moja, Josh alikaa chini na kuzungungumza na wanafunzi hawa. Walipoitaja imani yao iliyo katika Mungu, McDowell aliwafanya mzaha, "Ukristo ni kwa ajili ya watu wadhaifu, siyo kwa wasomi." Hata hivyo, alivutiwa sana na watu hawa hivyo akamwuliza mwanafunzi mmojapo, "Kwa nini mko tofauti sana na wanafunzi wengine wote katika kitivo na chuo hiki? Ni nini kilibadilisha maisha yenu?" Jibu la yule dada lilimshangaza McDowell; alisema, "Yesu Kristo."

Wakati McDowell aliposema kwamba hawezi kumwamini Yesu, rafiki yake alimpa changamoto ya kufanya kazi itakayomfanya achunguze kwa umakini kabisa madai kuhusiana na Yesu Kristo; kwamba ni Mwana wa Mungu; kwamba aliishi kama mwanadamu kamili katika ulimwengu huu; kwamba alikufa kifo cha msalaba kwa ajili ya dhambi za

²² Mithali 14:12

²³ Nyenzo hii ilinukuliwa kutoka katika ushuhuda wa Josh McDowell, imepatikana kutoka <https://www.cru.org/us/en/how-to-know-god/my-story-a-life-changed/my-story-josh-mcdowell.html> April 18, 2020.

wanadamu; kwamba alizikwa na akafufuka siku tatu baadaye; na kwamba yu hai bado na anaweza kubadilisha maisha ya mtu hata leo.

McDowell alikubaliana na changamoto hiyo ili kusudi aweze kuthibitisha kwamba habari zinazohusu Ukristo ni za uongo. Kama mwanafunzi wa elimu ya awali ya sheria, Josh alijua namna ya kuuchunguza ushahidi. Alianza kwa kujifunza Biblia. Alitaka kutafuta ushahidi kwamba Biblia haiaminiki.

Kwa miezi kadhaa, Josh alijifunza ushahidi wa Biblia. Alichokigundua kilibadilisha maisha yake. Aligundua kwamba vitabu vya Agano la Kale na Agano Jipya ni mojawapo ya nyaraka zilizokuwa zinaaminika zaidi katika ulimwengu wa kale. Hali hii ilimlazimisha kuwa na swalil gumi, "Je, Yesu alikuwa zaidi ya seremala? Je, alikuwa kweli ni Mwana wa Mungu?" McDowell alifikia uamuzi wa mwisho kwamba Yesu kwa uhakika alikuwa ni Mwana wa Mungu.

Mara tu akili zetu zinapogundua ukweli wa Injili, tunakuwa tuko tayari kukabiliana na swalil la moyo wetu. Baada ya kutambua ukweli wa Biblia, McDowell alikuwa bado hayuko tayari kukubali Kristo awe Bwana wake. Kulikuwa na sababu mbili za kutokuwa tayari kwake: starehe na kiburi.

McDowell alijua kwamba kuwa Mkristo kutamzuia kuendelea na maisha yake ya dhambi ya starehe na atatakiwa kuacha kujiongoza katika maisha yake. McDowell anasema, "Nilikuwa natembea katika uwanja wa mapambano. Akili yangu ilikuwa inaniambia kwamba Ukristo ulikuwa wa kweli, lakini mapenzi yangu yaliizuia kwa nguvu kwa kadri ilivyowezekana."

Pia alipambana na hali yake ya kiburi. Kama Injili ni ya kweli, basi yote aliyoyaamini siku za nyuma ni makosa. McDowell alikabiliana na mapambano yaliyoyofanana na yale C.S. Lewis aliyokutana nayo. Hata hivyo, baada ya miezi kadhaa ya mapambano, McDowell aligeuka na kuwa Mkristo.

Kuanzia wakati huo, maisha ya McDowell yalibadilika. Elimu ya kuitetea imani ilivunja viambaza vya akili vilivyomzuia kuamini. Kisha, roho Mtakatifu akamleta kwenye nafasi ya kuamini. Kama Wakristo tunaweza kuitumia elimu ya kuitetea imani kuwaleta wasioamini kwenye eneo ambalo litawaweka wazi katika kuisikia sauti ya Mungu.

Hitimisho

Jia alisikiliza kwa umakini swalil la Lee, "Je unaweza kuthibitisha kifo cha Yesu na kufufuka kwake kwa kutumia njia ya kisayansi?" Msichana alikumbuka kwamba, "silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome."²⁴ Kwa haraka aliomba kwamba Mungu ampe uwezo wa kuwasiliana kwa kutumia nguvu za kiungu.

Jia alijibu, "Lee, napenda nikuulize swalil. Wewe unaijua historia ya China sana. Kama unaweza kujibu swalil langu, nami nitakuwa tayari kujibu swalil lako. Hapo ni sawa?" Lee

²⁴ 2 Wakorintho 10:4

alikuwa na uhakika kwamba alikuwa anaweza kujibu swal i Jia; kwahiy o akajibu kwa ujasiri, "Hakika."

Jia akasema, "Nimekuwa nikiwa na mashaka sana kuhusiana na Sun Yat-sen. Vitabu vyetu vya historia vinatueleza kwamba alianzisha Jamhuri ya China. Hata anaitwa 'Baba wa Taifa.' Je, unaweza kuthibitisha kwa njia ya kisayansi na kwa uhakika wa asilimia 100% kwamba Sun Yat-sen aliishi?"

Lee alicheka. "Swali gani hilo la kijinga! Hakika, Sun Yat-sen aliishi. Hilo ni rahisi kuthibitisha. Acha nitafute gazeti la mwaka 1925. Litaonyesha ni lini Raisi Sun alifariki."

Jia aliingilia kwa kicheko, "Hapana, hapana, hapana! Kumbuka uliniuliza kuhusu kuthibitisha kwa njia ya kisayansi. Ina maana kwamba unapaswa urudie tukio hilo mara nyingi na ukiwa unaandika matokeo yake. Nitasubiri hapa wakati unasi mamia Sun Yat-sen azaliwe tena!"

"Hivyo siyo sawa," Lee alibwabwajika. "Haiwezekani kuyazaa kwa mara nyingine maisha ya Sun Yat-sen, lakini tunajua kwamba aliwahi kuishi! Tunazo shuhuda nyingi kutoka kwa waandishi wa wakati wa maisha yake; tunazo hotuba zilizoandikwa na watu waliokuwa wakimsikia akisema; tunazo hata picha za Raisi Sun. Je, unaweza kupuuzia uthibitisho huu wa kisheria-kihistoria?"

"Uko sahihi," Jia akasema, "Ninaamini Sun Yat-sen aliishi. Siwezi nikajithibitishia kwa uhakikia wa asilimia 100%, lakini kuna ushahidi mzuri wa maisha. Hiyo ni sababu sawa na ile iliyonifanya niamini kwamba Yesu aliishi, alikufa, na alifufuka kutoka kwa wafu. Vitabu vya Injili viliandikwa na watu waliokuwa wanamjua sana Yesu; Mathayo aliandika kuhusu mafundisho ya Yesu; watu wengi maarufu wenye kutia shaka walikuja kuwa waamini waliposhuhudia ufufuo wake kwa macho yao wenyewe.

"Injili ilifika China kutokea India. Ililetwa India na mtume aitwaye Thomasi. Lee, unanikumbusha kuhusu Tomaso. Walimwita jina la 'Tomaso mwenye Mashaka' kwa sababu alisema, 'Mimi nisipoziona mikononi mwake kovu za misumari... mimi sisadiki hata kidogo.'²⁵ Lee, miaka 2,000 iliyopita, Tomaso alikuwa na mashaka yanayofanana na uliyo nayo. Lakini alifunguka akili yake kwa ushahidi uliokuwepo – na maisha yake yakabadilika kabisa. Zisome, ruhusu Mungu aseme, na utaona sababu za kuamini."

²⁵ Yohana 20:25

Kazi za kufanya Somo la 2

(1) Elimu ya kuitetea imani na Kichwa: Utaanza kipindi kijacho cha darasa kwa kufanya mtihani unaorejea tafakuri ya maswali yaliyomo katika somo la 2. Yatafakari haya maswali kwa umakini kwa ajili ya maandalizi ya mtihani wa mwisho ujao.

(2) Elimu ya kuitetea imani na Moyo: Omba kwa ajili ya mwamini ambaye hajaamini uliyezungumza naye wiki lililopita. Omba kwamba Mungu amfungue macho yake ili auone ukweli. Omba kwamba Mungu akupe majibu utakapokuwa unazungumza nao wakati ujao. Mshukuru Mungu kwa nafasi ya kuwa mshuhudiaji kwa huyu mtu.

(3) Elimu ya kuitetea imani na Mikono: Zungumza na mtu mmoja ambaye anaamini angalao katika mojawapo ya dhana nne potofu katika somo hili. Ili kupima kama mtu ameshikiliwa katika dhana hizi potofu, unaweza kuuliza maswali kama:

- “Je, Ukristo unawezaje kuthibitishwa kama inawezekana kuthibitishwa?”
- “Je, utahitaji uthibitisho wa kiasi gani ili kuamini katika Ukristo?”
- “Ukweli ni nii?”
- “Je, kila mtu ana ukweli wake binafsi?”
- “Kuna umuhimu wa kiasi gani kwamba unaamini kitu au mtu sahihi?”

Mwulize mtu asiyeamini sababu za yeye kuamini kama anavyofanya. Mwulize kama atakuruhusu kumshirikisha maandiko ya kumbukumbu kutoka katika somo hili. Kama akikuruhusu, mshirikishe maelezo na mifano kutoka katika somo hili. Usiwe mpinzani sana lakini toa majibu rahisi na yaliyo wazi kuhusiana na dhana potofu anazoweza kuwa nazo mtu asiyeamini. Chukua maelezo ya kumbukumbu kuhusu mazungumzo yako kwa ajili ya kuyashirikisha kwenye kipindi chako cha darasa kijacho.

Mtihani wa somo la 2

- (1) Ni mambo gani muhimu yanayohusika na njia ya kisayansi?
- (2) Badala ya njia ya kisayansi, matukio ya kihistoria yathibitishwe kwa njia gani?
- (3) Kuna aina ngapi tatu za ushahidi katika ushahidi unaoutumika kuthibitisha njia ya sheria-historia?
- (4) Kwa nini tunasema, "Hatuwezi kuthibitisha tukio lolote la kihistoria kwa uhakika wa asilimia 100%"?
- (5) Kama huwezi kuthibitisha kitu kwa uhakika kabisa, lakini unao uthibitisho wa kutosha wa kuweza kuleta imani ya ndani kabisa kwamba ni kweli (na uko tayari kuishi sawa na imani hiyo ya ndani), wewe una _____.
- (6) Kauli ya kila ukweli siyo lazima uwe kweli _____, hivyo haiwezekani kuwa kweli.
- (7) Ukweli ni nini?
- (8) Haitoshi tu kuamini. Ni lazima tuiweke imani yetu kwa usahihi katika _____.
- (9) Orodhesha dhana nne potofu dhidi ya elimu ya kuitetea imani zilizofundishwa katika somo hili. Toa majibu mafupi kuhusiana na kila dhana.
- (10) Nukuu kutoka kichwani 2 Wakorintho 10:4-5.

Somo la 3

Je, Mungu Yupo?

Utangulizi

Jia hakuweza kumwona rafiki yake kijana Lee kwa wiki mbili. Alipoulizia kwa jirani yake, alipewa taarifa za kusikitisha kwamba mama yake na kijana Lee alifariki kutokana na ugonjwa wa muda mrefu. Lee alikuwa ameenda Taoyuan kuungana na familia yake.

Wakati Jia alipokutana na Lee wiki mbili baadaye, alielezea masikitiko yake kutokana na kifo cha mama yake. Lee alimshukuru sana yule dada kwa wema wake, lakini baadaye akaongea kwa uchungu, "Hii ndiyo maana mimi siwezi kumwamini Mungu wa Wakristo. Kama kuna Mungu, kwa nini aliruhusu mama yangu ateseke kiasi hicho? Mnasema Mungu wenu ni mwenye nguvu sana na mwenye upendo sana. Kama kweli alikuwa anampenda mama yangu, na kama kweli alikuwa na nguvu za kuweza kuzuia mama yangu asiteseke, kwa nini alimwacha ateseke kiasi hicho? Inawezekana kuna Mungu, lakini hana uwezo wa kutusaidia. Au inawezekana kuna Mungu, lakini hajali kuhusu mateso yetu. Au labda hakuna Mungu. Naamini tuko peke yetu katika ulimwengu huu."

► Utamjibuje Lee?

Je, Mtu yeyote aweza kujua kwamba Hakuna Mungu?

Je, mtu yeyote aweza kujua kwa uhakika kabisa kwamba hakuna Mungu? Jaribu kufikiria maarifa yote katika ulimwengu kama duara kubwa. Sasa jaribu kufikiria maarifa yako kama duara ndani ya maarifa yote ya dunia.

Isipokuwa duara la maarifa yako linalandana na duara la maarifa yote katika ulimwengu, hujui kila kitu. Kama maarifa yako ya sasa hayajumuishi maarifa kuwa Mungu yupo, anaweza kuwa yupo kwenye duara kubwa la maarifa na siyo katika duara lako mwenyewe. Itakubidi uwe na maarifa yote katika ulimwengu kuthibitisha kwamba Mungu hayupo. Watu wengi wasioamini wanakiri hili, ya kwamba inawezekana Mungu yupo, lakini bado hawajamgundua.

Kama inawezekana kwamba Mungu yupo, mtu mwaminifu atapaswa kuwa tayari kuupima ushahidi wa uwepo wa Mingu. Watu kama C.S. Lewis na Josh McDowell waliupima ushahidi huu na ikajatokea kuamini kwamba Mungu yupo na amejidhihirisha mwenyewe kupitia kitabu cha Biblia.

Somo hili litatusika na ushahidi wa kuwepo kwa Mungu. Tutaona kwamba kuna sababu nydingi za kuamini kwamba Mungu yupo.



Ushahidi wa Uwepo wa Mungu: Hoja kuhusu Sayansi ya Dunia

Hoja ya kosmolojia inadai maelezo toshelevu kuhusiana na kuwepo kwa dunia. Hoja hii inauliza, "Kwanini dunia ipo?" Inahitimisha, "Dunia ipo kwa sababu iliumbwa na Mungu – aliye nafsi binafsi, wa milele, na aliyepo binafsi bila kuumbwa."

Hoja ya kosmolojia inaanza na wazo kwamba kila kitu ni lazima kiwe na maelezo. Kwa mfano, fikiri kwamba uliniuliza mimi, "Kiti ulichokalia kinatoka wapi?" Fikiria kwamba nitajibu, "Kiti kimetokea tu kuwepo; hakuna aliyetengeneza kiti; hakuna aliyenunua hicho kiti kukileta chumbani; kiti kilitokea tu kuwepo." Utajua tu kwamba hii ni makosa. Kila kitu kinapaswa kiwe na maelezo yanayojitosheleza, ikiwemo dunia kwa ujumla.

Hoja ya kosmolojia ina vigezo vitatu na hitimisho:²⁶

Kigezo mantiki A: Haiwezekani kuwa dunia haijatokana na kitu chochote.

Kigezo mantiki B: haiwezekani Dunia kuendelea kuwepo nyakati zote kama ilivyo sasa.

Kigezo mantiki C: Haiwezekani kuwa Dunia iliumbwa na kitu kisicho na uhai au nguvu fulani.

Hitimisho: Kwahiyio, dunia iliumbwa na kiumbe chenye nafsi, cha milele, kilichopo chenyewe bila kutegemea chochote.

Hapa tujadili maelezo yanayowezekana kuhusu ulimwengu

Watu Wengine Husema Dunia Haijatokana na kitu Chochote

Inawezekanaje bila kuwa na kitu kikatengenezaka kitu? Kutokuwepo kitu kinapaswa kiwe kitu ili kiweze kutengeneza kitu kingine. Kama tutasema kwamba dunia ilijitengeneza yenewewe, tutapaswa tuseme kwamba dunia iliwhi kuwepo hapo mwanzo kabla haijawepo wakati huu. Dunia ilibidi *iwepo* na *isiwepo* kwa wakati mmoja. Hili linajichanganya lenyewe. Kitu hakiwezi kuwa *kipo* na *hakipo* kwa wakati mmoja.

Watu Wengine Husema Dunia Siku Zote Imekuwepo Kama Ilivyo

Sheria mbili za mwendojoto, (*yaani sayansi ya uhusiano wa joto na kazi za mitambo*) inaonyesha ni jambo lisilowezekana kwamba dunia imekuwepo siku zote kama ilivyo.

Sheria ya kwanza ya mwendojoto inaelezea kwamba mata/nguvu haviwezi aidha kuumbwa au kuharibika. Sheria ya pili ya mwendojoto inalezea kwamba nguvu iliyokwishatumika katika dunia inageuzwa tena polepole kuwa nguvu isiyoweza kutumika tena. Unapoweka sheria zote mbili mahali pamoja, zinaonyesha kwamba dunia hapo mwanzo ilianza na kiwango cha kudumu cha nguvu ya kutumika ambayo kwa polepole inapungua.

²⁶ Hoja kutoka Kigezo mantiki hadi hitimisho imeandaliwa muda mrefu kuleta mantiki. Kigezo mantiki ni kauli nyepesi. Katika hoja halali yenye mantiki, kama kauli mantiki zinakubaliana zote, hitimisho ni lazima liwe kweli.

Jambo hili lina umuhimu gani? Dunia kwa polepole inatoweka. Kama wakati wote imekuwa ipo kama ilivyo sasa, (ikiwa ni pamoja na sheria za mambo ya asili za dunia), nguvu iliyopo duniani itakuwa tayari imeshatumika, kila kitu kitakuwa katika joto la aina moja, na wote tutakuwa tumekufa.

Watu Wengine Husema Dunia Imetokana na mata au Nguvu

Kama dunia itakuwa imetokana na nguvu ambayo haina nafsi, maana yake ni kuwa kisababishi kilichotengeneza dunia kitakuwa hakina nafsi. Ni jambo lisilowezekana kwa kitu kisichokuwa na nafsi kuumba tabia. Lakini wanadamu tunazo tabia. Kama kisichokuwa na nafsi hakiwezi kutengeneza tabia, basi wanadamu watakuwa wameumbwa na kiumbe chenye nafsi, cha milele, kiishicho chenyewe bila kutegemea chochote.

Kama Hakuna Maelezo Mengine Yanayo jitoshaleza, Dunia Itakuwa Imeumbwa na Kiumbe mwenye nafsi, wa Milele, anayeishi mwenyewe bila Kutegemea Chochote

Kwa kuwa maelezo mengine mbadala siyo sahihi, maelezo mengine yenye mantiki kwa uwepo wa dunia ni Muumbaji anayeishi kwa kujitosheleza.

Aina nyingine ya hoja ya kosmolojia ina kauli mbili zilizo msingi wa maelezo na hitimisho:

Kigezo mantiki A: Kila kinachoanza kina chanzo.

Kigezo mantiki B: Dunia ilianza.

Hitimisho: Dunia ina chanzo chake.

"Hakuna mtu ye yote aliye weza kuonesha ni kwa jinsi gani muda pamoja na bahati vinaweza kutengeneza machangamano tata katika dunia, achilia mbali haiba ya mtu."
- Nukuu kutoka kwa Francis Schaeffer,
He Is There and He Is Not Silent

Kigezo mantiki A kinaungwa mkono na ukweli kwamba kitu hakiwezi kutokea pasipo kitu chochote. Kisayansi, hili limekuwa likithibitishwa mara kwa mara. Uzoefu wetu wa kawaida unathibitisha jambo hili.

Kigezo mantiki B kinaungwa mkono na kupanuka kwa dunia na sheria ya pili ya mwendojoto. Wanasyansi wengi wanaamini kwamba dunia ina mwanzo wake.

Kama Kigezo mantiki A na Kigezo mantiki B ni vya kweli, basi hitimisho ni la kweli: Dunia ina chanzo chake. Je, Chanzo hiki kikoje? Kinapaswa kuwa hakijawahi kuumba au kuwa tegemezi kwa kitu chochote au mtu ye yote, hakione kani kwa macho na kina nguvu sana isiyofikirika. Hicho Chanzo ni lazima kiwe na akili ya hali ya juu sana ili kuweza kuleta huo muundo na utaratibu wenyе mchangamano tata katika dunia. Tunaweza hata kujenga hoja hapa kwamba hicho Chanzo ni mtu. Sababu moja ya Chanzo kuwa ni lazima kiwe ni nafsi ni kwamba viumbe vyenye nafsi kama sisi – wenyе nguvu, akili, na utashi – haingeweze kana kutoka katika kitu ambacho hakina sifa hizi. Hii nafsi binafsi, kiumbe chenye nguvu zote atakuwa ni Mungu!

Hii ndiyo Hoja ya Kosmolojia kuhusiana na uwepo wa Mungu. Hapa kuna maswali ya kuuliza wakati unapozungumza na watu kuhusiana na chanzo cha kwanza:

"Je, unakubaliana na wimbi la wanasayansi kwamba kulikuwa na muda ambao dunia ilianza kuwepo lakini kabla ya hapo haikuwahi kuwepo?"

Kama watasema "Ndio," waulize:

"Je, mnaamini kwamba kitu (kama dunia) kinaweza kutoka pasipokuwa na chochote?"

Kama watasema "Hapana," waulize:

"Kwa hiyo kama kuna kitu kwa sasa kipo, basi kitu fulani kilikuwa kipo nyakati zote, sahihi?

"Je, kitu ambacho kila siku kimekuwepo kinaweza kuwa na nguvu, akili na utashi wa kuweza kusababisha kila kitu katika dunia?

"Je, hufikiri ya kwamba kama hiki kinachojulikana kuwa ni cha milele, kiumbe mwenye nguvu sana, alijihangaisha kutuweka sisi hapa, anapaswa atueleze sisi ni kwa nini alifanya hivyo?

"Kwa mujibu wa Biblia, sababu za Mungu kutuweka sisi hapa duniani ni kuwa na uhusiano binafsi na yeye."

Ushahidi wa Uwepo wa Mungu: Hoja ya Teleolojia

Hoja yenyewe kufanana na Hoja ya Kosmolojia inaitwa **Hoja ya Teleolojia**. Neno Teleolojia linatokana na neno la Kiyunani *telos* likiwa na maana ya "kusudi." Linahusika na malengo au muundo.

Hoja ya Teleolojia inauliza, "Ni kwa jinsi gani dunia ilipata uratibishaji makini wa muundo wake?" Inahitimisha kwamba "muundo tata katika dunia unahitaji Msanifu," Lazima kuwepo na lengo au kusudi linaloongoza dunia yetu. Tuone mifano ya kisayansi ni hii.


"Tuseme hakukuwepo na akili nyuma ya dunia, hakuna akili ya ubunifu. Katika hali hiyo, hakuna mtu aliyesanifu ubongo wangu kwa madhumuni ya kufikiri. Lakini, kama ni hivyo, nitaaminije kufikiri kwangu mwenyewe? Ni kama kuharibu lagi la maziwa na ukategemea kwamba kwa jinsi lilivyopasuka itakupa ramani ya London. Lakini kama siwezi kuamini kufikiri kwangu mwenyewe, siwezi nikaamini hoja zinazoelekeza kwenye imani kuwa hakuna Mungu muumba. Sina sababu ya kuwa mtu asiyesadiki kwamba Mungu yupo, au kitu kingine chochote. Kama sitaamini katika Mungu, sitaweza kuamini katika mawazo: kwahiyio kamwe siwezi kutumia wazo kutokuamini katika Mungu."

- C.S. Lewis, *The Case for Christianity*

Jicho

Jicho la binadamu²⁷ lina muundo tata sana. Kila sehemu ya jicho inasimamia dhumuni lake katika muundo mzima wa jicho. Hakuna shemu ya jicho "inaweza kugeuka" isipokuwa jicho liwe kamilifu. Irisi ya jicho haina kazi yejote bila utendaji wa jicho lote.

Sehemu zote za jicho zitakuwa zilikamilika kwa wakati mmoja. Namna hii inaelezea uumbaji, na siyo mabadiliko (evolution). Haiwezekani umbile la muundo kama hili na kusudi lake liwe limekuwepo kwa bahati.²⁸ msanifu pekee ambaye angeweza kutengeneza muundo wenye utata kiasi hicho ni Mungu mwenyewe.



VINASABA

Kipunje kimoja cha kinasaba (DNA)²⁹ kina tabia nyingi kuliko kompyuta yejote ya kisasa. Taarifa zote za kila mwili wa binadamu zimekusanywa katika kipunje cha kinasaba cha mwanadamu ambacho kinachukua nafasi ndogo sana kuliko nukta inayowekwa mwishoni mwa sentensi iliyoandikwa.

Kiwango cha taarifa ambazo zinaweza kuhifadhiwa kwenye kipini cha kichwa cha ujazo cha kinasaba ni sawa na lundo la mkusanyiko wa vitabu mara 500 ya umbali kutoka ardhini hadi kwenye mwezi. Hoja ya Teleolojia inasema kwamba utata wa Vinasaba vya mwanadamu unahitaji msanifu wa akili ya juu sana. Msanifu pekee mwenye uwezo wa kutengeneza muundo huo ni Mungu peke yake.



Mazingira ya Ardhi

Je, Umeshawahi kufikiria kwa kuzingatia maajabu ya mahali inapokaa dunia? Kama ingekuwa tuwe karibu na jua tungeungua. Kama tungekuwa mbali sana na jua, tungeganda kwa barafu hadi kifo. Hali ya hewa ya dunia iko sahihi katika kutuwezesha kuendesha maisha yetu. Kila kitu muhimu kwa ya maisha yetu kinapatikana katika ardhi ya dunia. Hii inamaanisha kwamba ardhi na hali ya hewa viliwekwa kwa ajili yetu na kiumbe mwenye akili sana aliyeiumba dunia katika muundo wake. Uwepo wa ardhi ya dunia yetu siyo matokeo ya kubahatisha. Ardhi ya dunia iliumbwaa kwa madhumuni yake na Mungu.

²⁷ Image: "Human eye diagram-sagittal view-NEI", National Eye Institute, National Institutes of Health, retrieved from https://commons.wikimedia.org/wiki/File:Human_eye_diagram-sagittal_view-NEI.jpg, public domain.

²⁸ Kujifunza zaidi kuhusu muundo wa Mungu kwa jicho, tembelea: www.answersingenesis.org/go/eye.

²⁹ Image: "Acido desoxirribonucleico (DNA)" by Kadumago retrieved from [https://commons.wikimedia.org/wiki/File:%C3%81cido_desoxirribonucleico_\(DNA\).png](https://commons.wikimedia.org/wiki/File:%C3%81cido_desoxirribonucleico_(DNA).png), licensed under CC BY 4.0, desaturated from the original.

Ushahidi wa Uwepo wa Mungu: Hoja ya Maadili

Hoja ya Maadili kwa ajili ya uwepo wa Mungu inauliza, "Kwa nini wanadamu wana ufahamu wa ndani yao wa kujua mema na mabaya?" Inajibu, "Ufahamu wa wanadamu wa kujua mema na mabaya unatoka kwa Mungu, Mto sheria Mkuu anayetupa sisi maadili."

Hoja hii ililetwa na C.S. Lewis katika kitabu chake cha *Ukristo-mradi (Mere Christianity)*. Aliandika kuhusiana na hisia ya "mambo yanayotakiwa" ambayo watu kutoka katika kila mila wanayo. Ingawaje mila nyingi tofauti mara nyingine zinatofautiana katika lipi ni jema na lipi ni baya, watu wote katika mila zote wanajua kwamba "wanatakiwa" kufanya mambo, au "wanatakiwa wasifanye" mambo kadhaa. Hii hisia ya "kutakiwa" inatoka wapi? Hoja ya Maadili inasema kwamba hii hisia ya maadili ya kujua mema na mabaya inatoka kwa Mto sheria Mkuu.

Hapa kuna hoja rasmi ya kimantiki:

Kigezo mantiki A: Ikiwa Mungu hayupo, hakuna misingi ya maadili na uwajibikaji.

Kigezo mantiki B: Misingi ya maadili na uwajibikaji ipo.

Hitimisho: Kwa hiyo Mungu yupo.

Kigezo mantiki A kinasema kwamba ukimwondoa Mungu, hakutakuwa na uwezekano wa kuwepo kwa maadili na majukumu ya msingi. Maadili hayangeweza kuwa ya kufanana kwa kila mtu kama hakungekuwepo na Mto sheria mwenye akili zinazozidi za wanadamu ambaye kwake yeche sisi sote tunawajibika. Maagizo ya kufuata maadili yanakuwa ya maana tu kama kuna mtu wa kutoa amri na mtu mwingine wa kupokea amri hiyo. Kama kuna baadhi ya amri ambazo zinatakiwa zitumike kwa usawa kwa kila mtu katika dunia, ni lazima kuwepo na mtu mwenye akili zinazozidi wanadamu wote ambako amri zote zitatoka kwake na ambaye watu wote watawajibika kwake. Zaidi ya hapo, hatia ya kimaadili inakuwa ni sahihi pale tu ambapo sheria kutoka kwa mtu mwingine imekiukwa. Hatia haiji tu kutokana na kuvunja sheria. Ni lazima mtu (mwenye mamlaka) ahusike.

Kigezo mantiki B kinasema kwamba misingi ya maadili na uwajibikaji ipo. Ni ya halali, iwe mtu yeyote anaiamini au haiamini; inagunduliwa, na siyo kwamba inabuniwa. Hata wale wenye itikadi kwamba Mungu hayupo wanakiri haya. Kwa mfano, mtu mmoja asiyekiri kuwa kuna Mungu Peter Cave alisema, "*Hoja zozote za kutia shaka zinazoweza kuletwakinyume na imani yetu kwamba kumuua mtu asiyekuwa na hatia kimaadili ni vibaya, tuna uhakika zaidi kwamba kuua ni vibaya kimaadili kuliko hata hoja yenyewe inavyojieleza... Kumtesa mtoto mdogo asiyekuwa na hatia kwa ajili ya kujifurahisha ni vibaya kimaadili.*" Baadhi ya mambo yanatambulika kama ni makosa katika mila zote na kwa nyakati zote.

Kama Kigezo mantiki A na B zote ni za kweli, basi hata hitimisho kwamba Mungu yupo ni lazima pia liwe hitimisho la kweli.

► Soma Warumi 2:12-16. Paulo anafundisha nini kuhusu sheria ya maadili iliyoandikwa katika mioyo ya wale wote ambao hawana kitabu cha Biblia?

Upinzani #1 kuhusiana na Uwepo wa Mungu: Uovu na Mateso

Upinzani ulio wa kawaida sana kuhusiana na uwepo wa Mungu ni huu: "Kama yuko Mungu mzuri na mwenye nguvu zote, kwa nini duniani kuna maovu na mateso? kuwepo kwa maovu kunadhihirisha kwamba hakuna Mungu mzuri, mwenye nguvu zote." Mara nyingi, upinzani huu unawakilishwa kama ifuatavyo:

Kigezo mantiki A: Mungu mzuri hawezi akaruhusu mateso duniani

Kigezo mantiki B: Mngu mwenye nguvu zote angeweza akaondoa mateso yote

Hitimisho: Kwa hiyo hakuna Mungu mzuri, mwenye nguvu zote

Watu hutarajia Mungu mzuri, mwenye nguvu zote, mara moja aanze kushughulika na maovu na mateso. Wanasema kwamba kama Mungu angekuwa ni mzuri na mwenye nguvu zote, angeweza kuiweka dunia iwe mbali na mateso na maovu. Ni kwa jinsi gani tulijibu swali hili, "Kwa nini kuna maovu duniani?"

► Ni kwa jinsi gani utalijibu swali hili? "Kama kweli Mungu ni mzuri na mwenye nguvu zote, kwa nini anaruhusu maovu yawepo duniani?"

Hapa kuna baadhi ya majibu kuhusiana na upinzani huu:

Maovu ni matokeo ya Chaguo la Hiari la Mwanadamu kutomtii Mungu

Kuna maovu katika dunia kwa sababu wanadamu wa kwanza waliipuzia uhuru wao na kuchgua kutomtii Mungu. Mateso ni matokeo ya mwanadamu kukosa utii.

Adamu na Hawa walikataa kumtii Mungu, na matokeo yake, dunia nzima ikalaaniwa.³⁰ Hata watu ambao hawakuwa na hatia wanateseka kwa sababu ya laana hii.

Baadhi ya watu watauliza, "Lakini kwa nini Mungu alifanya viumbe huru, kama Mungu angefanya wanadamu bila kuwa na nguvu ya kuchagua dhambi, hakungekuwepo na mateso duniani."

Jibu moja katika swali hili ni kwamba Mungu aliumba mwanadamu kwa ajili ya upendo na mahusiano. Haiwezekani kuwepo na upendo pasipo uhuru wa kuchagua. Mungu alitoa kwa binadamu uhuru wa kuchagua upendo – au kuchagua uasi.

Tatizo la Maovu linadhihirisha kwamba Mungu Yupo

Kumbuka Hoja ya Maadili kwa ajili ya uwepo wa Mungu. Tatizo halisi la ouvu linaonyesha kwamba Mungu yupo. Hatutaweza kujua kama uovu upo bila ya kuwepo kwa viwango kamili vyaa mema na mabaya. Viwango kamili vyaa mema na mabaya ni lazima vitoke kwa Mto sheria kamili, ambaye ni Mungu.

³⁰ Soma Mwanzo 3:14-19 na Warumi 8:20-23.

Kama hakuna Mtoa sheria, huwezi kusema kuna uovu duniani. Bila ya Mtoa sheria, unachokiita wewe uovu, mimi naweza kukiita kizuri. Kama nitaamua kuiba fedha kutoka kwako, aidha siyo jema au baya; ni kiasi cha kufanya uchaguzi tu. Ni Mtoa sheria peke yake ndiye panga kuwa hili ni baya na hili ni jema.

Ni pale tu tunapokubaliana na sheria ya maadili ya mema na mabaya tunapokutana na uwepo wa uovu. Tatizo la uovu linatambua kwamba Mungu mzuri yupo. Lakini, kama Mungu ni mzuri na mwenye nguvu zote, kwanini aruhusu uovu duniani?

Mungu Ametoa Jibu kwa Tatizo la Uovu na Mateso

Baadhi ya watu watauliza, "Kwa nini Mungu hafanyi lolote kuhusiana na Uovu na Mateso katika dunia? Kwa nini anaruhsu mateso yaendeleee?"

Jibu ni kwamba Mungu *tayari* ameshafanya kitu kuhusiana na jambo hilo. Kupitia Yesu, Mungu mwenye upendo usiokuwa na kikomo, aliingilia kati kwenye historia ya mwanadamu na akawa sehemu ya dunia iliyovunjika tunayoishi. Alichukua mwenyewe mateso na hata kifo, kisha akakiharibu kifo katika kufufuka kwake. Kwa sababu ya upatanisho wa Mungu na binadamu kwa maisha na kifo cha Kristo, tunaweza kuwa huru mbali na dhambi na siku moja kuепukana na mateso kabisa.

Kwa nini inachukua muda hivi kwa maumivu ya mateso yetu kuondoka? Bado tunaishi katika ulimwengu ulioanguka; na Mungu bado kwanza anashughulika na dhambi, kama chimbuko la mateso yetu. Kushughulika na dhambi kunachukua muda kwa sababu watu ni wagumu.

Pamoja na ukweli kwamba mateso ni matokeo ya maadili ya uovu haina maana kwamba mateso yote ni matokeo ya dhambi ya mtu mmoja. Kila mtu anayo maumivu kwa sababu ya dhambi ya Adamu, siyo lazima iwe ni kwa sababu ya dhambi binafsi, iwe ni kwa mwanamume au mwanamke. Katika ulimwengu wetu ulioanguka, hata watu wasiokuwa na hatia wanaumia pasipo haki kwa sababu ya dhambi za watu wengine. Lakini mateso yote kwa vyovoyote yataondoka kwa wale wote wanaomruhusu Mungu ashughulikie dhambi ndani ya mioyo na maisha yao wenyewe.

Hata pale tunapokutana na maumivu sasa, tunayo faraja ya Mungu. Kama Wakristo, tunao uhakika kwamba, "katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao."³¹ Ingawaje inawezekana tusilielewe hili, Mungu analo kusudi lake katika yale anayoruhusu yapitie katika maisha yetu. Yeye huyatumia hata maumivu katika maisha yetu katika kuwavuta watu wengine kwenye mahusiano na yeye mwenyewe. C.S. Lewis alisema, "Mungu hunong'ona nasi tuwapo katika furaha, anasema ndani ya dhamira zetu, lakini hupiga kelele wakati wa maumivu yetu. Ni kipaza sauti cha Mungu kuiamsha dunia isiyosikia."³²

³¹ Warumi 8:28

³² C.S. Lewis, *The Problem of Pain*, (NY: Macmillan Publishing, 1962), 93

Elimu ya Kuitetea Imani katika Vitendo – Ushuhuda wa Lee Strobel

Nukuu kutoka katika ushuhuda alioutoa Lee Strobel (mzaliwa wa 1952):³³

Karibu maisha yangu yote sikuamini kabisa kwamba Mungu yupo. Nilifikiri kwamba wazo la muumbaji aliye na upendo na mwenye nguvu zote ni la kipuuzi. Ukrejea nyuma, mimi nina taaluma ya uandishi wa habari na sheria. Mimi ni mtu mwenye kushuku. Nilikuwa mhariri wa taarifa za kisheria katika gazeti la Chicago Tribune. Kwa hiyo, nilihitaji ushahidi kabla ya kuamini jambo lolote.

Siku moja mke wangu akasema kwamba ameamua kuwa mfuasi wa Yesu Kristo. Niifikiri huu ndio ungekuwa mwisho wa ndoa yetu, Lakini kitambo kidogo kikapita nikaanza kuona mabadiliko chanya katika maadili yake, katika tabia, na katika njia za kuhusiana na mimi pamoja na watoto. Ilikuwa inavutia na nikataku kuanza utafiti kuhusiana na imani yake mpya.

Nilienda kanisani siku moja na nikasikia ujumbe kuhusiana na Yesu katika njia ambayo niliweza kuielewa. Nilisikia kwamba msamaha ni zawadi ya bure, kwamba Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, na kwamba tunaweza kurithi pamoja naye uzima wa milele. Bado niliendelea kutoamini kuwa Mungu yupo, lakini nilitoka nje nikisema, "Kama haya ni kweli, yaana maana kubwa katika maisha yangu."

Kwa takribani miaka miwili, nilitumia mafunzo yangu ya uanahabari na sheria katika kuchunguza usahihi wa Ukristo. Ilipofika Novemba 8, 1991, niligundua kwamba kuwa mtu nisiyeamini Mungu yupo, inapasa kuukana ushahidi wote unaoonesha ukweli wa injili. Lakini sikuweza kufanya hivyo. Kwa kuwa nilifundishwa katika uandishi wa habari na sheria kukubaliana na ukweli. Kwa hiyo, katika siku hiyo, nikampokea Yesu Kristo kama mwenye kunisamehe na kiongozi wangu. Kama ilivyokuwa kwa mke wangu, maisha yangu yakaanza kubadilika. Maadili yangu, tabia zangu, na makusudi ya maisha yangu yakaanza kubadilishwa. Kila ninapoangalia nyuma, siwezi nikayalinganisha maisha yangu ya awali na muujiza na furaha iliyopo ya kumfuata Yesu Kristo.

Hitimisho

Wakati Jia akijiandaa kumjibu Lee, alihisi Roho Mtakatifu akimwambia kwamba jibu kwa ajili ya swali la Lee lilikuwa la kiakili zaidi. Kwa hiyo anapaswa azungumze na moyo wake zaidi na siyo kwa ajili ya kichwa tu.

Jia akamwambia Lee, "Kwanza, nataka wewe utambue kwamba ninajisikia kama umeumia. Wewe ni rafiki yangu na wakati ukiwa umejeruhika, na mimi pia ninakuwa nimejeruhika. Zaidi ya hapo, nataka ujue kwamba Mungu anausikia moyo wako pia. Mungu Baba alikuwa

³³ Nakala hii imenukuliwa kutoka katika ushuhuda wa Lee Strobel, "Atheist to Evangelical." Imechukuliwa kutoka <https://youtu.be/E8IE9Y4wudk> March 5, 2021.

akiangalia tu wakati mtoto wake mpendwa akifa pale msalabani. Anajua maumivu ya kumpoteza mtu aliye karibu na yeye.

"Siwezi nikaelezea maumivu yote katika dunia yetu, lakini najua kwamba Mungu aliumba ulimwengu pasipo mateso. Aliumba ulimwengu uliokamilika bila kifo, Kwa masikitiko, baba yetu wa kwanza, Adam, aliasi dhidi ya Mungu na akaileta dhambi katika dunia hii. Dhambi ikaileta mateso na kifo. Adamu alijua mapema na kabla ya kuvunja amri ya Mungu kwamba dhambi yake itasababisha kifo kiwepo duniani. Mwanadamu akauharibu ulimwengu uliokuwa mkamilifu ambao Mungu aliumba. Kila mmoja wetu akaendeleza ule mnyonyoro wa dhambi iliyoanza na Adamu. Kila mmoja wetu huivunja sheria ya Mungu.

"Kwa sababu ya dhambi ya Adamu, tunazaliwa ndani ya dunia yenyewe maumivu. Tunaishi katika dunia iliyoharibika. Lakini, Lee, Je, ninaweza kukuelezea mambo mawili ya kukumbuka kuititia machozi yako?

"Kwanza, Mungu mwenyewe alifanyika sehemu ya maumivu ya dunia yetu. Alimtuma Mwanae kuwa sehemu ya dunia yetu. Alimtuma Mwanae aje afe ili dunia yetu siku moja iweze kuwa huru kutokana na laana ya dhambi

"Pili, kwa sababu Mungu alimtuma Mwanae, unaweza ukapata uzima wa milele. Biblia hiyo hiyo inayoonya kuhusu adhabu ya dhambi inaahidi kwamba kwa wale wote watakaomwamini Yesu Kristo watakuwa na uzima wa milele. Kitabu hiki kinaahidi kwamba siku moja Mungu 'atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena.'³⁴

"Lee, jaribu kufikiria juu ya Mungu anayetupenda sana ambaye amemtuma Mwanawe aje afe na kuleta tiba kwa ajili ya kifo. Huyo ni Mungu aliye na nguvu zote, lakini aliyejitoa mwenyewe kwa upendo kwa ajili yetu sisi. Na kwamba Mungu anakupenda kwa upendo wa kushangaza."

Kazi za kufanya Somo la 3

(1) Elimu ya Kuitetea imani na Kichwa: Utaanza kipindi kinachofuata kwa mtihani kutokana na maswali ya tafakuri yaliyoko katika Somo la 3. Jifunze maswali haya kwa uangalifu kwa maandalizi ya mtihani.

(2) Elimu ya Kuitetea imani na Moyo: Mara nyingine ni rahisi "Kuelezea" uovu na mateso; ni vigumu zaidi kuwa na hisia pamoja na mateso. Omnia kwamba Mungu aweze kukupa moyo wa huruma kwa ajili ya wale wanaoteseka. Omnia kwamba azungumze kuititia wewe kwa ajili ya kuleta farijiko kwa walioumizwa.

(3) Elimu ya Kuitetea imani na Mikono: Zungumza na mtu asiyeamini kuhusiana na hoja za uwepo wa Mungu. Shirikisha wengine hoja tatu zilizoko katika somo hili. Ikiwezekana, shirikisha hoja hizi kwa mtu asiyeamini uliyezungumza naye kuhusiana na somo liliopita.

³⁴ Ufunuo 21:4

Mtihani wa Somo la 3

- (1) Ni swali gani linaloulizwa na Hoja ya Kosmolojia?
- (2) Ni kwa jinsi gani Hoja hii ya Kosmolojia inajibu swali hili?
- (3) Kuna mambo gani matatu yasiyokuwa na mantiki kwa ajili ya dunia?
- (4) Wasilisha hoja ya Kosmolojia kwa kufasiri vigezo mantiki 2 na hitimisho.
- (5) Ni swali gani linaloulizwa na Hoja ya Teleolojia?
- (6) Ni kwa jinsi gani Hoja ya Teleolojia inajibu swali hili?
- (7) Ni swali gani linaloulizwa na Hoja ya Maadili?
- (8) Ni kwa jinsi gani Hoja ya Maadili inajibu swali hili?
- (9) Wasilisha Hoja ya Maadili kwa kufasiri vigezo mantiki 2 na hitimisho.
- (10) Ni upinzani gani ulio wa kawaida sana kuhusiana na uwepo wa Mungu?
- (11) Toa majibu matatu kuhusiana na swali hili, "Inawezekanaje Mungu mzuri na mwenye nguvu zote akawepo kama kuna maovu katika dunia?"
- (12) Nukuu kutoka kichwani Warumi 1:19-20.

Somo la 4

Elimu ya Kuitetea Imani ya Uumbaji

Utangulizi

Jia aликуwa anatembea kwenye hifadhi ya pori siku ya Jumapili asubuhi. Wakati akiwa anaangalia maua, alianza kumsifu Muumbaji na akaanza kufikiria juu ya taarifa ya uumbaji katika kitabu cha Mwanzo. Mara akakutana na Lee akiwa anatembea kuja kwake.

Jia akaita, "Lee, je, hifadhi hii ni nzuri si ndiyo! Unadhani ilifikaje hapa?"

Lee akacheka, "Labda unafikiria kwamba Mungu wako asiyonekana ndiye aliumba vitu vyote hivi?" Lakini mimi najua sayansi; kila mwana sayansi mahiri anajua kwamba dunia imekuwa ikigeuka geuka kwa mabilioni ya miaka. Viumbe vimekuwa vikikua na kugeuka kutoka maumbo rahisi na hadi viumbe vyenye maumbo utata. Uzuri wote huu umetokea kwa bahati nasibu na kwa muda wa mabilioni ya miaka.

"Tofauti kati yetu Jia, ni kwamba: imani yako katika uumbaji imeegemea kwenye imani kipofu; uhakika wangu katika mageuko haya yameegemea ukweli usioepukika. Hakuna mwanasayansi yeyote anayeamini katika uumbaji!"

Jia akasema, "Hilo linafurahisha sana. Nikuambie kitu – tuwekeane dau la changamoto. Jumapili ijayo mchana, tukutane tena kwenye hifadhi hii. Nitajibu changamoto yako: 'Taja hata mwanasayansi mmoja muhimu aliamini katika uumbaji!' Lakini utakutana na changamoto kutoka kwangu: Nipe mfano mmoja wa kitu chochote kisichokuwa na uhai ambacho kimeweza kugeuka na kuwa kiumbe hai. Ninaamini kwamba imani yako katika mageuko (*mabadiliko*) imeegemea 'iman' kama na mimi ilivyo imani yangu katika uumbaji! Tuyazungumzie hayo Jumapili ijayo"

► Unafikiri nini kuhusiana na kauli ya Jia? Je, imani ya mageuko imeegemea kwenye imani, au yaweza kuthibitishwa kisayansi? Vipi kuhusianana uumbaji?

Imani katika Uumbaji au Imani katika Mageuko

Katika somo hili, tutajifunza ushahidi kwamba sisi tuliumbwa na Mungu. Ni jambo la kushangaza kwa ugumu wa wanadamu walio nao wa kujaribu kumkataa Muumbaji wetu. Vitabu vingi vimeandikwa na watu wanaopinga kwamba tuliumbwa na Mungu.

Wanamageuko hudai kwamba uumbaji siyo sayansi ya kweli. Wanadai kwamba sayansi ya kweli haiwezi kuwa na maelezo yoyote ambayo akili haiwezi kuelewa. Kwao, kila kitu ni lazima kiwe na maelezo yatokanayo na vianzo vya asili. Hata hivyo, madai kwa pande zote mbili za mageuko na uumbaji ni lazima tuyakubali kwa imani. Vyote ni "maoni yanayotokana imani." Tunamaanisha nini kusema hivi?

Siyo mageuko wala uumbaji vinavyoweza "kuthibitishwa kisayansi." Kwa pamoja uumbaji na mageuko hujaribu kuelezea mambo yaliyowahi kutokea nyakati za nyuma. Hili ni suala la *kihistoria* na siyo suala la *kisayansi*.³⁵

Hakuna mwanadamu ye yote anayeishi kwa sasa aliyeona ulimwengu ulivyotengenezwa. Hakuna hata mmoja wetu aliyewahi kuona uumbaji au mageuko ya mwanadamu. Aidha tunalazimika:

1. Kuamini taarifa ya mtu mwagine kwa ajili ya kupata chanzo cha dunia - au
2. Kutafuta dalili nyingine zinazotuzunguka katika dunia.

Je, tunaweza kuamini Suala zima la Uumbaji katika Biblia?

Inaingia akilini kwamba kama Mungu alituumba sisi katika kiwango cha kuweza kufikiria asili na kusudi letu, atatueleza sisi uumbaji. Katika Biblia, Mungu anaelezea kuutengeneza ulimwengu na kila kitu kilichomo kwa siku sita. Katika somo lijalo, tutajifunza ushahidi kwamba Biblia iliandikwa na Mungu. Kama tunaweza kuwashawishi watu wengine kwamba Biblia inatokana na Mungu, tunaweza kuwatia nguvu kuamini kile ambacho Mungu alisema kuhusu mahali ambapo kila kitu kilitoka.

Wakristo wanaoamini katika uumbaji wanasema kwamba tunaweza kuamini taarifa ya Mungu kuhusiana na mwanzo wa dunia. Tunaamini kwamba maneno yake katika kitabu cha Mwanzo 1-2 ni taarifa ya kweli ya uumbaji. Tuna imani na taarifa ya uumbaji kwa sababu tunayo imani katika Mungu aliye kivuvia kitabu cha Mwanzo.

Je, kuna viashiria vingine vinavyotuzunguka katika dunia?

Wakati tunajaribu kuwashawishi wasiokuwa Wakristo kuhusu usahihi wa Biblia, tunapaswa pia tuwaelekeze kwenye ulimwengu unaotuzunguka na kuwasaidia waweze kuona kwamba taarifa za vianzo katika Biblia ndizo zenyne mantiki sana kuliko nyingine kuhusu dunia yetu. Hatuwezi kutumia njia ya kisayansi peke yake katika kupima tukio la *kihistoria* la uumbaji kwa sababu hatuwezi tukauona mwanzo wa ulimwengu. Hata hivyo, tunaweza kuwaonyesha watu jinsi ushahidi wa kisayansi unavyounga mkono mtizamo wa kibiblia kuhusu uumbaji.

Mpelezei huwa anatafuta ushahidi wa alama za vidole katika tukio la halifu ili

"Kama ukisoma sayansi kwa undani sana na kwa muda mrefu, itakulazimisha wewe kumwamini Mungu."

- Lord William Kelvin

"Katika kukosekana kwa ushahidi mwagine wowote, [muundo wa] kidole gumba peke yake kinatosha kunishawishi mimi kuhusu uwepo wa Mungu."

- Sir Isaac Newton

"Sayansi kidogo tu hukuweka mbali na uwepo wa Mungu, lakini inavyoendelea kuongezeka zaidi ya hapo inakupeleka kwake."

- Louis Pasteur

³⁵ Kurudia mada hii, angalia somo la 2 kuhusu "Dhana potofu dhidi ya Elimu ya Kuitetea Imani."

kuweza kumpata mtu aliyefanya mauaji. Ushahidi unaopatikana huelekeza kwenye ukweli, Tunaweza kuangakia ushahidi wa kisayansi kama wa DNA kuonyesha kwamba, siyo bahati nasibu na muda wa miaka, ni Mungu alitenda tendo la uumbaji, Alama za vidole za Mungu zinapaitkana kila mahali katika ulimwengu huu.

Mtazamo moja wapo wa kuangalia ushahidi kutokana na dunia inayotuzunguka ni kuangalia yale ambayo wanamageuko na wanauumbaji wangeyaona kama imani yao ungekuwa ya kweli.

► Kama msimamo wa mageuko ungekuwa wa kweli, tutegemee kuona nini katika dunia yetu inayotuzunguka? ³⁶ Kama msimamo wa uumbaji ungekuwa wa kweli tutegemee kuona nini katika dunia inayotuzunguka? ³⁷

Baada ya kujua ni nini kila nadharia inadokeza, tunaweza kuuliza, "Je, yale tunayoyaona karibu na sisi yanakidhi matarajio ya *mageuko au uumbaji?* Je, ni mtazamo gani wenyewe Ushahidi usioyumba? Je, matokeo ya uchunguzi wa wanasayansi yanaoana na mageuko au uumbaji?"

Tunaposoma ushahidi wa dunia yetu inayotuzunguka, tunaona kwamba dunia enaelezeka vizuri kwenye uumbaji na siyo kwenye mageuko. Kwa hakika, nadharia ya mageuko siyo ya kisayansi. haikubaliani kabisa kwenye ushahidi uliomo katika dunia yetu.

Kiashiria cha #1: Sheria ya uhai hutoa Uhai

Miaka mia moja iliyopita, watu wengi waliamini kwamba uhai unaweza kwa mara moja kutokea kwenye kitu ambacho kilikuwa hakiishi. Walidhani kwamba kama utaacha sanduku la matakataka pembezoni mwa eneo lolote kwa muda mrefu, linaweza kuzalisha panya – kutokana na matakataka hayo yasiyokuwa na uhai.³⁸

Louis Pasteur, mwanasayansi maarufu ambaye alikuwa pia Mkristo mwaminifu, alifanya majaribio mengi yaliyothibitisha sheria ya **uhai hutoa uhai**.

Wanamageuko huikataa sheria hii ya muhimu ya sayansi wanaposema kwamba uhai hauna budi utoke katika vitu visivyo na uhai angalao mara moja. Wanamageuko wengi hudhania kwamba uhai unaotokana na vitu visivyo na uhai huanza mapema vikiwa katika hali ya kemikali mchanganyiko. Ingawaje wanajua sheria hii ya uhai hutoa uhai, hawako tayari kukubali kwamba Mungu alitengeneza uhai. Badala yake, wanasisitiza kwamba uhai ilitokana na vitu visivyokuwa na uhai. Hata hivyo, hakuna hata mwanasayansi mmoja aliyewahi kuunda uhai kutoka kwenye kitu kisichokuwa na uhai.

³⁶ Baadhi ya majibu sahihi ni: mabadiliko ya mpito katika kumbukumbu za mtu wa zamani, ushahidi wa maumbile ukitoa maelezo mapya, urahisi kuliko utata, ukaaji usiokuwa na utaratibu maalumu wa jinsi dunia inavyofanya kazi, n.k.

³⁷ Baadhi ya majibu sahihi ni: Ushahidi wa kubuni, viwango vya mabadiliko ndani ya aina za mimea na wanyama, ushahidi wa aina tofauti katika kumbukumbu za mtu wa zamani, uanzishwaji wa sheria za sayansi zinazoonyesha kwamba ulimwengu uliwekwa mahali ulipo na Msanii Mchoraji Mkuu asiyebadilika, n.k.

³⁸ "Uhai kutoa Uhai" maana yake ni kwamba uhai hauna budi utoke katika vitu visivyo na uhai.

MWONEKANO WA UHAI	
MAGEUKO YANATABIRI	UUMBAJI UNATABIRI
Uhai hutoka katika vitu visivyo na uhai.	Uhai hutoka katika Uhai peke yake.
USHAHIDI WA DUNIA YETU UNAONYESHA	
Uhai hutoka katika Uhai peke yake.	

Kiashiria cha #2: Sheria za Mwendojoto

Tulijifunza Sheria ya Mwendojoto katika somo la 3, lakini acha tuzitafakari tena.

- Sheria ya kwanza ya mwendojoto ni ipi?³⁹

Sheria ya kwanza ya mwendojoto inasema kwamba mata /nguvu aidha haiwezi kuumbwa au kuharibiwa. Mata iliyopo ilitoka mahali fulani; haiwezi kujitengeneza yenyewe. Hii inamaanisha kwamba mata na nguvu viliumbwa na chanzo cha nje, yaani Mungu. Mata mpya na nguvu mpya haviwezi kutoka mahali pasipokuwa na kitu.

- Sheria ya pili ya mwendojoto ni ipi?⁴⁰

Sheria ya pili ya mwendojoto inalezea kwamba nguvu iliyokwishatumika katika dunia inageuzwa tena polepole kuwa nguvu isiyoweza kutumika tena. Inabadilika kutoka nguvu inayotumika hadi nguvu isiyotumika. Kwa mfano, mwanga wa jua hutengenezwa kutoka katika nguvu kubwa sana ya jua; lakini sehemu kubwa ya nguvu huishilia huko angani, na hata kile kinachofika duniani mara nyingi hakihifadhiwi kwa ajili ya matumizi. Nishati ambayo haiwezi kutumika katika ulimwengu inajulikana kama "hali ya kuharibika" ("entropy").

Kwa pamoja, hizi sheria mbili zinasema kwamba kuna kiasi yenyе mwisho cha mata na nguvu katika ulimwengu ambacho kinaendelea inazidi kuwa haiwezi kutumika. Ulimwengu unazidi kuzorota. Kwa hiyo, ni kwa jinsi gani hili linahitilafiana na dhana ya mageuko?

Wanamageuko wanaoamini kwamba hakuna Mungu lazima waseme (1) mata/nguvu havitokani na chochote - au (2) mata/nguvu wakati wote vimekuwepo. Chaguo la kwanza linahitilafiana na sheria ya kwanza ya mwendojoto. (Mata haiwezi ikapatikana pasipo na kitu.)

Chaguo la pili linahitilafiana na sheria ya pili ya mwendojoto. Kama ulimwengu wakati wote umekuwepo ukiwa na kiasi cha kudumu cha nguvu, na zaidi sana nguvu hii haitumiki, basi

³⁹ Jibu sahihi ni: Sheria ya kwanza ya mwendojoto inasema kwamba mata /nguvu haiwezi aidha kuumbwa au kuharibiwa.

⁴⁰ Jibu sahihi ni: Sheria ya pili ya mwendojoto inasema kwamba nguvu iliyokwishatumika katika dunia hugeuzwa polepole kuwa nguvu isiyotumiwa tena.

hadi sasa ulimwengu ungekuwa umezorota kabisa na hatungekuwepo. Wanamageuko hawako kisayansi wakati wanapohiilafiana na sheria za mwendojoto.

NGUVU	
MAGEUKO YANATABIRI	UUMBAJI UNATABIRI
Mata/nguvu havitokani na chochote au nyakati zote vimekuwepo.	Mata/nguvu kwa polepole vinakuwa havitumiki na ulimwengu unashuka chini.
USHAHIDI WA DUNIA YETU UNAONYESHA	
Kuna kiasi cha kudumu cha nguvu iliyotumika katika ulimwengu. Nguvu hii inazidi kuwa haitumiki zaidi na zaidi.	

Kiashiria cha #3: Kumbukumbu za Mabaki na Alama za Kale za Kiumbe

Kwa mujibu wa nadharia ya mageuko, aina mbalimbali za wanyama wa sasa polepole waligeuzwa kutoka maumbo rahisi, wakianzia na seli moja. Kama ndivyo ilivyo, tunategemea tuone aina mbalimbali ya maumbo ya mpito (kuanzia maumbo rahisi hadi tata kabisa) katika kumbukumbu za mabaki na alama za kale za kiumbe. Lakini baada ya miaka 150 ya uchimbuaji, wanasayansi hadi sasa bado hawajapata ushahidi za maumbo ya mpito.

Kukosekana kwa mabaki na alama za kale zinazoonyesha maumbo ya mpito za mageuzi kunapingana na utabiri wa mageuzi. Kwa kufanya ulinganifu, wanaouna mkono dhana ya uumbaji wanatabiri kwamba kunapaswa kuwepo na viumbe vinavyotofautiana kwa kila siku ya uumbaji, ambayo haitahitaji maumbo ya mpito wa mageuzi.

- Soma kitabu cha Mwanzo 1 na orodhesha kila kitu alichoumba Mungu kwa kila siku kwenye wiki yote ya uumbaji.

WIKI YA UUMBAJI	
Siku ya 1	Nuru
Siku ya 2	Anga
Siku ya 3	Bahari, nchi, na mimea
Siku ya 4	Jua, mwezi, na nyota
Siku ya 5	Viumbe vyta baharini na angani
Siku ya 6	Wanyama wa nchi na mwanadamu
Siku ya 7	Mungu alipumzika

Kwa hiyo, ni nini tunachokipata kutoka katika kumbukumbu za mabaki na alama za kale za viumbe? Tunaona aina mbalimbali za viumbe vinavyotofautiana na mimea inayotofautiana. Kumbukumbu za mabaki na alama za kale za viumbe zinaashiria kwamba dhana ya uumbaji wa kibiblia ni ya busara zaidi kuliko dhana ya mageuko/mageuzi.

MABAKI NA ALAMA ZA KALE ZA VIUMBE	
MAGEUKO YANATABIRI	UUMBAJI UNATABIRI
Maumbo mengi ya mpito ya mageuko	Mimea na wanyama vinavyotofautiana
USHAHIDI WA DUNIA YETU UNAONESHA	
Viumbe vinavyotofautiana na mimea inayotofautiana bila maumbo ya mpito ya mageuko	

Kiashiria cha #4: Sheria za Jenetikia (chembe za urithi katika mwili)

- Kama kulikuwa na mbwa wawili tu kwenye safina ya Nuhu, ni kwa nini kwa sasa tunao mbwa wengi sana wa aina tofauti?

Watu wengi wa dhana ya mageuko wanasema kwamba tofauti zilizopo mionganoni mwa wanyama, kama vile mbwa, ni uthibitisho kwamba mageuko yalifanyika kuitia uchaguzi wa asili. Wanasema kwamba mabadiliko ya maumbile husababisha aina mpya za mimea na wanyama.

Hata hivyo, mabadiliko mengi tunayoyaona kwa wanyama ni kwa sababu ya taarifa za maumbile ambazo siku zote zimekuwa kwenye DNA zao. Kwa mfano, angalia aina mbalimbali za mbwa. Je tofauti zilizopo kati ya hawa mbwa beagle na bulldog ni matokeo ya mabadiliko ya kawaida? Hapana. **Sheria za Mendel za Jenetikia** zinazeleza kwamba muungano wa vinasaba mbalimbali hutengeneza maumbo mbalimbali kwa mtoto. Mbwa aina ya *Cocker spaniel* hana tofauti sana na *collie* kwa sababu ya mabadiliko katika vinasaba (mutations), lakini ni kwa sababu sehemu fulani ya jamii ya mbwa ilitengwa kutokana na wengine na wakaanza kuzalishana kwa kuchanganya damu. Vinasaba vya *cocker spaniel* vilikuwa tayari ni sehemu ya dimbwi la vinasaba vya mbwa. Ingawaje mabadiliko katika vinasaba yanaweza kuwa na athari katika jamii, wingi wa tabia tunazoziona kwenye mchanganyiko wa mbwa wengi tofauti ni matokeo ya kuzaliana.

Kuzaliana kunaweza kumbadilisha mbwa kwa muda maalumu tu. Haijalishi mwenye mbwa atamzalisha mara ngapi, mbwa wake bado wataendelea kuwa mbwa. Mbwa hawesi akawa paka kuitia kuzaliana!

Mabadiliko katika vinasaba mbalimbali hayawezi kufanya kile ambacho wenyewe dhana ya mageuko wanasema wanaweza kufanya. Mabadiliko yanaweza kubadili kinasaba na kwa hali hiyo kuweza kubadili taarifa ya DNA, lakini mabadiliko katika vinasaba hayawezi kuongezea taarifa mpya kwenye DNA. Kwa mfano, mabadiliko katika vinasaba yanaweza kusababisha ng'ombe azaliwe na mguu wa ziada, lakini hayawezi kusababisha ng'ombe

akawa na gamba la kobe. Kimsingi, ng'ombe hana vifaa vya maumbile vya kuweza kuzalisha gamba la kobe. Kuna mipaka ya kwa kiasi gani kiumbe kiweze kubadilika.

Watu wenyе dhana ya uumbaji wanategemea kuwepo na mipaka ya kubadilika ndani ya viumbe mbalimbali tofauti. Uchunguzi wa maisha yanayotuzunguka unaonyesha kwamba kuna mipaka katika mabadiliko.

Watu wenyе dhana ya mageuko wanategemea kuona ushahidi wa kubadilika kutoka aina ya kiumbe mmoja muhimu kuwa kiumbe kingine. Ushahidi wa utabiri wa wanamageuko haupo.

JENETIKIA	
MAGEUKO YANATABIRI	UUMBAJI UNATABIRI
Kuna mabadiliko kutoka aina ya kiumbe kimoja kuwa kiumbe kingine	Kuna mabadiliko yenye mipaka ndani ya aina ya kiumbe
USHAHIDI WA DUNIA YETU UNAONESHA KUWA	
Kuna mabadiliko yenye mipaka ndani ya viumbe mbalimbali tofauti.	

Kiashiria cha #5: Ulimwengu Mchanga

Ili kutoa muda kwa wanyama kugeuka kwa bahati nasibu, watu wenyе dhana ya mageuko wanadai kwamba ulimwengu una umri wa mabilioni ya miaka. Tumeshona kwamba mageuko yatakuwa hayawezekani hata kama ulimwengu utakuwa na umri wa mabilioni ya miaka. Lakini kuna sababu nyingi za kuamini kwamba ulimwengu ni mchanga. Asilimia 90% ya mbinu zilizotumika kutafuta umri wa ulimwengu zinatoa sababu za kuthibitisha kwamba ulimwengu hauwezi ukawa na umri wa mabilioni ya miaka.

DNA ndani ya bakteria wa "Kale"

Wanasayansi wa dhana ya mageuko walipata bakteria ndani ya jiwe la chumvi liliolofikiriwa kuwa na umri wa miaka milioni 250, lakini walishangazwa na ugunduzi wao kwamba bakteria waliokutwa walikuwa bakteria [sawa] na bakteri wa sasa. Wanasyansi walishangazwa pia kwamba DNA ya huyo bakteria ilikuwa bado haijabadilka kabisa. Kama kweli mawe ya chumvi ambako bakteria hao walipatikana yalikuwa yamewekwa na mafuriko ya mvua yaliyotokea miaka 4500 iliyopita, basi kutakuwepo na uwezekano mkubwa wa kuwa bila mabadiliko na kuwa sawa na bakteria wa sasa.

Tishu laini katika mifupa ya Dinosaur

Mwaka 2005, Dr. Mary Schweitzer alikuta chembechembe nyekundu za damu na himoglobini kwenye mifupa ya dinosaur iliyoko Montana. Hii imesababisha kuwepo tatizo kubwa kwenye nadharia ya mageuko. Kisayansi, tishu laini haziwezi kudumu kwa zaidi ya miaka elfu chache. Kwa uhakika haiwezi kudumu kwa miaka milioni 65 tokea wakati wenyе dhana ya mageuko walipofikiria kwamba *dinosaur* wa mwisho aliishi.

Kiwango cha Chumvi katika Bahari

Chumvi inamiminika kwa wingi kuelekea baharini kuliko inavyotoka. Bahari hajakaribia kuwa ya chumvi kabisa kwa sababu hili lilikuwa lifanyike kwa mabilioni ya miaka. Ulimwengu hauwezi kuwa na umri wa mabilioni ya miaka kutegemeana na kiwango cha chumvi kilichoko kwenye bahari.

Maafa Makubwa ya Mafuriko ya Dunia

Mafuriko ya Nuhu yanakubaliana na hoja kuwa ulimwengu ni mchanga kwa sababu kama Mafuriko ya dunia [yaliuharibu] ulimwengu, na kusababisha matabaka mengi katika safu ya kijiolojia, basi haya matabaka hayakutandikwa chini kwa mamilioi ya miaka.

Kama matabaka ya miamba yaliwekwa haraka na kupangana bila kuvunjika, inaonesha ushahidi pia kwamba aina tofauti za mimea na wanyama vilizikwa na haya mafuriko makubwa yenye takataka za chini (*mashapo*), basi safu ya kijiolojia haipaswi ielezewe kama ya mamilioni ya miaka ya maendeleo ya polepole ya viumbe wengine, bali badala yake ielezwe kwa kurejea kwenye mafuriko ya madhara makubwa ambayo yalizika na kuhifadhi masalia ya mimea na viumbe vikiwa havina dosari ye yote ndani ya ulimwengu mchanga.

Maswali machache kwa Wana-mageuko

Kuna maswali machache ambayo watu wanaoamini katika dhana ya mageuko (*mabadiliko*) wanapata muda mgumu kuyajibu, kwa sababu mageuko siyo ufanuzi unaotosheleza ukweli. Kama utazungumza na mtu anayekubaliana na dhana ya mageuko, maswali haya yanaweza kuwasadia kufikiri kuhusiana na kile wanachokiamini na kuhoji imani zao.

1. Ni kwa jinsi gani mihemuko kama ya upendo inakua?
2. Ni kwa jinsi gani kufikiri kwa hali ya juu kunakua?
3. Ni kwa jinsi gani hatua ya usanidimwanga (photosynthesis) inabadilika?
4. Ni kipi kilanza kukua kwanza, mimea au wadudu wanaokaa juu yake na kusambaza mbelewele kwenye mimea?
5. Je, unaweza kunipa mfano wa mabadiliko katika vinasaba ambayo yameongeza kwa upya maelezo ya maumbile kwa kiumbe?
6. Ni kwa jinsi gani utaelezea mwanzo wa asili wa seli hai ya kwanza kutoka katika mata isiyokuwa na uhai?
7. Kwa nini baadhi ya wana-mageuko ambao hutambua kwamba uhai usingetokea katika maisha yasiyokuwa na uhai katika ulimwengu huu hutoa maoni kuwa maisha yalihamishwa kutoka ulimwengu mwingine – wakati wanajua kwamba wanalisogeza tu tatizo kwenye upande mwingine wa ulimwengu?
8. Kama unaamini kwamba mata/nguvu vimekuwpo siku zote, utashughulikaje na Sheria ya Mwendojoto inayosema kwamba, kuna kiwango maalumu cha nguvu katika

ulimwengu, lakini nguvu hii inazidi kutotumika zaidi na zaidi. Je, ulimwengu hautakuwa umeenda chini hadi sasa?

9. Je, unao uhakika na majibu yako kwamba yana mantiki, ni sahihi, na yamethibitika kisayansi, au una imani kipofu katika nadharia ya mageuko?

Imani kwa Muumbaji

Katika somo hili, tumeona kwamba mageuko hayaendani na kweli za kisayansi. Utabiri wa watu wanaoiamini dhana ya mageuko hauungwi mkono na ushahidi wa dunia yetu. Wanategemea kuona ushahidi kwamba uhai unaweza ukatoka katika vitu ambavyo havina uhai; wanategemea muda na bahati nasibu ya kuweza kutengenezwa kitu chenye utata; wanategemea mabadiliko yaweze kuelezea mageuko kutoka seli moja ya kiumbe hadi kuwa mwanadamu; na wanategemea kupata aina za maumbo ya mpito kati ya makundi makubwa ya mimea na wanyama. Pamoja na hayo, bado matazamio yao hayajatekelezeka.

Watu wenyе dhana ya mageuko wanapingana na sheria za mwendojoto; wanapingana na sheria za maumbile; wanapingana na rekodi za masalia ya mtu wa zamani, na wanapingana na ushahidi wa ulimwengu mchanga. Hawana uwezo wa kujibu maswali magumu yanayohusiana na nadharia yao kwa sababu nadharia yao siyo ya ukweli.

Wale wote wanaoamini kwamba Mungu alitumia mageuko wamekubaliana na nadhria za kibinadamu kuhusu umri wa ulimwengu na mageuko, wakati huo huo wakipuuzia mafundisho ya wazi ya Biblia.

Ushahidi kutoka kwa dunia inayotuzunguka, kwa uwazi kabisa inaunga mkono imani katika Mungu na uumbaji wake kuliko mageuko. Mategemeo ya watu wenyе kuamini dhana ya uumbaji wanaungwa mkono na utafiti wa kisayansi. Wakristo wanatambua kwamba uhai ni lazima utokane na uhai; na kwamba hatimaye maisha yetu ya kimwili na maisha yetu ya kiroho yanatoka kwa Mmoja ambaye ndiye Njia, Kweli, na Uzima. Tunatambua kwamba haijatokea sisi kuwepo kwa kubahatisha.

Tunaamini katika yeye aliye msanifu Mkuu. Tunakubaliana na sheria za mwendojoto na kanuni za mabadiliko. Hizi zote hazijapingana na imani yetu. Kumbukumbu za masalia ya kale ya mimea na wanyama ni sawa na imani yetu kwamba Mungu aliumba kila kitu kama kinavyoonekana. Tunaamini kwamba Bibila inafundisha kuwa ulimwengu kwa kiasi kikubwa ni mchanga, kwahiyo ushahidi kwa ajili ya ulimwengu ulio mchanga hautusumbui. Wanaoamini katika uumbaji kwa pamoja wanaye Mungu na sayansi upande wao! Tunayo imani katika taarifa ya uumbaji kwa sababu tuna imani katika yeye aliye Muumbaji.

Elimu ya Kuitetea Imani katika Vitendo – Ushuhuda wa Richard Lumsden

Sikiliza ushuhuda wa mwanasayansi msomi ambaye alikutana na ushahidi na akawa mwamini mwenye msimamo wa dhana ya uumbaji na Ukristo.

Dr. Richard Lumsden⁴¹ (1938-1997) alikuwa profesa wa elimu ya vimelea na seli za viumbe (*biolojia*) katika Chuo Kikuu cha Tulane. Alitumika kama mshauri kwa wahitimu wa shahada ya uzamili, na ameandika majarida mengi ya kisayansi. Alifundishwa dhana ya mageuko ya Darwini. Sayansi ilikuwa ndiyo dini yake. Dr. Lumsden aliamini kwamba dhana ya mageuko ya Darwini ndiyo kanuni ya kisayansi iliyokuwa imejengeka, na mara nyingi alikejeli imani za Kikristo.

Siku moja, mwanafunzi (*msichana*) alikuja ofisini kwake kuuliza maswali kuhusiana na mhadhara wa siku hiyo uliokuwa juu ya mageuko. Mwanafunzi hakupingana na chochote alichofundisha. Badala yake, aliuliza mfululizo wa maswali:

- Je, maisha yalitokeaje?
- Je, DNA si ni kitu tata sana kiasi kwamba hakiwezi kujitokeza kwa bahati?
- Kwa nini kuna nafasi za kumbukumbu za masalia ya kale ya viumbe na mimea kati ya makundi tofauti?
- Ni vitu gani vinakosekana kati ya sokwe na mwanadamu?

Mwanafunzi hakupenda kushindana; aliuliza maswali tu. Dr. Lumsden akatoa majibu yenyewe viwango vya mageuko kwa mujibu wa yale maswali. Lakini hakuwa anajisikia mwenye furaha kutokana na mazunguzo yale. Hakuwa amejiandaa kwa maswali ya uhakika kama yale. Wakati alipokuwa anajibu, alianza kufikiri, "Haya ni makosa. Ninachojua kuhusu biolojia ni kinyume kabisa na ninayosema."

Baada ya muda, mwanafunzi alimshukuru mwalimu kwa majibu yake na akaondoka. Kwa nje, Dr. Lumsden alionekana mwenye uhakika; lakini kwa ndani, alikuwa ameteketea. Alijjua kwamba kile alichokuwa amemweleza mwanafunzi huyu kilikuwa cha uongo. Dr. Lumsden alikuwa na unyofu wa kukabiliana na mashaka yake. Alianza kusoma na kujifunza hoja zote zinazoshabihiana na mageuko. Mwishowe, alitambua kwamba kwa kutegemea ushahidi wa kisayansi, anapaswa aukane u-Darwini. Dr. Lumsden akawa mwamini wa dhana ya uumbaji.

Lakini baadaye Dr. Lumsden alikabiliwa na swali jingine jipya. "Kama dunia ilikuwa imeumbwa, ni nani Muumbaji?" Muda mfupi baadaye, mtoto wa kike wa Lumsden alimpa ukaribisho wa kushiriki kanisani. Hapo awali, hakuwa na moyo wa kupenda dini; lakini sasa alitamani kujua kama Biblia ilikuwa kweli. Je, Mungu wa Biblia ndiye aliyeiumba dunia?

Dr. Lumsden alisikia habari njema kwamba Mungu alimtuma Mwanaye kulipa adhabu ya dhambi zetu na kutoa msamaha kwa wanadamu na uzima wa milele. Mwisho wa ibada, mchungaji aliwaita waliokuwa bado hawajaamini ili kumpokea Kristo mbele ya hadhara. Asubuhi ile, mtu aliyeokuwa haamini kama Mungu yupo na mwenye kuitikadi dhana ya

⁴¹ Imechukuliwa kutoka "From Evolution to Creation: The Testimony of Dr. Richard Lumsden" (November19,2009).Retrievedfromhttp://www.wayoflife.org/database/from_evolution_to_creation_lumsden.html April 25, 2020.

mageuko, anauna ushahidi wa uumbaji, akainama mbele za Muumba wake akageuka kuwa mwamini.

Hitimisho

Jumapili iliyofuata, Jia alikuja bustanini mapema. Alikuwa na shauku ya kukutana na Lee! Lakini alipomwona Lee, Jia alijua kwamba hakuwa na shauku kubwa sana. "Kuna tatizo gani? Je, umeleta jibu la swali langu? Jia aliuliza.

Lee akasema, "Nimejisomea kwa wiki nzima, lakini sijaweza kupata mfano hata mmoja wa kitu kisichokuwa na uhai kuweza kuwa kiumbe chenye uhai. Ninaanza kuihoji sayansi yangu. Yawezekana imani yangu katika mageuko iko kwenye msingi wa imani ya Darwini badala ya ushahidi wa kisayansi. Sitaki hivyo!"

Jia akacheka, "Nadhani uko sahihi. Unaamini katika Darwini; Mimi ninaamini katika Muumbaji. Nadhani dunia inatoa sababu za kutosha kuamini katika suala la uumbaji wa Mwanzo."

Ghafla Le akafunguka, "Sawa,ninaweza nisiwe na jibu la swali lako, lakini nadhani na wewe pia hukuweza kupata jibu la swali langu! Je, uliweza kumpata hata mwanasayansi mmoja maarufu sana anayeamini katika taarifa ya uumbaji?"

Jia akacheka. "Uko sahihi, Lee. Sikumpata mwanasayansi mmoja anayeamini katika dhana ya uumbaji. Nimepata *dazani* ya wanasyansi maarufu wanaoamini katika dhana ya uumbaji! Kwa jinsi wanasyansi wanavyozidi kujifunza kuhusu hii dunia, ni kwa jinsi hiyo hiyo wanavyozidi kutambua kwamba ushahidi unaelekeza kwa Muumbaji. Siwezi nikakuchosha kwa orodha ndefu; lakini jaribu kuona kama unayatambua majina haya, Lee."

Jia alianza kuorodhesha baadhi ya wanasyansi mashuhuri katika historia:

- Copernicus, ambaye mwanzo alitambua kwamba jua liko katikati ya ulimwengu.
- Galileo, anayechukuliwa kama "Baba wa Sayansi ya sasa."
- Johannes Kepler, ambaye mwanzoni alielezea mwenendo wa sayari.
- Sir Isaac Newton, aliyeandaa sheria ya nguvu ya uvutano.
- Robert Boyle, anayedhaniwa kwamba ndiye mkemia wa kwanza wa zama hizi.
- Louis Pasteur, aliyetengeneza chanjo ya kwanza ya kichaa cha mbwa na kimeta.
- Max Planck, aliyeanzisha mitambo ya kisasa.

"Lee," Jia alihitimisha, "Kama ukiuchunguza ushahidi, utaona kwamba akili za wanasyansi maarufu katika historia zimeelewa kwamba maelezo pekee ya uzuri na utata wa dunia yetu ni kwa Mungu wa nguvu za milele na uumbaji. Kuna sababu nzuri na za msingi za kumwamini Muumbaji."

Kazi za kufanya Somo la 4

(1) Elimu ya kuitetea imani na Kichwa: Utaanza kipindi kinachofuata kwa mtihani kutokana na maswali ya tafakuri yaliyoko katika Somo la 4. Jifunze maswali haya kwa uangalifu kwa maandalizi ya mtihani.

(2) Elimu ya kuitetea imani na Moyo: Unaweza ukawa unao marafiki au wanafamilia ambao wameshawishika kwamba mageuko ni kweli. Kabla ya kushirikishana nao taarifa ya somo hili, omba msaada wa Roho Mtakatifu. Mwombe Mungu awavuvie ukweli kuhusu uumbaji mkuu wa Mungu.

(3) Elimu ya kuitetea imani na Mikono: Fikiria kuhusu mtu yejote aliye na maswali yanayohusiana na uumbaji. Mwulize mtu huyo kama unaweza kushirikishana naye yote yeli uliyojifunza katika somo hili. Kama mtu huyo anaamini katika mageuko, uliza maswali kutoka sehemu ya mwisho ya somo hili. Toa taarifa darasani ya mwingiliano wako na huyu mtu.

Mtihani wa Somo la 4

(1) Inamaanisha nini kusema kwamba kwa pamoja mageuko na uumbaji ni "maoni yanayotokana imani"?

(2) Sheria ya uhai hutoa uhai inafundisha nini?

(3) Kwa mujibu wa sheria za _____, kuna kiasi fulani cha kudumu cha mata na nguvu katika ulimwengu. Nguvu hii inazidi kuendelea kutotumika zaidi na zaidi.

(4) Kwa mujibu wa nadharia ya mageuko, ni masalia gani tunayopaswa tuyatafute?

(5) Je, Maelezo ya Biblia kuhusiana na uumbaji yanatabiri nini kuhusiana na mabadiliko ya maumbile?

(6) Toa mifano mitatu ya ushahidi wa kisayansi kuhusu ulimwengu mchanga.

(7) Nukuu kutoka kichwani Mwanzo 2:1-3.

Somo la 5

Hoja za Ujumla kuhusu Imani ya Kikristo

Angalizo kwa Mwanafunzi

Somo hili fupi linatambulisha hoja ambazo zitatolewa katika Somo la 6-8. Unaweza usilielewe somo hili kwa ukamilifu hadi hapo utakapojifunza masomo yanayofuata. Ili kuelewa vyema hoja kuhusu Imani ya Kikristo, soma somo hili, kariri kazi za kufanya zilizotolewa, soma masomo 6-8, kisha fanya marejeo ya somo hili tena. Baada ya kuwa umesoma hoja zote katika masomo yote yafuatayo, unaweza ukarejea kweye somo hili kwa ajili ya uelewa mpana zaidi.

Utangulizi

Wakati msichana Lee alipokutana na Jia nje ya jingo lao la kuishi, alionekana kuwa yuko makini sana. Baada ya kuonana kwa muda mfupi, alisema, "Naweza nikakuuliza swali? Tafadhalii nipe jibu la kweli."

"Hakika!" Lee alijibu kwa mashaka. Ingawaje mara kwa mara alikuwa akihojiana na Jia, aliheshimu sana imani yake ya Kikristo. Ni jambo lililokuwa wazi kwamba kwa moyo safi alimjali sana Lee kama mtu. Kijana alikuwa na matumaini kwamba msichana wake hatakuwa na hasira dhidi yake. Aliendelea, "Kuna jambo lolote baya?"

"Hakuna lolote baya, lakini nimekuwa nikifikiria. Tunazungumzia kuhusu imani ya Kikristo, lakini una uhakika kwamba unatafuta ukweli? Kama maswali yako si chochote zaidi ya kuifanyia akili mazoezi, kamwe hutaweza kujua kwa ukweli Mtoaji wa Ukweli. Je, moyo wako unatafuta ukweli?"

Lee alifikiria kwa dakika kadhaa. Mara nyingine anaionea wivu imani ya Jia katika Mungu; lakini hakuwa na uhakika kama alkuwa tayari kuikubal dini ya Jia, hata kama atajibu maswali yake yote. Lee akasema, "Mimi sijui. Nadhani nitakubaliana na ukweli hata kama siupendi. Lakini sina uhakika."

Jia akajibu, "Nadhani inabidi ujiulize wewe mwenyewe, kama 'Je, mimi kweli ninautafuta ukweli?' Bila ya uaminifu wa akili, mazungumzo yetu hayataenda zaidi ya udadisi wa akili tu. Fikiri kuhusu swali hili kisha tuongee kesho."

Kujenga Shauri juu ya Imani ya Kikristo


Kama unataka kuwakilisha shauri juu ya Imani ya Kikristo, ni vyema ukawa na hoja nzuri juu ya uvuvio wa Biblia na ukweli wa Ukristo. Watu wengi leo husema, "Haijalishi kama dini ni ya kweli. Kinachojalisha ni kama dini yako ina manufaa na wewe." Wanasisitiza, "Hakuna mambo yaliyo makamilifu kabisa, kwa hiyo hatuwezi kujua kama dini yejote ni ya kweli."

Hata hivyo, tulijifunza katika Somo la 2 kwamba hoja hii ni batili. Ukweli kuhusiana na dini yetu ni jambo la msingi sana. Kama Ukristo siyo wa kweli, basi Wakristo ni wapumbavu kwa kufuata dini ya uongo.

Katika somo hili, tutaanza kujenga shauri kuhusiana na imani ya Kikristo. Tutaona kwamba Ukristo ni imani ya maana. Tunaweza tukaamini kwamba Ukristo ni wa kweli. Shauri letu linadai kwamba:

1. Biblia ni Neno la Mungu.
2. Yesu ndiye njia peke yake ya kuingia Mbinguni.
3. Imani ya Kikristo ni ya kweli.

Masomo yanayofuata yatatupa ushahidi kamili wa kila umbo kwa kila kipengele katika shauri letu la Ukristo. Kwa sasa, utajifunza kuhusu kila umbo linalotumika katika shauri letu.



Umbo la kwanza katika shauri letu ni **Historia Inayoaminika**. Agano Jipyä linaaminika kihistoria. Kama Biblia haiaminiki katika historia yake, hatuna chochote cha kutegemea. Lakini kama Agano Jipyä kihistoria ni sahihi, tunao ushahidi wa kutosha kuamini kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu na akatimiza unabii mwingi unaohusiana na Masihi.

Maumbo ya **Unabii** na **Kufufuka** yanaonyesha kwamba Yesu ni yeye yule aliyesema alikuwa – Masihi, Mwana wa Mungu, Mungu aliyejidhihirisha kwa njia ya mwili. Maumbo ya Unabii na Ufufuo yanaunga mkono ukweli kwamba **Yesu ni Mungu**.

Sehemu nyingine ya shauri letu inasema **Yesu hafanyi makosa**. Kwa kuwa Yesu ni Mungu, tunajua kwamba yeze hawezi kukosa. Kuwa asiyeweza kukosa *inamaanisha kwamba Yesu hawezi kukosea*. Yesu alisema kwamba *Biblia ni Neno la Mungu* na kwamba yeze ndiye *njia pekee ya kumwona Mungu*.

Ukweli kwamba Yesu ni asiyeweza kukosea inaunga mkono umbo la juu la shauri letu: **Ukristo ni wa kweli!** Yesu, Mwana wa Mungu, alifanyika mwili wa mwanadamu, akafa msalabani, akafufuka kutoka kaburini ili tuweze kusamehewa na kupatanishwa tena na Mungu. Huu ndio ujumbe wa Imani ya Kikristo.

Je, imani ya Kikristo ni ya kweli?

Maumbo sita yanawakilisha mfuatano wa vigezo mantiki zinazoelekeza kwenye hitimisho lenye mantiki. Kwenye masomo ya 6-8, tutaona ushahidi kwa kila Kigezo mantiki. Kwa somo hili, kariri kila Kigezo mantiki na hitimisho lake.

Kigezo mantiki A: Agano Jipyä inaaminika kihistoria

Huu ndio msingi wa shauri letu katika Imani ya Kikristo. Kama Biblia haiaminiki katika historia yake kwamba ni sahihi, basi hatuna shauri. Kama Biblia inaaminika katika historia yake kwamba ni sahihi, tunaweza kusema kwa nguvu zote kuhusu ukweli wa Imani ya Kikristo.

Kigezo mantiki B: Yesu alitimiza unabii unaohusiana na Masihi.

Maisha ya Yesu, huduma, na kifo chake vilitimiza msururu wa dazani za unabii zilizotolewa kwa mamia ya miaka kabla ya kuzaliwa kwake.

Kigezo mantiki C: Yesu alifufuka kutoka kwa wafu.

Kutokana na usahihi wa Agano Jipyä, tunaweza tukauamini ushahidi kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu.

Kigezo mantiki D: Ufufuko wa Yesu na kutimia kwa unabii kunaonyesha kwamba alikuwa Masihi, Mwana wa Mungu, na Mungu aliyejuka katika hali ya mwili.

Kama Yesu alifufuka kutoka kwa wafu na akatimiza unabii za Agano la Kale kuhusiana na Masihi, ni lazima awe Mwana wa Mungu.

Kigezo mantiki E: Kwa kuwa Yesu ni Mungu, hawezi akafanya makosa.

Kutoweza kufanya makosa ni kukaa bila kuwa na dosari yeyote. Kama Yesu ni Mungu, maneno yake kwa hakika ni thabiti na ya kutegemewa.

"Sijawa Mkristo kwa sababu Mungu aliahidi kwamba nitakuwa na maisha ya furaha kuliko niliyo nayo wakati nikiwa siamini kwamba Mungu yupo. Hakuwahi kuahidi kitu kama hicho... Niligeuka kuwa Mkristo kwa sababu ushahidi ulikuwa ni kuvutia sana kwamba Yesu kwa hakika ni mmoja tu na aliye Mwana wa Mungu aliyethibitisha uungu wake kwa kufufuka kutoka katika wafu. Hiyo inaamanisha kumfuata yeze lilikuwa ni jambo la busara na hatua yenye mantiki ambayo ningeweza kuichukua."

- Lee Strobel

Kigezo mantiki F: Yesu Kristo alifundisha kwamba Biblia ni Neno la Mungu na kwamba peke yake ni njia pekee ya kumwona Mungu.

Kwa kurudiarudia, Yesu alithibitisha kwamba Maandiko Matakatifu ni Neno la Mungu.⁴² Kwa kurudiarudia, Yesu aliwaeleza wasikilizaji wake kwamba yeye peke yake ni njia ya kumwona Mungu⁴³.

Hitimisho: Kama Yesu alikuwa Mungu, ni lazima tuamini alichokisema: Biblia ni Neno la Mungu, na Yesu ndiye peke yake njia ya kumwona Mungu. Kwa hiyo, Ukristo ni wa kweli.

Kama kila Kigezo mantiki hapa juu ni kweli, hitimisho ni lazima liwe la kweli. Kila Kigezo mantiki kinajenga Kigezo mantiki kiliyopita, ikianzia na usahihi wa historia ya Biblia.

Kwanza, tutajifunza ushahidi wa Agano Jipyka kihistoria ni sahihi. Wakosoaji wanasema, "Biblia imenakiliwa mara nyingi sana kiasi kwamba hajulikani ni Biblia ipi iliandikwa mwanzo," au "maelezo yaliyoko kwenye Agano Jipyka ni matukio yaliyopitana kwa muda." Matukio halisia yalikuwa si chochote zaidi ya mambo ya kufikirika katika Agano Jipyka."

Je, unaweza kutoa majibu ya maelezo haya? Haya ni upinzani wa kawaida kuhusu usahihi wa historia wa Agano Jipyka. Katika somo linalofuata, tutajifunza jinsi ya kuonesha kwamba Biblia inaaminika kihistoria.

► Jadili kila kauli kwenye vigezo mantiki sita zilizoonyeshwa na hitimisho lake. Hakikisha unaelewa ni kwa nini hitimisho ni lazima liwe kweli kama kauli ni za kweli. Kariri hizo kauli sita na yanayofuata. Utahitajika kuandika kauli hizi na hitimisho lake kwenye chemsha bongo ya somo hili.

Elimu ya Kuitetea Imani katika Vitendo – Ushuhuda wa Anayetafuta-Ukweli

Jordani Monge⁴⁴ alikuwa mtu asiyeamini kwamba Mungu yupo hadi kufikia elimu ya juu ya sekondari. Wakati Wakristo walipokuwa wakizungumza naye kuhusiana na Biblia, alikuwa anaweza kushinda hoja zao zote.

Mwaka wa 2008, Jordani alijiunga na Chuo Kikuu cha Harvard kwa masomo yanayohusiana na utawala. Kaulimbiu ya kile Chuo cha Havard ni *Veritas*, "Ukweli." Kama mwanafunzi asiyeamini kwamba Mungu yupo, katika Chuo Kikuu cha Havard, Jordani Monge alikutana uso kwa uso na ukweli wa umilele.

Akiwa Harvard, Jordani akawa rafiki wa mwanafunzi mwingine, Yusufu Porter, aliyekuwa Mkristo mwaminifu. Siyo tu kwamba Porter alikuwa Mkristo, bali alikuwa na akili sana na aliweza kujibu hoja za Monge zilizokuwa dhidi ya uwepo wa Mungu. Kila Jordani alipokuwa

⁴² Mathayo 5:18, 15:4; Marko 12:36; Luka 24:44-46

⁴³ Yohana 14:6

⁴⁴ Nyenzo hii imechukuliwa kutoka kwa ushuhuda wa Jordan Monge, uliochukuliwa kutoka <https://www.christianitytoday.com/ct/2013/march/atheists-dilemma.html> April 25, 2020.

akileta hoja baada ya hoja kwake. Alimsikiliza kwa heshima kubwa na akamjibu kwa uangalifu. Alikuwa hajawahi kukutana na Mkristo wa aina hii.

Dada Monge alikuwa haamini kwamba Mungu yupo, lakini aliamini kwamba kuna sheria za maadili zisizobadilika zinazoitawala dunia. Yusufu alimwonesha kuwa madai kuwa kuna mambo mema na mambo mabaya hayatapatana bila kuamini kuwa kuna Mungu aliyeumba madili hayo yasiyobadilika. Pia alimwonyesha isivyowiana kwa kuamini kwamba dunia iliumbwa kwa "Mlipuko Mkubwa" bila kuonyesha kwamba kuna mtu au kitu kilichosababisha Mlipuko Mkubwa kutokeea.

Kwa sababu ya hoja hizi, Jordani akawa muumini asiyekubali ufunuo. Aliamini kwamba Mungu yupo, lakini bado akamkataa Yesu kama Mungu aliyefanyika mwili.⁴⁵ Kwa jinsi alivyoendelea kusoma, hata hivyo, alijifunza kwamba Wakristo wanafafanua upendo kama "kuwa mwaminifu kwa jambo la ukweli la mtu mwingine." Dada Monge alitambua kwamba hii ndiyo sababu ya Mungu kumtoa sadaka Mwanae kufa kwa ajili ya wenye dhambi. Mungu "aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanae wa pekee." Huo ndio upendo wa kweli.

Siku moja, Jordani akasoma kwa mara ya kwanza habari ya kusulubiwa. Alianza kulia alipotambua uzuri wa sadaka ya upendo ya Mungu.

Kwa miezi kadhaa iliyofuata, Jordani alichunguza maandiko ya Wakristo maarufu kama Augustine, Blaise Pascal, na C.S.Lewis. Alianza kutambua kwamba imani ya Kikristo siyo tu kwamba ni nzuri; ni ya ukweli. Kwenye Pasaka ya 2009, Jordani Monge alibatizwa kama mwamini mpya. Kwa mara ya kwanza, alijua "Ukweli," (*Veritas*).

Hitimisho

Asubuhi iliyofuata, Lee alikuwa anangojea kwenye barabara ya pembezoni kwa ajili ya Jia. "Nimeshafikiria kuhusu swali lako. Sidhani kwamba unaweza kuthibitisha ukweli wa imani ya Kikristo kwa sababu ninafikiri ni kama hadithi ya kusimuliwa tu. Hata hivyo, Nataka niwe mtu mkweli, kama utaweza kunionyesha kwamba imani ya Kikristo ni ya kweli, nitakiri kosa langu, na nitajaribu kuamini."

Jia alijibu kwa furaha, Lee "Hilo ndilo ninalohitaji. Naamini kwamba Mungu wa Ukweli atajifunua mwenyewe kwa mtu yeyote ambaye kwa dhati anaitafua kweli. Nimekuwa nikichunguza sababu za kuamini imani ya Kikristo. Kama Mungu atanisaidia, nafikiri naweza nikakuonyesha kwamba kuna sababu nzuri ya kuamini kwamba Mungu yupo na kwamba Yesu Kristo aliishi, alikufa na alifufuka kutoka kaburini ili kutuleta kwenye mahusiano na Mungu. Tuongee tena wiki ijayo kuhusu Biblia na inaonyesha nini kuhusu ukweli wa Yesu Kristo Masihi."

⁴⁵ Deist anakubaliana na "nguvu za kiungu," lakini haamini kwamba Mungu hujifunua mwenyewe kama mtu kwa wanadamu. Deist hukataa Mungu kuwa na umbo la mwanadamu na aina zote za mafunuo maalumu, lakini anakubalina na ufunuo wa ujumla wa nguvu za asili.

Kazi za kufanya Somo la 5

(1) Elimu ya kuitetea imani na Kichwa: Utaanza kipindi kinachofuata kwa mtihani kutokana na maswali ya tafakuri yaliyoko katika Somo la 5. Jifunze maswali haya kwa uangalifu kwa maandalizi ya mtihani

(2) Elimu ya kuitetea imani na Moyo: Wakati wa kumshuhudia mtu asiyeamini, kuna hatari ya kuanzisha mashindano ya kutumia ufahamu wa akili. Hii inamfanya kujishuku kwa kujisikia kwamba kama ukweli wa imani ya Kikristo utamshawishi, atakuwa ‘amepoteza’ hoja. Mwombe Mungu akupe wepesi wa hisia kwa ajili ya roho za watu unaowashuhudia. Elimu ya kuitetea imani ni lazima iwe ya mawasiliano ya moyo kwa moyo na siyo kichwa kwa kichwa.

(3) Elimu ya kuitetea imani na Mikono: Baada ya kuwa umehakiki hoja za imani ya Kikristo, shirikisha hizi kauli kwa mtu asiyeamini. Ikiwezekana, ongea na mtu asiyeamini ambaye ulizungumza naye katika masomo yaliyopita. Uliza, “Kama nitaweza kukuonyesha kwamba kila umbo katika maumbo haya ni kweli, utakuwa tayari kusikiliza kile nitakachowakilisha kwako? Kumbuka kwamba lengo lako siyo kushinda hoja iliyopo, bali kupata nafasi ya kushirikisha ukweli. Toa taarifa kuhusu mazungumzo yenu katika kipindi cha darasa kitakachofuata.

Mtihani wa Somo la 5

(1) Kuna sehemu ngapi tatu za shauri la Imani ya Kikristo katika somo ili?

(2) Maumbo sita yanayounga mkono shauri la Imani ya Kikristo ni yapi?

(3) Orodhesha vigezo mantiki sita na hitimisho lake vinavyoleta shauri la Imani ya Kikristo.

(4) Nukuu kutoka kichwani 1 Wathesalonike 2:13.

Somo la 6

Kuaminika kwa Agano Jipy

Jambo la kukumbuka kwa Kiongozi wa Darasa

Somo hili ni refu sana na limebeba taarifa nyingi sana za muhimu. Unaweza ukaligawa somo hili katika sehemu mbili kama utakavyoona inafaa.

Utangulizi

Jia alikuwa amekaa bustanini akisoma habari za kusulubiwa na kufufuka kwa Yesu. Tangu alipokuwa Mkristo, hii ilikuwa ni sehemu aliyokuwa ameipenda sana katika Agano Jipy. Alikuwa amesoma mara nyingi kitabu cha Injili ya Yohana kiasi kwamba angeweza hata kunukuu taarifa ya ufufuo kwa kichwa.

Lee alipokuwa akipita karibu, aliona alichokuwa anasoma. "Jia, kwanini unapenda kukisoma kitabu hicho mara nyingi hivyo? Siyo kizuri hata kuzidi hadithi zetu za kale za Kichina!"

Jia alipinga, "Hiki ni zaidi ya hadithi za Kale; Hili ni Neno la Mungu! Maelezo katika kitabu hiki yameandikwa na watu ambao walitembea na Yesu kwa miaka. Kitabu hiki kinanielezea jinsi ilivyokuwa kumsikia Yesu akifundisha na kuona miujiza yake. Ninakipenda kitabu hiki!"

Lee alicheka, "Nina hakika kinafurahisha, lakini Injili ziliandikwa muda mrefu baada ya Yesu kufa. Wakati Agano Jipy lilipokuwa linaandikwa, taarifa nyingi za maisha ya Yesu zilikuwa zimeshabadilika. Hatuwezi kukitegemea kitabu hicho kwa historia. Ni kitabu cha dini, siyo kitabu cha historia! Unaweza kuwa na 'imani' katika kitabu hicho ukiamua, lakini huwezi ukajua kama ni kweli."

"Ninakukatalia!" Lee alijibu. "Ninaiweka hatima yangu kwenye kitabu hiki kwa sababu ninajua ni cha kweli. Je, ninaweza kukuonyesha mambo kadhaa ambayo nimejifunza ili kuunga mkono kuaminika kwa kitabu hiki? Ndiyo, nina imani, lakini imani yangu iko kwenye chimbuko la msingi wa ukweli wa historia."

► Wewe utamjibuje Lee? Je, tunaweza tukaamini maelezo yaliyoko kwenye Biblia? Tutajuaje kwamba maelezo haya ni ya kweli?

Tarehe ya Agano Jipy

Baadhi ya watu wanasema, "Haijalishi unaamini nini ili mradi uko mwaminifu katika imani yako." Katika somo la 2. Tuliliona tatizo la tamko hili. Hata kama unaamini kabisa kwamba bilauri ya sumu ni maji, bado utakufa kutokana na ile sumu. Haitoshi tu kuamini; imani yako ni lazima ishikamanishwe na ukweli.

Katika somo la 5, tulijifunza hoja kinzani za ujumla kuhusu Ukristo. Ulijifunza jinsi ya kujenga shauri kwa ajili ya Ukristo, umbo kwa umbo, au kauli kwa kauli. Sasa tunapaswa

tuonyeshe kwamba kauli zote na za kweli. Kama ni za kweli, hitimisho litakuwa kweli. Lakini tunapaswa tuonyeshe kwamba ni za kweli, kuanzia na kauli ya kwanza au umbo lililojengwa.

► Ni kitu gani kitatokea katika shauri letu la Ukristo endapo atatokea mtu mmoja athibishe kwamba Agano Jipy AAIKUWA ya kuaminika kihistoria?

Kama Agano Jipy siyo la kuaminika kihistoria, basi sisi ni wafuasi wa dini ya uongo. Je, Agano Jipy linaaminika kihistoria? Katika somo hili, tutajifunza vipingamizi vitatu vya kawaida katika kuaminika kwa Agano Jipy na kisha tutajibu vipingamizi hivyo.

Kipingamizi cha 1: Agano Jipy liliandikwa miaka 100-200 baada ya maisha ya Kristo. Maelezo mengi ya Agano Jipy ni hadithi za kubuniwa.

Wakosoaji wanasema kwamba Agano Jipy liliandikwa miaka 100-200 baada ya kifo cha Yesu. Kwa miongo kadhaa, maelezo ya maisha ya Yesu yaliwasilishwa kwa njia ya mdomo kuliko njia ya kuandika. Hii inamaanisha kwamba maelezo yatakuwa yameshabadilika. Wakosoaji wanaofanya pingamizi hili wanasema kwamba maelezo mengi yaliyoongezwa katika vitabu vya injili ni hadithi za kubuniwa zilizoandaliwa katika kipindi hiki cha miaka 100-200.

Majibu ya kipingamizi cha 1: Agano Jipy lilikuwa limekamilika ndani ya kipindi cha miaka sitini cha cha kuhesabika maisha ya Yesu. Huo haukuwa muda wa kutosha wa kwa maelezo kuhusiana na Yesu yaweze kuvurugwa na kuwa hadithi za kubuniwa.

Kuna ushahidi wenye nguvu sana kwamba Agano Jipy iliandikwa na watu walioshuhudia kwa macho maisha ya Yesu. Wakati Injili zilipokuwa zinaandikwa, kulikuwa na watu wengi sana waliokuwa bado wanaishi amba walishuhudia mambo ya Yesu yaliyoelezwa. Watu hawa wangeweza kujua kama maelezo hayo hayakuwa ya kweli.

Tuna ushahidi mzuri kwamba Agano Jipy ilikamilika ndani ya kipindi cha miaka sitini baada ya kifo cha Yesu. Kwa uhakika, vitabu vingi vya Agano Jipy viliandikwa ndani ya miaka thelathini baada ya kifo cha Kristo. Hapa kuna vigezo vinne vya ushahidi kuunga mkono majibu yetu ya kipingamizi cha 1.

Ushahidi:

1. Maandishi (Manuscripts) yamekuwa yakipatikana kuanzia mwanzo wa karne ya pili. Mafunjo (papyrus) ya John Ryland⁴⁶ ni sehemu ya maandiko ya injili ya Yohana iliyopatikana Misri. sehemu hii ya Yohana ilionekana kuandikwa mwaka 125 B.K. Ili kipande hiki cha karatasi za mafunjo cha John Ryland kiweze kufika Misri na kunukuliwa mwaka 125 B.K. Maandishi ya asili lazima yawe yaliandikwa mapema zaidi kuliko hapo.
2. Mababa wa Kanisa la kwanza⁴⁷ kama Clementi na Ignatusi walikuwa wanankuu vitabu vya Agano Jipyä hadi mwaka 100 B.K. Hii inaonyesha kwamba vitabu hivi vilikuwa vimeshasambaa kipindi hicho.
3. Sehemu kubwa ya uandishi wa Agano Jipyä utakuwa umefanywa kabla ya Yerusalemu kubomolewa na jeshi la Kirumi mwaka 70 B.K. kwa sababu hakuna kumbukumbu za kurejewa kwa tukio hili la kihistoria katika Agano Jipyä, kama ambalo lilishafanyika. Ubomoaji wa mji wa Yerusalemu ulikuwa na athari kubwa sana kwa kanisa la Kikristo. Kuandika Agano Jipyä **baada** ya mwaka 70 B.K. bila ya kutaja ubomoaji wa mji wa Yerusalemu itakuwa ni sawa na kuandika historia kuhusu Uingereza ya karne ya ishirini bila ya kutaja Vita Kuu ya II ya dunia.
4. Matendo ya Mitume na nyaraka zote za Paulo ziliandikwa mara tu baada ya kifo cha Paulo katikati ya miaka ya 60.⁴⁸ Matendo ya Mitume 1:1-2 kinaonyesha kwamba Injili ya Luka iliandikwa kabla ya kuandikwa kwa kitabu cha Matendo ya Mitume. Kitabu cha Luka kwa hali hiyo kiliandikwa kabla ya katikati ya miaka ya 60.



Hitimisho: Mambo yote yaliyoko kwenye Agano Jipyä yaliandikwa na mashuhuda walioona mambo hayo kwa macho yao wenyewe ndani ya miongo michache sana ya maisha ya Yesu.

Mwaka	Tukio
c. 33 B.K.	Kupaa kwa Yesu
c. 65 B.K.	Kifo cha Paulo
70 B.K.	Kubomolewa kwa Yerusalemu
100 B.K.	Clementi na Ignatusi
125 B.K.	Mafunjo ya Yohana Ryland

⁴⁶ Image: "P52 recto", John Rylands Library, retrieved from https://commons.wikimedia.org/wiki/File:P52_recto.jpg, public domain.

⁴⁷ Neno “baba wa kanisa” linarejea maaskofu walioongoza Kanisa la Kikristo karne ya kwanza baada ya Krsto.

⁴⁸ Mfalme Nero wa dola la Kirumi alikufa mwaka 68 A.D. Kwa mujibu wa mwanahistoria wa kanisa la kwanza Eusebiu, Paulo alihukumiwa kifo wakati wa utawala wa Nero.

Kuaminika kwa Agano Jipy: Kipimo cha Bibliografia

Tumeshona muda wa makadirio ya muda ambao Agano Jipy iliandikwa, lakini, je, tunajua ni kitu gani ambacho awali kilikuwa kimeandikwa humo? Wakosoaji wanahoji kwamba vitabu vilivyoko katika Agano Jipy ni tofauti na vile vya awali vya injili. Kama hatuwezi kupata vile vilivyoandikwa awali, basi hatuwezi kuiamini Agano Jipy.

Vipimo vikubwa vitatu vinatumika kupima kuaminika kwa nyaraka za zamani. Vipimo hivi vitatu vinatumika kwenye kipande chochote cha maandiko ya awali. Vipimo hivi vinatusaidia sisi kuthibitisha kuaminika kwa historia ya nakala tunazosoma. Kipimo cha kwanza kinajulikana kama *Bibliografia* (*vitabu vya rejea*).

Kipimo cha Bibliografia kinapima ni kwa kiwango gani nyaraka ilikuwa imehifadhiwa vizuri. Kutokana na kipimo cha Bibliografia, tunajua aidha kama tunayo au hatunayo nakala ambayo ni nakala halisi ya awali.

Kuna vipengele vitatu vya kipimo cha Bibliografia:

1. *Urefu wa Muda*. Kipimo hiki hupima muda wa miaka kati ya maandiko ya asili na nakala zake za kale zilizosalia. Muda ukiwa ni wa kitambo kifupi, ndio jinsi tutakavyoendelea kuziamini nakala zetu za awali.
2. *Idadi*. Kipimo hiki hupima idadi iliyopo ya nakala zilizoandikwa kwa mkono. Kwa jinsi kunavyopatikana wingi wa idadi ya nakala zilizosalia, kunatuletea kuwa na uhakika zaidi wa nakala za awali.
3. *Ubora*. Kipimo hiki kinapima ni kwa jinsi gani maandishi yaliyobakia yanafanana kwa ubora. Hiki kinapima tofauti iliyopo kati ya nakala za maandishi ya mkono tulizo nazo kwa sasa. Jinsi tofauti ndogo ya ubora inavyoonekana kati ya nakala zilizopo, tunakuwa na uhakika zaidi wa nakala za awali.

Vipimo hivi hujibu vipingamizi vya wakosoaji wakidai kwamba hatuwezi kuamini nakala zetu za Agano Jipy. Tuangalie kipingamizi cha pili cha wakosoaji .

Kipingamizi cha 2: Hatuwezi kuamini nakala zetu za Agano Jipy kwa sababu kuna muda mrefu sana kati ya Maandiko ya awali na nakala za mwanzo zilizosalia.

Kipingamizi hiki kinalenga kwenye ukweli kwamba kunapotokea kuwepo na muda mrefu kati ya maandishi ya asili na nakala zilizopo, kunakuwepo na uwezekano mkubwa wa makosa. Lakini kipingamizi hiki kwa makosa kinadai kwamba kulikuwa na muda mwingi sana kati ya Agano Jipy na nakala za mwanzo; na kwamba, kwa hali hiyo, hatuwezi kuiamini Agano Jipy letu.

Kipimo cha Bibliografia: urefu wa muda

Majibu yetu kwa hili pingamizi yanaangalia kwenye urefu wa muda kati ya uandishi wa awali wa Agano Jipy na nakala zetu za mwanzo zilizosalia.

Majibu ya kipingamizi cha 2: Urefu wa muda wa Agano Jipywa ni mfupi zaidi kuliko andiko lolote la ulimwengu wa zamani.

Urefu wa muda kati ya maandishi ya awali na nakala za mwanzo zilizosalia kuhusiana na maandiko ya utamaduni na elimu ya Wayunani wa zamani ni miaka 1,000. Kwa mfano, kuna miaka 950 kati ya maandishi ya asili ya Kumbukumbu za historia za Tacitu na nakala yetu ya *mwanzo* (cha nusu ya pili). Kwa kulinganisha, urefu wa muda wa vitabu vingi vya Agano Jipywa ni takribani miaka 150.

Mwaka	Tukio
33 B.K.	Kupaa kwa Yesu
60 B.K.	Vingi vya vitabu vya Agano Jipywa viliandikwa
125 B.K.	Mafunjo ya John Ryland (papyrus)
200 B.K.	Utoaji wa nakala nyingi za Agano Jipywa

Kalenda hii ya matukio inaonyesha kwamba sehemu kubwa ya Agano Jipywa iliandikwa ndani ya miaka thelathini baada ya kupaa Yesu. Tunazo nakala za vitabu vingi vya Agano Jipywa kuanzia takribani miaka 150 iliyopita baada ya kuandikwa kwa mara ya kwanza. Linganisha hili na maandiko mengi muhimu ya zamani ya Wayunani.

Mwandishi	Andiko	Muda kati ya uandishi wa awali na nakala ya mwanzo
Plato	<i>Tetraloji</i>	Miaka 1,300
Kaisari	<i>Vita vya Wafaransa</i>	Miaka 950
Tacitu	<i>Kumbukumbu za kihistoria (nusu ya kwanza)</i>	Miaka 750
Homer	<i>Iliadi</i>	Miaka 400
	<i>Agano Jipywa</i>	Miaka 150

Angalia urefu wa muda ulivyo mdogo kati ya nyaraka za awali za Agano Jipywa na nakala zetu za mwanzo. Hakuna hata mmoja anayesema kwamba hatuwezi kumwamini Plato au Kaisari. Kama maandiko hayo yaliweza kukaa miaka 1,000 bila kupotoshwa, kwanini sisi tudhanie kwamba Agano Jipywa limepotoshwa katika kipindi cha miaka 150 tu?

Wanahistoria wanakubali nyaraka nyingine za zamani kama zinazoaminika baada ya miaka 1,000. Lakini wakosoaji bila kufikiria, wanakataa kwamba Agano Jipywa haliaminiki, ingawaje Agano Jipywa limepita bila dosari katika viwango vyote vya vipimo vya kuaminika vizuri zaidi kuliko nyaraka nyingine za zamani.

Kipingamizi cha 3: Hata kama kuna muda mfupi kati ya yale maandiko ya asili na zile nakala za mwanzo, kuna tofauti nyingi sana mionganoni mwa maandiko yaliyosalia ya Agano Jipyä kwa sisi kuweza kujua ni nini kilichokuwemo kwenye maandishi ya asili. Tunazo nakala nyingi sana za maandiko yanayohitilafiana.

Huu ni upinzani wa kawaida kuhusiana na kuaminika kwa Agano Jipyä. Kulingana na upinzani huu, Wamormoni wanasema kwamba tunataka Kitabu cha Mormoni; Waislamu wanasema kwamba tunataka Kurani.

► Je, utamjibuje mwamini wa Mormoni anayesema kwamba tunataka kitabu cha Mormoni kwa sababu Agano Jipyä haliaminiki?

Majibu ya kipingamizi cha 3: Kiwango kikubwa cha idadi ya maandiko ya Agano Jipyä yaliyopo na idadi ndogo ya migongano yake inaonyesha kwamba tunaweza kuliamini Agano Jipyä. Vipengele vya idadi na ubora wa vipimo vya Bibliografia vitaonyesha hili.

Vipimo vya Bibliografia: Idadi

Kipengele cha *idadi* kinashughulikia idadi ya maandiko ya awali iliyopo kwa ajili ya ulinganifu. Jinsi tutakavyokuwa tuna maandiko mengi, ndivyo tunapokuwa karibu na kusogelea kwenye kusoma maandishi ya asilia. Mfano huu unaonyesha thamani ya kuwa na maandiko mengi.

X					
X	X				
X	X	X			
X	X	X	X		
X	X	X	X	X	

Fikiria kwamba **X** hapo juu ndiyo nakala asilia, x zingine ni nakala za baadaye. Ingawaje kuna tofauti ndogo sana kwenye x za baadaye, lakini ni wazi kwamba kila nakala ni "x". Hutaangalia katika mstari wa nne (nakala ya mwisho) halafu usome kundi la "o."

Hii inaonyesha umuhimu wa idadi ya nakala. Kwa kuwa hatunazo tena ile maandishi asilia ya Agano Jipyä, tunategemea kwenye nakala ili kugundua ni nini cha asilia kilichokuwa kimeandikwa. Njia bora zaidi ya kujenga upya kitu cha asilia ni kulinganisha nakala nyingi za maandiko kadiri inavyowezekana. Endapo nakala nyingi zitafanyiwa uchambuzi, tunaweza kupima aina ya kifungu cha asili.

Tunazo nakala ngapi za mwanzo za Agano Jipyä? Wasomi wamekuta kuna kiasi cha miswada na vipande vya maandiko 25,000. Hii ni pamoja na maandiko ya Kiyunani 5,800, zaidi ya maandiko ya Kilatini 10,000, na maelfu mengine ya maandiko katika lugha nyinginezo.

Zaidi ya hapo, kuna maelfu ya nukuu katika maandiko ya mababa wa kanisa. Kwa hizi peke yake, mtu anaweza kuziunganisha na ikapatikana Agano Jipyä iliyokamilika.

Linganisha hii na idadi ya maandiko ya kumbukumbu za kihistoria za Kiyunani na maandiko ya Kirumi. Baada ya Agano Jipyä, kipande cha maandiko ya zamani chenye idadi ya nakala nyingi zinazopatikana ni *Iliadi* za Homer. Ukilinganisha na nakala 25,000 za Agano Jipyä, tunazo kiasi cha nakala 1,800 za *Iliadi*. Ushahidi wa maandiko kwa ajili ya Agano Jipyä ni wa kiwango cha juu kabisa ukilinganisha na ushahidi wa maandiko ya kumbukumbu za historia za Kiyunani na Kirumi. Kwa mara nyingine tena, ushahidi unaonyesha kwamba tunaweza tukaamini kuwa Agano Jipyä linaaminika.

"Mkristo anaweza kuichukua Biblia yote mikononi mwake na kusma bika hofu au mashaka kwamba anachoshikilia ndani yake ni Neno la Mungu la kweli, lilioshuka bila upotevu wowote muhimukutoka kizazi hadi kizazi kwa karne zote."

- Sir Frederick Kenyon,
Mkurugenzi wa Makumbusho ya Uingereza

Kipimo cha Bibliografia: Ubora


Kipengele cha *ubora* kinapima tofauti zilizopo kati ya maandiko iliyopo ya andiko la awali. Kuelewa hili, angalia kielelezo hiki hapa chini.

X				
O	Y			
G	7	॥		
Q	A	Z	0	
U	E	F	I	P

Kielelezo cha 1

Kama ilivyokuwa hapo juu, fikiria kwamba **X** iliyoko kileleni ndio andiko la awali asilia. Herufi nyingine zote ni nakala. Kwa mfano huu, tofauti zilizopo ni kubwa sana! Sasa "x" inakuwa "e" au "p". Kiwango cha ubora wa nakala hizi ni hafifu.

Sasa linganisha kielelezo cha 1 na hiki cha 2 hapa chini:



Kielelezo cha 2

Hapa, nakala za baadaye zinaonyesha tofauti kidogo sana. Ni wazi kwamba kila mojawapo katika hizi ni "x". Ubora wa hizi nakala ni wa juu.

Kielelezo cha 2 ni picha nzuri ya tofauti katika nakala zetu za Agano Jipy. Kutokana na upimaji wa maelfu ya nakala za awali, inaonekana kuwa kuna chini ya asilimia 1% ya Agano Jipy ambayo imeathiriwa sana kutokana na tofauti za usomaji (inakaribia maneno 400 kati ya maneno 138,000 ya Agano Jipy).⁴⁹ Hii asilimia 1% haihusiki na mabadiliko yenyе maana kuu, pia katika tofauti hizi, hakuna zinazoleta hitilafu yeyote kwenye mafundisho ya msingi ya imani au maamrisho yeyote ya maadili ya Agano Jipy. Fundisho lolote muhimu la imani linalofundishwa kutoka katika andiko ambalo maandishi yake hayaeleweki linafundishwa kutoka katika sehemu nyingine za Biblia.

Kama tutalinganisha hili na maandiko mengine ya awali ya Kirumi au Kiyunani, tunaona kwamba Agano Jipy ni la kuaminika sana. Maandiko ya *Iliadi* ya Homer ndiyo peke yake yanayoweza hata kukaribia kuwa karibu kwa ubora ikilinganishwa na nakala za Agano Jipy. Ushahidi huu unathibitisha kwamba tunayo maandiko ya awali ya asili yaliyoandikwa na waandishi wa Biblia.

Kuaminika kwa Agano Jipy: Kipimo cha Ushahidi wa Ndani

Baadhi ya wakosoaji watakichukulia maanani kipimo cha Bibliografia na watasema, "Hayo ni sawa. Tunayo yale ambayo waandishi wa Agano Jipy waliandika. Lakini tutajuaje kwamba walikuwa sahihi? Inawezekana walitunga hadithi za kusimulia."

Kipingamizi cha 4: Hatuwezi kuwaamini waandishi wa Agano Jipy kuweka kumbukumbu sahihi za matukio ambayo yalitokea. Siyo mashuhuda wa kuaminiwa.

Kujibu kipingamizi hiki, tutaangalia kwenye *ushahidi wa ndani* na *ushahidi wa nje* wa kuaminika kwa Biblia. Kipimo cha ushahidi wa ndani kinaangalia kwenye uandishi wenywewe.

⁴⁹ Kuna idadi kubwa ya nakala zinazotofautiana mionganoni mwa nakala nyingi, lakini nyingi ya hizi zina makosa ya utamkaji wa herufi mionganoni mwa nakala nyingi jambo ambalo haliwezi kuharbu maana ya nakala. .

Kinachanganua ni nini kilichoandikwa kupima kama tunaweza kumwamini mwandishi. Ushahidi wa kipimo cha ndani unahoji, "Je, tunaweza kuamini haya yaliyoandikwa na waandishi? Je, walikuwa wakweli na wenye ustadi?" Kipimo cha ushahidi wa nje kinaangalia taarifa za nje ambazo zinaunga mkono ukweli wa Agano Jipya.

Majibu ya kipingamizi cha 4: Kipimo cha ushahidi wa ndani na kipimo cha ushahidi wa nje kinaonyesha kwamba Agano Jipya ni kumbukumbu ya historia inayoaminika.

Ushahidi wa Ndani: Ushuhuda wa kuona kwa macho

► Soma 2 Petro 1:16; 1 Yohana 1:1, na Luka 1:1-4. Aya hizi zinatueleza nini kuhusiana na ushuhuda wa waandishi?

Injili zilikuwa zimetegemezwa kwenye kumbukumbu za watu ambaa walikuwa kwenye ukaribu mkubwa na Yesu. Walitoa taarifa ya kile walichokiona kwa macho yao na kusikia wenyewe.

Kumbukumbu zao zinaweza kuaminika kwa sababu kuu mbili:

1. Muda waliokaa na Yesu ulikuwa jambo muhimu sana ambalo liliwahi kutendeka kwao. Kwa kuwa muda wa wanafunzi wa kukaa na Yesu ulikuwa ni wa muhimu sana kwao, walikuwa katika uhakika wa kukumbuka mambo yote kwa undani vizuri zaidi.

► Je, unaweza kukumbuka ulikokuwa siku ya Jumanne asubuhi miezi sita kabla ya kuanza kujifunza somo hili? Yawezekana hapana. Lakini, je, unaweza kukumbuka siku uliposalimisha maisha yako kwa Kristo na kufanyika mwana wa Mungu? Hakika! Tunakumbuka mambo yote ya matukio muhimu kuliko maisha ya kila siku.
2. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba Roho Mtakatifu angewakumbusha yote aliyokuwa amewaambia (Yohana 14:25-26).

Ushahidi wa Ndani: Uwepo wa Mashuhuda walio Hai

Kipindi cha wakati wa uandishi wa Injili, kulikuwa na mashuhuda wengi waliokuwa bado wanaishi. Watu hawa walikuwa wamemwona Yesu na hivyo wangejua kama Injili imechanganya na taarifa za uongo.

Baadhi ya mashuhuda hawa walikuwa watu ambaa hawajaamini. Hawa wakosoaji wangeweza kuwafedhesha wanafunzi. Kama waandishi wangefanya makosa, wakosoaji hawa ni lazima wangeonyesha makosa yao. Kwa mfano, kama mwili wa Yesu bado ungekuwa ungaliko kaburini, ilikuwa ni jambo jepesi kwa viongozi wa Mafarisayo kudai, "Huu hapa mwili wake!"

Vitabu vya injili vinamwelezea Yesu akilisha zaidi ya watu 5,000 wanaume, pamoja na wanawake na watoto. Kama taarifa hii ingekuwa ni ya uongo, mtu angeweza akasema, "Nilikuwepo siku hiyo. Haikuwahi kutokea namna hiyo. Sisi wote tulikuja na vyakula vyetu vya mchana!"

Ushahidi wa Ndani: Waandishi waliifia Imani yao

Mitume walikufa kwa sababu hawangeweza kuikana imani yao ya Kikristo. Baadhi yao waliteswa; wote kwa pamoja walipitia mateso ya upinzani; wengi wao walikufa kama mashahidi wafia imani. Mara nyingine watu hufa kwa ajili ya kile wanachoamini kwamba ni cha kweli, lakini siyo kwa kitu wanachokijua kwamba ni cha uongo.

Kama kupaa kwa Yesu mbinguni hakukutokea, Mitume wangejua hayo yote. Mitume amba walikuwa wamejificha kwa ajili ya hofu baada ya Yesu kukamatwa hawangeweza kukubali kufia kitu ambacho wangejua ni cha uongo. Utayari wao wa kuyatoa maisha yao kwa ajili ya imani kunathibitisha kuamini kwao.

Waandishi wa vitabu vya Injili walikuwa waaminifu sana na wenye ustadi mkubwa. Huu ni ushahidi wa ndani kwamba tunayo Agano Jipya inayoaminika.

"Vipi kuhusu kuhitilafiana ndani ya Biblia?"

Wakati Randall McElwain alipokuwa akifundisha katika seminari moja Afrika, alimfundisha mwanafunzi mmoja aliyejikuwa amejifunza kutoka kwa wakosoaji huria amba walikataa ukweli wa Biblia. Ukosoaji huu ulimshawishi huyu kijana mdogo mwanafunzi kwamba Biblia ilikuwa na kuhitilafiana kwingi. Takribani kila siku, Toni atamwambia Randall, "Nimegundua kuhitilafiana katika Biblia. Je, unaweza kuelezea...?"

Mwanzoni, Randall alikuwa na hofu kwamba Toni angepata huko tatizo ambalo hangekuwa na jibu zuri la kumjibu. Hata hivyo, kwa kitambo walichochukua kujifunza, kulimpa Randall nafasi zaidi ya kutambua kwamba "kuhitilafiana" kwake alikokuona ni matokeo ya kutoielewa Biblia vizuri. Ulipofika mwisho wa darasa, Toni alikiri kwamba, "Biblia inaaminika zaidi kuliko nilivyokuwa ninafikiria."

Ili kujibu kinachodhaninwa kuwa ni kuhitilafiana, unapaswa uelewe sheria ya kutokuhitilafiana. Sheria hiyo inasema kwamba, "**Taarifa haiwezi kuwa ya kweli na wakati huo huo kuwa siyo ya kweli kwa wakati mmoja katika kitu kinachofanana.**" Kwa hiyo, kama taarifa moja kabisa inahitilafiana na taarifa nyingine, moja wapo katika taarifa hizo itakuwa siyo ya kweli.

Ili taarifa moja iweze kabisa kuhitilafiana na nyingine, ni lazima kusiwepo na maana moja ya kufanana ili kila taarifa zote ziwe za kweli. Kama kuna maelezo yanayowezekana ya kimantiki, hiyo siyo kuhitilafiana halisi. Mifano aliyokuja nayo Toni ilikuwa ni kuhitilafiana kunakoonekana na siyo kuhitilafiana halisi.

Tuone mifano ya kuhitilafiana kunakoonekana na kuhitilafiana halisi:

Kuhitilafiana Kunakoonekana:

Jeni anasema, "Niliona gari ya samawati iliyopata ajali nikiwa njiani kuja shulen asubuhi ya leo."

Robert anasema, "Niliona gari nyekundu iliyopata ajali nikiwa njiani kuja shulen i asubuhi ya leo."

Mtu anaweza akasema, "Taarifa hizo zinajichanganya zenyewe!" Lakini hii peke yake ni kuhitilafiana kunakoonekana. Inawezekana Jane na Robert waliona ajali mbili tofauti. Inawezekana magari yote mawili kwa pamoja yalipatwa na ajali; Jane aliona gari la samawati, na Robert aliona gari nyekundu, Taarifa zote mbili zinaweza kuwa ni za kweli. Hii siyo kuhitilafiana halisi.

Kuhitilafiana Halisi:

Jeni anasema, "Nikiwa naelekea shulen i leo asubuhi, niliona gari la samawati likigonga ng'ombe."

Robert anasema, "Niliona ajali hiyo hiyo. Kulikuwa na gari moja tu na mnyama mmoja; lakini gari hiyo ilikuwa nyekundu, siyo samawati; na iligonga farasi siyo ng'ombe."

Hii ni kuhitilafiana halisi. Taarifa zote mbili haziwezi kuwa za kweli. Angalao mojawapo ya hizi taarifa siyo sahihi.

Kinachodhaniwa kuwa ni kuhitilafiana katika Vitabu vya Injili

Tuangalie mfano mmoja kutoka katika vitabu vya Injili. Mathayo anataja malaika mmoja kwenye kaburi la Yesu; Luka anasema walikuwa wawili

► Je, hii ni kuhitilafiana kunakoonekana au ni kuhitilafiana halisi? Fafanua jibu lako.

Je, hii ni kuhitilafiana kabisa? Hapana. Mathayo hasemi "malaika mmoja" kwenye kaburi; ye ye anamtaja tu mmoja. Inawezekana kabisa kuwa Mathayo alimtaja malaika mmoja tu. Wakati Luka (mwana-historia aliyependa sana maelezo ya kina) alitaja malaika wote wawili kwa pamoja ambao walikuwa pale.⁵⁰

Baada ya miaka 2000 ya kujifunza, hakuna mkosoaji aliweza kuthibitisha kuhitilafiana kabisa ndani ya Biblia. Hakika, kwa jinsi tunavyozidi kuendelea kujifunza sayansi, historia na Biblia, ndiyo kwa kiwango kikubwa matatizo yanayodhaniwa ndani ya Biblia yanavyozidi kutatuliwa. Orodha ya mambo yaliyoko katika kuhitilafiana kunakoonekana inazidi kuwa fupi sana.

Kuaminika kwa Agano Jipyä: Kipimo cha Ushahidi wa Nje

Kipimo cha Ushahidi wa Ndani kinaangalia kwenye uandishi peke yake kupima kama mwandishi alikuwa mwaminifu na mwenye ustadi. Kipimo cha Ushahidi wa Nje kinaangalia

⁵⁰ Kwa mfano mwingine, rudi kwenye somo la 1 na soma mazungumzo ya Jia na Lee kuhusiana na muda wa Yesu wa kusulubiwa. Huu ni mfano mwingine wa hitilafu isiyokuwa halisi, na wala siyo halisi.

taarifa za nje zinazounga mkono nyaraka. Kwenye suala la Agano Jipya, kipimo hiki kinauliza, "Kuna ushahidi gani uliopo *nje ya Maandiko* unaohusu ukweli wa Agano Jipya?"

Ushahidi unaounga mkono kutoka kwa Waandishi wengine wa Kikristo wa Mwanzo

Viongozi wa Kikristo wa mwanzo waliitegemeza imani yao kwenye ukweli wa Injili. Kama ilivyokuwa kwa mitume wenyewe, Wakristo hawa wa mwanzo waliweka maisha yao rehani kwa ajili ya imani yao.

Papia alikuwa rafiki wa mtume Yohana. Aliandika kwamba Yohana alishuhudia kuwa Ijnili ya Marko ilitegemezwa na kumbukumbu za Simeoi Petro za maisha ya Yesu na huduma. Huu ni ushuhuda wa nje kwamba Injili ya Marko inanukuu mtu aliyeona kwa macho yake mwenyewe kuhusiana na huduma ya Yesu.

Irenaeu alizaliwa karibia mwaka wa 125 B.K. pungufu ya miaka arobaini baada ya Yohana kuandika Injili yake. Irenaeu aliandika:

Uthabiti imara ndio msingi mkuu ambao hizi Injili zimekaa, kwamba hata wakosoaji mahiri wenyewe wamekuwa mashahidi kwao wenyewe, na kuanzia na nyaraka hizi, kila mmoja wao anajitahidi kuanzisha imani yake mwenyewe.

Kwa mujibu wa Irenaeu, hata wapinzani katika kanisa la mwanzo waliheshimu kumbukumbu za Injili. Vitabu vya Injili vilikuwa vinazingatiwa kwa kiwango cha juu sana kama nyaraka zinazoaminika.

Ushahidi Unaounga Mkono kutoka Vianzo vya wasiokuwa Wakristo

Hivi tungejua nini kuhusu Yesu na Ukristo wa mwanzo kama hatungekuwa na Biblia? Ushahidi wa nje unatizama sana vianzo vya wasiokuwa Wakristo ambavyo vinathibitisha kumbukumbu za Agano Jipya.

Marejeo ya kihistoria kutoka kwa watu wasiokuwa Wakristo kunathibitisha kwa kiwango kikubwa Agano Jipya. Hii ni pamoja na:

- Barua kutoka kwa Pliny Mdogo, gavana wa Bithynia kwenda kwa Mfalme Trajani mwaka wa 112 B.K.
- Maandiko ya Josephus, mwana-historia wa Kiyahudi.
- Tacitu, seneta wa Kirumi na mwana-historia.
- Luciani, mwandishi wa Kiyunani wa karne ya pili.
- Suetonia, mwana-historia wa Kirumi
- Talmud, kitabu cha maoni na maelezo ya Kiyahudi kuhusiana na sheria ya Musa.

Vianzo hivi vya wasiokuwa Wakristo vinaunga mkono vigezo vingi vianvyohusiana na muktadha wa Agano Jipya:

- Yesu alisulubishwa chini ya utwala wa Pointio Pilato wakati wa Pasaka (Tacitu, Josephus, Talmud).
- Wanafunzi wake waliamini kwamba alifufuka kutoka kwa wafu siku tatu baadaye (Josephus).
- Viongozi wa Kiyahudi walimshutumu Yesu kwa kufanya uchawi (Talmud).⁵¹
- Ukristo ulienea hadi Rumi (Tacitu, Suetonia).
- Nero na watawala wengine wa Kirumi waliwatesa na kuwauwa Wakristo wa mwanzo (Tacitu).
- Wakristo waliikana imani ya kuabudu miungu wengi wakaishi kwa mujibu wa mafundisho ya Kristo, na wakamwabudu Kristo (Pliny, Luciani).


Tunawajua wote hawa kutokana na historia ya ulimwengu na ya Kiyahudi. Hii inaleta udhihirisho wa nje kwamba Agano Jipya ni sahihi kihistoria.

Ushahidi wa uungwaji mkono kutoka elimu ya vitu vya kale (Akiolojia).

Akiolojia (*au elimukale*) ni kigezo kikubwa muhimu kwa chanzo cha ushahidi wa nje. Tangu karne ya kumi na tisa, wana-akiolojia wameweza kutafuta maeneo mengi yaliyotajwa kwenye Agano Jipya. Mara zote, waliyojifunza yanaendana sawasawa na kumbukumbu za Agano Jipya.

Elimu ya Kuitetea Imani katika Vitendo – Ushuhuda wa Sir William Ramsay

Sir William Ramsay (1851-1939) alikuwa ni mmoja wa wana-akiolojia aliyejkuwa anaheshimika sana mwanzoni mwa karne ya ishirini.⁵² Alisoma chini ya wanazuoni maarufu sana wa wakati ule katika Aberdeen na Oxford. Kwa kuwa wakufunzi wake hawakuwa wanakubaliana na ukweli wa Biblia, Ramsay alidhania kwamba Biblia haikuwa na umuhimu wowote kama nyaraka ya kihistoria.



Baadaye, Ramsay alisafiri hadi Ugiriki na Asia Ndogo kujifunza kuhusu ulimwengu wa kale. Mwanzoni, hata hakutaka kusoma Biblia inasemaje kuhusu nchi hiyo, kwa sababu alidhania haiaminiki. Hata hivyo, hatimaye alianza kuyasoma maandiko ya Luka, akawa ameshangazwa na usahihi wa maandiko ya Luka.

Kwa maisha yake yote yaliyosalia, alijifunza kitabu cha Matendo na barua za Paulo. Alipoanza mafunzo yake, miji mingi iliyokuwa imetajwa katika Kitabu cha Matendo ilikuwa haijulikani. Hata hivyo, Ramsay alishawishika kwamba Kitabu cha Matendo ni kumbukumbu

⁵¹ Hata maadui wa Yesu walitambua kwamba alikuwa anafanya miujiza. (waliuita uchawi).

⁵² Image: "Portrait of Sir William Ramsay", retrieved from the Wellcome Collection, <https://wellcomecollection.org/works/fwfdpnry>, licensed under CC BY 4.0, desaturated from the original.

inayoaminika inayohusiana na ulimwengu wa kale. Sir William Ramsey hatimaye aliandika vitabu juu ya historia na jiografia ya Asia Ndogo, safari za Paulo, na masomo mengine mengi. Mwana-akiolojia huyu mahiri sana alijifunza kwamba Agano Jipyä ni ya kuaminika

Uthibitisho wa 1: Kuaminika kwa Maandiko ya Luka.

Sir William Ramsay alitumia maandiko ya Luka kujifuza jiografia ya Asia Ndogo. Aligundua kwamba ufahamu wa Luka ulikuwa hauna kifani katika historia na jiogarfia. Kwa mfano, Luka anataja kuhusu nchi thelathini na mbili, miji hamsini na nne, na visiwa tisa. Katika kila alichojifunza Ramsay, aligundua kwamba muktadha wa Luka ulikuwa sahihi.

Uthibitisho wa 2: Kugunduliwa kwa Sakafu ya Mawe

Yohana 19:13 kinarejea kiti cha hukumu ambacho Pilato alikalia wakati akimhukumu Yesu.

Basi Pilato, aliposikia maneno hayo, akamleta Yesu nje, akaketi juu ya kiti cha hukumu, mahali paitwapo Sakafu ya Mawe.

Kwa miaka mingi, wakosoaji wenyewe msimamo wa kupenda mabadiliko, waliyaita maelezo haya kwamba ni hadithi ya kusimuliwa ya kutungwa. Hata hivyo, wana-akiolojia wamepata hapa panapoitwa Sakafu ya Mawe, na panaweza kuonekana kwa wageni wanaoitembelea Yerusalem. Wakati jenerali wa kijeshi Tito wa Kirumi alipoibomoa Yerusalem alijenga kambi ya jeshi kwenye eneo hilo la Sakafu ya Mawe. Wakati makambi haya yalipobomoka, majengo mengine yalijengwa juu yake. Sakafu ya mawe ikatoweka. Wana-akiolojia wa mwanzo walichimba sana hadi eneo la chini la hiyo sakafu ya mawe lakini hawakuendelea zaidi ya hapo. Kwenye miaka ya 1970 wana-akiolojia waliendelea kuchimbua eneo hilo la kambi ya jeshi kwa kina na wakagundua palipokuwa panaitwa Sakafu ya mawe. Hili eneo katika Agano Jipyä lilithibitika kwamba lipo.

Uthibitisho wa 3: Birika la Bethzatha

Kitabu cha Yohana 5 kinaelezea kuhusu Birika la Bethzatha, likiwa na matao matano. Pia, kwa sababu hakuna kumbukumbu kutoka katika vianzo vya Kiyahudi au vya ulimwengu, wakosoaji waliita hii ni hadithi ya kusimuliwa ya kutungwa. Mnamo Mwaka 1888, wana-akiolojia walilipata hilo birika baada ya kuwa wamechimba futi arobaini kwenda chini ya ardhi karibu na kanisa la Mtakatifu Ainea. Birika lilikuwa na matao matano, kama Yohana alivyokuwa ameelezea.

Agano Jipyä inaaminika kihistoria. Hatuhitaji kuwa na hofu kwamba wana-akiolojia wataacha kuithibitisha Biblia. Kwa jinsi wana-akiolojia walivyoendelea kuchimbua, walipata ushahidi unaoongezeka kuunga mkono ukweli wa Biblia.

Hitimisho

Jia alimwonyesha Lee kila kipimo kinachutumika kwa ajili ya kuhalalisha Agano Jipyä. Msichana Jia alimwonyesha kijana Lee kwamba *kipimo cha Bibliogarafia* kinathibitisha kwamba Agano Jipyä tuliyo nayo leo inafundisha imani ileile iliyokuwa ikifundishwa kutoka

katika maandiko asilia ya awali. Alimwonyesha kwamba *Vipimo vya Ushahidi vya Ndani na Nje* vinathibitisha kuaminika kwa Agano Jipy.

“Lee,” Jia akahitimisha, “Unaweza ukachagua kuamini madai ya Agano Jipy au ukachagua kuyakataa. Hata hivyo, huwezi kukanusha kwamba Agano Jipy ni nyaraka ya kuaminika kihistoria. Bado kuna ushahidi wa zaidi wa ukweli wa Agano Jipy kuliko nyaraka nyingine zozote kutoka katika ulimwengu wa kale, iwe magharibi au China. Agano Jipy ni nyaraka ya kihistoria ya kuaminika kabisa.”

Kazi za kufanya Somo la 6

(1) Elimu ya kuitetea imani na Kichwa: Utaanza kipindi kinachofuata kwa mtihani kutokana na maswali ya tafakuri yaliyoko katika Somo la 6. Jifunze maswali haya kwa uangalifu kwa maandalizi ya mtihani

(2) Elimu ya kuitetea imani na Moyo: Kuaminika kwa Biblia ni zaidi ya utafiti wa kitaaluma. Tunafurahia kwamba tunaweza kuliamini Neno la Mungu kutufunulia mapenzi ya Mungu kwetu. Katika 2 Timotheo 3:16, Paulo anatuambia kwamba Neno la Mungu “lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki.” Sasa kwa kuwa umejifunza kuaminika kwa Neno la Mungu, mwombe Mungu azungumze na wewe kupitia Neno lake. Kwa wiki ijayo, mruhusu Mungu akuonyeshe:

- Mafundisho, kuuelewa vizuri ukweli
- Kuwaonya watu makosa yao, kukuongoze katika tembea yako ya Ukristo
- Masahihisho, Kumfanania zaidi Kristo
- Kujifunza kuishi kwa usahihi

(3) Elimu ya kuitetea imani na Mikono: Mwishoni mwa Somo la 5, ulimwuliza asiyeamini akuruhusu umshirikishe kuhusu maumbo yanayounga mkono imani ya Kikristo. Zungumza na huyu mtu tena na mshirikishe taarifa uliyoiopata kutoka katika somo hili. Kama walishasikia tetesi kuhusu hitilafu katika Biblia, watake wakuonyeshe hizo hitilafu. Waonyeshe mfano mmoja wa hitilafu ya wazi ambayo imetatuliwa. Toa taarifa kuhusu mazungumzo yenu katika kipindi cha darasa kitakachofuata.

Mtihani wa Somo la 6

- (1) Jibu pingamizi lifuatalo: "Agano Jipyä liliandikwa miaka 100-200 baada ya maisha ya Kristo. Maelezo mengi ya Agano Jipyä ni hadithi za kubuniwa." Toa angalao vigezo vitatu vya ushahidi kuunga mkono majibu yako.
- (2) Kipimo cha Bibliografia kinajaribu kuonyesha nini kinapotumika kwenye nyaraka yeyote ya zamani?
- (3) Orodhesha vipengele vitatu vya Kipimo cha Bibliografia vinavyodhihirisha kuaminika kwa Agano Jipyä.
- (4) Watu wengine husema, "Hatuwezi kuamini nakala zetu za Agano Jipyä kwa sababu kuna muda mrefu sana kati ya Maandiko ya awali na nakala za mwanzo zilizosalia." Ni kwa jinsi gani kipengele cha *Urefu wa muda* Kipimo cha Bibliografia kinaweza kujibu hiki kipingamizi?
- (5) Toa majibu kwa kipingamizi kifuatacho: "Hata kama kuna muda mfupi kati ya yale maandiko ya asili na zile nakala za mwanzo, kuna tofauti nyingi sana mionganoni mwa maandiko yaliyosalia ya Agano Jipyä kwa sisi kuweza kujua ni nini kilichokuwemo kwenye maandishi ya asili. Tunazo nakala nyingi sana za maandiko yanayohitilafiana."
- (6) Jibu pingamizi lifuatalo: "Hatuwezi kuwaamini waandishi wa Agano Jipyä kuweka kumbukumbu sahihi za matukio ambayo yalitokea. Siyo mashuhuda wa kuaminiwa."
- (7) Orodhesha sababu tatu za Agano Jipyä kufaulu katika "Kipimo cha Ushahidi wa Ndani."
- (8) Sheria ya Kutokuhitilafiana ni nini?
- (9) Je, yuko mtu yeyote anayeweza kudhihirisha ukiukwaji halali wa Sheria ya Kutokuhitilafiana katika Maandiko?
- (10) Orodhesha mistari mitatu ya ushahidi itakayoweza kusaidia Agano Jipyä kufaulu kipimo cha Ushahidi wa Nje.
- (11) Taja ugunduzi mbili za akiolojia zinazounga mkono usahihi wa historia ya Agano Jipyä.
- (12) Nukuu kutoka kichwani 2 Timotheo 3:16-17.

Somo la 7

Unabii wa Masihi na Ufufuo

Jambo la kukumbuka

MUHIMU SANA: Mtihani kwa ajili ya somo hili utakuwa kwa njia ya mjadala utakaofanyika katika kikao chako cha darasa kinachofuata. Kabla ya kuanza somo, soma maelekezo ya kazi za kufanya kipengele cha "Elimu ya kuitetea imani Kichwa" mwishoni mwa somo hili. Tafakuri zilizoko katika somo hili zitasaidia wanafunzi kujiandaa kwa ajili ya mjadala.

Utangulizi

Jia alikuwa na msisimko. Mungu alikuwa amemsaidia kumwonesha Lee kwamba Agano Jipy ilikuwa linaaminika. Kwa hakika, punde tu ataikubali Injili. Hii ni zaidi ya chemsha bongo ya kimaadili; Jia alikuwa anaomba aweze kupata nafasi ya kumshirikisha Injili rafiki yake. Wakati Lee alipomkaribia Jia kwenye mgahawa wa chai, alicheka na kusema, "Umeshafikiria juu ya mazungumzo ya wiki iliopita?"

Lee alicheka, "Ninaweza kuona umemaanisha kabisa kuhusu kitabu chako! Umeweza kunishawishi mimi kwamba Wakristo wa mwanzo waliamini kwa uhakika kabisa kwamba Yesu alikuwa Masihi, na kwamba alifanya miujiza aliyonukuliwa kwenye vitabu vya Injili. Ninashawishika kwamba Agano Jipy ni kumbukumbu sahihi ya kile ambacho kanisa la kwanza liliamini. Hata hivyo, bado kuna tatizo. Hata kama kiukweli Wakristo wa kwanza waliamini kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu, leo tunajua kwamba ufufuko ni jambo lisilowezekana!"

"Ndio, Wakristo wa mwanzo *waliamini* katika Ufufuo, lakini hilo halifanyi kuwa ni la kweli. Kumbuka, watu katika ulimwengu wa kale waliamini katika hadithi nyingi za kusimuliwa. Waliamini kwamba ulimwengu ni bapa; waliamini katika mizimu; waliamini katika ufufuo. Lakini tunaishi katika kizazi cha sayansi Jia. Unajua kwamba ulimwengu ni duara! Unajua kwamba mizimu haipo! Unawezaje ukaamini kwa kumaanisha kwamba mtu aliyekufa anaweza kutoka kaburini?"

► Ni kwa jinsi gani unaweza kumjibu Lee? Je, upo ushahidi wa kihistoria unaotosholeza kwa ajili ya ufufuo wa Yesu Kristo?

Katika somo hili, tutaangalia vipengele viwili vya ushahidi kuonesha kwamba Yesu aliyejithibitisha mwenyewe. Kwanza, tuaangalia unabii wa Masihi. Tutaonesha kwamba Yesu alitimiza kikamilifu yote yaliyotabiriwa kwake miaka mamia kabla ya kuzaliwa kwake. Pili, tutaupima ushahidi unaohusu ufufuo. Tutaona kwamba Ufufuo ni zaidi ya hadithi nzuri; ni tukio la kihistoria.

Je, Yesu alitimiza unabii wa Masihi?

► Tafadhali toa majibu kwa seti hizi mbili za maswali...

Seti ya kwanza:

- Je, hali ya hewa itakuwaje kesho katika mji wako?
- Ni nani atakuwa raisi atakayefuata baada ya sasa katika nchi yako?
- Katika miaka ishirini ijayo, uchumi wa nchi yako utakuwa mzuri zaidi au mbaya?
- Maswali haya ni magumu kwa kiwango gani?
- Je, unadhani kwamba utabiri zilizotolewa angalao ni sahihi?

Seti ya Pili:

- Nani atakuwa raisi wa nchi yako ifikapo mwaka 2130?
- Atazaliwa mahali gani?
- Atakufaje?
- Maswali haya ni magumu kwa kiwango gani?
- Kuna tofauti gani kati ya maswali haya na seti ya kwanza hapo juu?

Ni rahisi kidogo kutabiri baadhi ya mambo katika siku zijazo. Kulingana na hali ya hewa ya leo, ninaweza kuhisi vizuri hali ya hewa ya kesho itakavyokuwa. Kulingana na taarifa za habari, ninaweza hata kutabiri kuhusu raisi ajaye.

Ni vigumu zaidi kutabiri kitu cha miaka mia moja ijayo. Siwezi nikajua ni nani atakuwa anaishi ifikapo 2130; kwa hiyo siwezi nikatabiri jina la raisi, mahali pa kuzaliwa, au aina ya kifo.

Unabii katika Biblia kuhusiana na Masihi unahusika na kundi la pili. Manabii walitabiri matukio kadhaa mamia ya miaka mingi kabla ya kutokea, na tabiri hizi zilikuja kutokea vile vile kama zilivyokuwa zimetabiriwa.

Kuna karibia utabiri sitini maalumu za kinabii katika maisha ya Yesu. Katika somo hili, tutaangalia nabii kumi na mbili miongoni mwa hizi. Marabi wa Kiyahudi walioishi *kabla ya kuzaliwa kwa Yesu* walizichukulia hizi kama za Masihi

► Ligawe darasa katika makundi mawili. Kwa kila unabii mruhusu mtu mmoja kutoka kundi la 1 asome unabii. Kisha mruhusu mtu mwininge kutoka kundi la 2 asome kutimia.

UNABII ULIOTIMIA KATIKA MAISHA YA YESU	
UNABII	KUTIMIA
Kabila la Yuda – Mwanzo 49:10	Luka 3:23, 33
Nyumba ya Daudi – Yeremia 23:5	Luka 3:23, 31
Amezaliwa Bethlehemu - Mika 5:2	Mathayo 2:1
Kutambulishwa na mjumbe – Isaya 40:3	Mathayo 3:1-3
Kufundisha na huduma ya uponyaji – Isaya 61:1, 2; 32:3-4; 35:5	Mathayo 9:24; Luka 4:17-21
Kuishi kabla ya hekalu na Yerusalemu kubomolewa – Danieli 9:26	Hekalu na Yerusalemu vilibomolewa mwaka wa 70 B.K.
Aliitwa Bwana na Mungu – Yeremia 23:6; Isaya 8:6	Luka 2:11; Yohana 29:28
Aliingia Yerusalemu kwa punda – Zekaria 9:9	Mathayo 21:1-8
Kukaa kimya mbela ya washtaki wake – Isaya 53:7	Mathayo 27:12
Kuumizwa kwa maumivu – Isaya 53:5	Mathayo 27:26
Mwili ulichomwa mkuki katika kusulubiwa – Zekaria 12:10	Yohana 19:34
Alizikwa pamoja na matajiri – Isaya 53:9	Mathayo 27:57-60

Je, itawezekana kwamba haya yote yaliyotabiriwa yalitimia kwa kubahatisha?

Haiwezekani. Tumeorodhesha unabii kumi na mbili mionganii mwa dazani za unabii ziizotimizwa na Yesu. Ukadiriaji wa kihafidhina wa kujua uwezekano wa hizi unabii kumi na mbili kuwa zilitimia kwa kubahatisha ni 1 katika 100,000,000,000,000,000 (1 × 10¹⁷).

Fikiria kuifunika Ufaransa yote na vipande vya sarafu ya fedha kwa kina cha futi mbili. Katika hizo sarafu moja iwekee alama nyekundu ya "X". Kisha mfunge mtu machoni na umwambie akaiokote hiyo sarafu. Uwezekano wa kubahatisha kuiokota sarafu yenye alama nyekundu "X" ni 1 × 10¹⁷. Haiwezekani!

Je, itawezekana kwamba Yesu kwa matakwa yake alitimiza haya yaliyotabiriwa?

Haiwezekani. Yesu angeweza kuchagua kuwa mwalimu, au kuchagua kuwa kimya mbele ya washtaki wake; lakini hangeweza kuchagua familia yake, mahali pa kuzaliwa, au jinsi Warumi watakavyoutoboa mwili wake baada ya kusulubiwa.

Je, itawezekana kwamba Mungu ndiye aliyetoa unabii wote?

Hakika. Kama unabii wote haungetimia au kama Yesu angetimiza kwa kuchagua yeye, utabiri huu lazima ungekuwa umetoka kwa Mtu mwingine mwenye uwezo wa kuangalia mambo ya mbele.⁵³ Kwa kuwa ni Mungu tu mwenye kujuu mambo yajayo, utabiri wa mambo haya ni lazima uwe umetokana na Mungu. Yeyote atakayetekeleza tabiri hizi atakuwa aliyechaguliwa na Mungu.

Kufufuka kwa Yesu Kristo

Kufufuka kwa Yesu aidha ni mzaha mkubwa sana au ni muujiza mkuu mno wa utukufu wa nyakati zote. Ukristo unasimama au unaanguka kwenye jibu la swali lifuatalo, "Je, Yesu alifufuka kimwili kutoka kwa wafu?" Paulo alisema kwamba, kama Kristo hakufufuka, imani yetu ni bure na sisi ni watu wanyonge sana. Kwa nini? Kwasababu kama Kristo hakufufuka, hatuna matumaini ya uzima wa milele⁵⁴.

Ili kujibu hili swali, "Je, Yesu alifufuka kimwili kutoka kwa wafu?" tutatizama mambo matatu:

1. Je, Yesu alikufa? Baadhi ya watu wanakataa kabisa kwamba Yesu hakika hakufa msalabani.
2. Kwa nini kaburi lilikuwa wazi? Baadhi ya watu wanadai kwamba Yesu hakufufuka kutoka kwa wafu. Wanasema kuna maelezo mengine yanayohusu kaburi kuwa wazi.
3. Kulitokea nini baada ya Kufufuka? Je, kunao ushahidi wa Kufufuka katika matukio yaliyotokea baada ya asubuhi ya Jumapili ya kwanza ya Pasaka asubuhi?

Kutokana na majibu ya maswali haya, tutaona kwamba kuna ushahidi wa kutosha kuamini kwamba Yesu alifufuka kimwili kutoka kwa wafu. Hii ni zaidi ya hadithi; ni ukweli wa historia.

Je, Yesu alikufa?

Tunapojadili suala la Kufufuka, tunalazimika kwanza tuoneshe kwamba Yesu alikufa. Baadhi ya wapinzani wa Ukristo, kama vile Waislamu, wanakataa kwamba Yesu kwa hakika hakufa. Kuna ushahidi gani wa kifo chake?

Kupoteza damu kabla ya kusulubishwa

Kabla Yesu hajasulubishwa, alipigwa fimbo sana na askari wa Kirumi. Upigaji fimbo wa Kirumi ulikuwa wa kikatili na mara nyingi walioangukia kuwa wahanga wa ukatili huu hufa. Tabibu mmoja wa wanadamu aliandika:

⁵³ Baadhi ya wakosoaji husema kwamba hizi unabii ziliandikwa baada ya matukio waliyoyaeleza. Hata hivyo, ni rahisi kudhihirisha kwamba hizi unabii zilitolewa miaka 200 kabla ya Kristo. Kitabu cha *Septuagint* (tafsiri ya Agano la Kale kutoka Kiyunani kwenda Kiebrania) kiliandikwa miaka 200 kabla ya Kristo. Kwa kuwa unabii za Agano la Kale zilitafsiriwa kutoka Kiebrania kwenda Kiyunani kwenye mwaka 200 K.K. zitakuwa ziliandikwa mapema kabla ya wakati huu.

⁵⁴ 1 Wakorintho 15:14-22

Kuchapa kwa kiboko kwa Warumi kwa kawaida kulihitajika mijeledi thelathini na tisa.... Askari atatumia fimbo iliyosukwa kwa nyazi za ngozi ikiwa na vimipira vya chuma vilivyoshonewa ndani yake. Wakati fimbo itakapochapwa kwenye nyama ya mwili, hivi vimipira vitasababisha majeraha ya ndani sana, ambayo yatakuwa yanapasuka kutokana na mwendelezo wa kipigo. Fimbo hiyo pia huwekwa vipande vidogo vidogo vya mifupa, vitakavyoweza kuichanachana nyama ya mwili sana.

Sehemu ya mgongoni itakuwa imepigwa sana kiasi kwamba mara nyingine sehemu ya uti wa mgongo ilikuwa inaweza kuonekana kutokana na kukatwa kwa kina sana. Kipigo kilifanywa katika maeneo yote ya mwili kuanzia mabegani hadi mgongoni, kwenye makalio, na nyuma ya miguu.⁵⁵

Hata kabla ya kusulubiwa, Yesu alikuwa kwenye kipindi kigumu cha maumivu makali na kupoteza damu nyingi kulikosababisha azimie. Ilibidi wamtafute mtu mwingine wa kuubeba msalaba wake, Yesu alikuwa katika hali ya umahututi hata kabla ya kuangikwa msalabani.

Ushahidi kutoka kwenye msalaba

Juu ya msalaba, mtu anaweza tu kupumua kwa kuvuta juu kwa mikono yao na kusukuma juu kwa miguu yao. Baada ya mtu kuwa juu ya msalaba kwa muda mrefu wa kutosha kumfanya mtu kuanza kukosa nguvu, askari wa Kirumi wataivunja miguu yake ili aliyesulubiwa asiweze kuvuta miguu yake juu tena, Hatua hii humfanya aliyeangikwa kushindwa kupumua.

Viongozi wa Kiyahudi hawakutaka kuuacha mwili wa Yesu juu ya msalaba wakati wa kuanza kwa sikukuu ya Pasaka. Kwa sababu ya hiyo, askari walisogelea ili kuivunja miguu ya Yesu na ya wale wezi wawili. Hata hivyo, hawakuivunja miguu ya Yesu kwa sababu alikuwa tayari alishakufa. Askari wa Kirumi amba walikuwa wamepewa jukumu la kusulubisha walijua vyema jinsi ya kutambua kama aliyeangikwa ameshakufa. Walijua tayari Yesu alikuwa ameshakufa.⁵⁶

Njia moja ambayo askari wa Kirumi alitumia kuthibitisha kwamba aliyeangikwa msalabani alikuwa kweli ameshakufa ilikuwa ni kumpiga mkuki uingie ubavuni mwake. Damu na maji ikitoka nje ilikuwa ni ishara ya kuwa mtu alishakufa. Kama mtu atakuwa bado yu hai, damu peke yake itatoka. Wakati askari alipompiga Yesu mkuki wa ubavuni, "mara hiyohiyo ikatoka damu na maji."⁵⁷ Hii ikamthibitishia askari kwamba Yesu alishakufa.

Akida aliweza kumthibitishia Pilato kwamba Yesu alishakufa. Mwili wa Yesu ulifungwa kwa kuvungirishwa ndani ya sanda na baadaye ukalazwa kaburini. Hakuna aliyekuwa na shaka kwamba Yesu alikuwa amekufa.

⁵⁵ Imenukuliwa kutoka Lee Strobel, *The Case for Christ* (MI: Zondervan, 1998), 195

⁵⁶ Yohana 19:31-33

⁵⁷ Yohana 19:34

Kwa nini Kaburi Lilikuwa Wazi?

Wanahistoria wa Kiyahudi na Kirumi wote wanakiri kwamba Yesu aliuawa kwa njia ya kusulubiwa. Swali jingine linahusika na kaburi kukutwa liko wazi . Mitume walihubiri kwamba Yesu alitoka na mwili wake wote alipofufuka kutoka kaburini. Walifundisha ufufuo wa mwili. Walijua kwamba kaburi lilikuwa wazi.

Vitabu vya Injili vinathibisha kwamba kaburi lilikuwa wazi. Mlinzi wa Kirumi hakuweza kukanusha kwamba kaburi lilikuwa wazi; Viongozi wa Kiyahudi hawakuweza kukanusha kwamba kaburi lilikuwa wazi. Fikiria kama Mitume waliitengeneza hii taarifa ya Kufufuka. Ingekuwa rahisi sana kwa viongozi wa Kirumi na Kiyahudi kuutoa huo mwili – na huo ndio ungekuwa mwisho wa Ukristo. Badala yake, taarifa za kaburi kukutwa liko wazi lilihamasisha watu wengi kuamini katika Kristo.

Wasioamini wamejaribu kutoa maelezo mengine kuhusiana na kaburi kuwa wazi. Wanasema kwamba:

Wanafunzi waliuiba mwili wa Yesu.

Mara tu kaburi lilipokutwa liko wazi, viongozi wa Kiyahudi walipendekeza kwamba mitume wameiba mwili wa Yesu.⁵⁸ Katika karne ya pili, mwandishi wa Kiyahudi, Trypho, alisema,

Yesu, Mgalilaya mdanganyifu, tuliyemsulubisha, lakini wanafunzi wake wamemwiba usiku na sasa wanadanganya watu wakidai kwamba amefufuka kutoka kwa wafu na amepaa kwenda mbinguni.⁵⁹

► Je, haya ni maelezo mazuri? Kwa nini au Kwa nini siyo?

Kuna vipengele viwili vya ushahidi vilivyo kinyume na nadharia hii.

Kwanza – Ili kuweza kuuiba ule mwili, mitume ilibidi wawazidi nguvu walinzi wenye mafunzo wa Kirumi, wavingirishe lile jiwe zito, na watoroke na ule mwili. Wanafunzi hawa hawa walikimbia kwa hofu wakati Yesu alipokamatwa. Ni jambo lisiloaminika na la kushangaza kwamba sasa wamekuwa na ujasiri wa kukabiliana na walinzi wa Kirumi.

Walinzi wa Kirumi wangekabiliwa na adhabu ya kifo kama wangeshindwa na majukumu yao ya ulinzi. Walikuwa na kila sababu ya kuwa waangalifu. Hakuna sababu ya kuamini kwamba walizidiwa nguvu na mitume wasiokuwa na nguvu, au kwamba walilala usingizi wakati wakiwa katika lindo.

Pili – Kama mitume waliuiba mwili, *walijua maelezo ya kufufuka yalikuwa ya uongo*. Katika maneno ya Josh McDowell, “Nani anaweza kufu kwa ajili ya uongo?” Ndiyo, watu walishakufa *wakiamini* kwamba uongo ndio uliokuwa ukweli, lakini watu wachache watakuwa *wakijua* kwamba wanakufa kwa ajili ya uongo.

⁵⁸ Mathayo 28:11-15

⁵⁹ Nukuu kutoka Justin Martyr, *Dialogue with Trypho*

Ili kuamini kwamba mitume waliiba mwili kunatuhitaji sisi tuamini kwamba watu kumi na moja waliweka maisha yao rehani kwa hoja ambayo walijua siyo ya kweli. Hawakupata utajiri au nguvu katika hoja hii; waliwindwa na kuuawa kwa sababu ya hoja hii. Fikiria jinsi hawa mitume walivyokufa:

- Petro alisulubiwa.
- Andrea alisulubiwa.
- Mathayo alikatwa kichwa.
- Yakobo, mwana wa Alfayo alisulubiwa.
- Filipo alisulubiwa.
- Simeoni alisulubiwa.
- Tomaso aliuawa kwa kupigwa mikuki.
- Bartholomayo alisulubiwa.
- Yakobo, mwana wa Zebedayo, aliuawa kwa upanga.

Watu hawa waliyatoa maisha yao kwa imani kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu. Hawakufa kwa ajili ya uongo.

Mamlaka za Kirumi na Kiyahudi ziliuondoa ule mwili.

Baadhi ya wakosoaji wanapendekeza kwamba Warumi au Wayahudi waliuondoa mwili. Wanasema kwamba Warumi au Wayahudi waliuficha ule mwili ili Wakristo wasiweze kuupata.

► Je, haya ni maelezo mazuri? Kwa nini au Kwa nini siyo?

Jibu halina mantiki kabisa. Wayahudi walitaka kuisambaratisha hii dini mpya; Warumi walitaka kuweka amani kati ya Wayahudi na Wakristo ndani ya Yerusalemu.

Wakati dini ya Kikristo ilipoanza kusambaa, Warumi au Wayahudi wangeweza wakauonyesha mwili kama ulikuwa umefichwa, kuthibitisha kwamba Yesu bado ni marehemu. Walikuwa na kila kigezo cha kuweza kuthibitisha kwamba Yesu hakuwahi kufufuka kutoka kwa wafu. Hakuna sababu yeyote ya wao kuuficha mwili.

Yesu hakufa; alikuwa amezirai wakati alipozikwa.

“Nadharia ya kuzirai” ndiyo inayoshamiri miongoni mwa Waislamu wengi leo. Wanasema kwamba Yesu hakuwahi kufa pale msalabani. Badala yake, alizimia kwa sababu ya maumivu na kupoteza damu. Askari walidhania kwamba alikuwa ameshakufa, kwa hiyo wakamzika. Mle kaburini, Yesu alizinduka kutoka katika kuzimia na akatoka nje ya kaburi. Wafuasi wake waliamini kwamba amefufuka kutoka kwa wafu.

► Je, haya ni maelezo mazuri? Kwa nini au Kwa nini siyo?

Ili nadharia hii iweze kuwa ya kweli, fikiria yote ambayo ni lazima yatokee:

- Yesu ingebidi aendelee kuishi baada ya kile kipigo cha kutisha na upotevu wa damu pale msalabani.

- Ilikuwa aweze kuwapumbaza wale askari waliokuwa wamepewa mafunzo ya kuua na kuthibitisha kifo.
- Baada ya kuzinduka kutoka kule “kuzirai” kwake, huyu mtu aliyejewa mdhaifu angepaswa avingirishe lile jiwe zito kutoka pale kaburini.
- Angepaswa awazidi nguvu wale walinzi wa Kirumi, waliokuwa wamepewa jukumu la kulilinda kaburi.
- Katika hali hii ya udhaifu, angejitokeza akiwa na nguvu sana ili wafuasi wake waweze kushawishika kwamba alikuwa Bwana wa Maisha na Mshindi juu ya Kifo.

Haya hayawiani na chochote tulichokisoma kuhusu kusulubiwa na kufufuka. Njia nyingine inayoweza kuleta mantiki katika haya mambo yote ni kwamba Yesu alifufuka kama alivyosema.

Nini kilitokea baada ya Kufufuka?

Ushahidi wa kufufuka hauishii tu pale kaburini. Yesu aliwatokea mamia ya watu wiki kadhaa baada ya kufufuka. Kufufuka kulibadilisha maisha yao – na kuendelea kubadilisha hadi leo.

Ushahidi wa kuonekana kwa Yesu baada ya Kufufuka

Moja ya orodha kamili sana ya kuonekana kwa Yesu baada ya kufufuka ni **orodha ya Paulo** katika 1 Wakorintho 15:3-8. Paulo aliiandika orodha hii mnamo mwaka 55 B.K., miaka ishirini hadi ishirini na tano baada ya Ufufuo. Orodha hii ya mashahidi ni pamoja na Petro, wanafunzi kumi na mbili, na Yakobo.

Paulo anataja kundi la watu zaidi ya 500 waliomwona Yesu aliyefufuka. Wengi wa watu hawa walikuwa bado wanaishi. Kama hesabu ya Paulo ilikuwa ya makosa, wangeweza kulidhihirisha kosa lake. Paulo alijua kwamba watu hawangeweza kutoa changamoto kwa neno lake.

Vitabu vyote vya **Injili** vinne vimebeba ushuhuda wa watu waliomwona Kristo baada ya Kufufuka. Wakristo hawa wa kwanza walihatarisha maisha yao kwa ajili ya ushuhuda wao. Wengi walikufa kwa ajili ya kile walichokiamini. Kama Ufufuo haungetokea, wangelijua. Hawangekubali kufa kitu wanachokijua kwamba kilikuwa uongo

Kipengele mojawapo muhimu sana cha kukumbukwa cha kuonekana kwa Yesu baada ya kufufuka ni kile cha **wanawake kama mashahidi wa kwanza**. Mariamu Magdalene, Yoana, Mariamu mamaye na Yakobo na Salome walikuwa kati ya watu wa kwanza kufika kaburini.⁶⁰ Kwa leo, hili linaweza lisioneokane kama ni muhimu, lakini katika ulimwengu wa kale, hiki ni kigezo kikubwa sana cha kuunga mkono ukweli wa vitabu vya Injili.

Kwenye karne ya kwanza, ushahidi wa mwanamke ulikuwa haukuliki mahakamni. Kwa sababu ya sheria zao za hadhi ya chini ya kijamii , wanawake walikuwa hawana haki ya

⁶⁰ Mathayo 28:1-10; Marko 16:1-11; Luka 24:1; Yohana 20:11-18

kisheria kusimama. Hata mitume mwanzoni kabisa walikuwa wameukataa ushuhuda wa hawa wanawake.⁶¹

Kama waandishi wa vitabu vya Injili wangekuwa wanatunga taarifa hii, hawangewahusisha wanawake kama mashuhuda wa kaburi kuwa wazi. Mwadishi anayebuni angeweza akatumia mashahidi wenyе hadhi na kuheshimika kama vile viongozi wa dini wanaoheshimiwa ili kushuhudia kuhusu Kufufuka. Badala yake, waandishi wa vitabu vya Injili waliandika taarifa sahihi kama zilivyotokea.

Katika utafiti wa kihistoria, tunatoa umuhimu mkubwa katika kuamini ushahidi wa walioona kwa macho yao. Hali hiyo pia inatakiwa iwe kweli wakati tunapoifunza ukweli wa historia ya Kufufuka. Hawa walikuwa mashuhuda wa kwanza. Ushahidi wao unapaswa upate kipaumbele cha kuchukuliwa kama ushahidi wa thamani katika ukweli wa Kufufuka

Ushahidi wa maisha yaliyobadilishwa

Ushahidi mwingine wa Kufufuka ni mguso wake kwa watu wengine. Watu wengi katika karne ya kwanza walishawishika na ukweli wa Ufufuo. Maisha yao yalibadilishwa na Kristo aliyefufuka. Majina ya watu wachache itaonyesha udhihirisho wa hatua hii:

Paulo, aliyeetuwa adui mkubwa wa Ukristo kisha akajageuka kuwa mtetezi wake mkubwa. Alisafiri eneo lote la utawala wa Kirumi akidhihirisha ukweli wa Ufufuo.

Yakobo, Ndugu yake mdogo na Yesu, alikuwa mkosoaji mkubwa wakati wa maisha ya Yesu hapa duniani. Hata hivyo, alipomwona Yesu akiwa hai tena baada ya Kufufuka kulimshawishi Yakobo kuhusu madai ya Yesu kwamba yeye ndiye Masihi. Yakobo alikuja kuwa kiongozi mkuu wa Kanisa la Yerusalem.

Mguso endelevu ndani ya Kanisa

Ili kusheherekeea Kufufuka kila wiki, Wakristo wa mwanzo waliivusha **siku yao ya kuabudu** kutoka Jumamosi hadi Jumapili. Kwa kuwa kufufuka kulitokea siku ya kwanza ya wiki, waliabudu katika siku ya kwanza ya wiki. Wakristo wa kwanza waliisherehekea Pasaka ii kuadhimisha ufufuko katika hali ya uhalisia wa mwili wa Yesu.

⁶¹ Luka 24:11

Sanaa kuanzia karne ya kwanza inaonyesha imani ya Wakristo kwamba "Yesu ni Mungu." Sarafu ya fedha iliyoko hapa kulia ina mchanganyiko wa alama ambazo zilikuwa maarufu sana katika Kanisa la mwanzo.⁶²

Kwanza, ina alama mbili zinazoingiliana kutoka katika alfabeti za Kiyunani: **x** (*chi*) na **p** (*rho*), alama mbili za mwanzo ni za neno la Kiyunani *Christòs*" au "Kristo." Kisha, inaongeza **a** (*alpha*) na **ω** (*omega*) herufi ya kwanza na ya mwisho katika alfabeti ya Kiyunani, ikionyesha kwamba Yesu ndiye mwanzo na mwisho wa mambo yote.



Kuta za makaburi zinaonyesha muhtasari mwingine wa mwanzo wa imani za Kikristo, katika umbo la samaki. Jina lingine kwa ajili ya samaki lilikuwa *ἰχθύς* (*ichthus*).⁶³ Kila herufi ilikumbushia Wakristo wa mwanzo baadhi ya vipengele vya imani kuhusu Yesu wa Nazareti. Alama ya samaki ilikuja kufanyika ni kanuni nyepesi ya imani kwa Wakristo wa mwanzo: Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, Mkombozi wetu.

- i = *Iesous* (Yesu)
- x = *Christos* (Kristo)
- θ = *Theou* (Ya Mungu)
- ύ = *Uios* (Mwana)
- ς = *Soter* (Mkombozi)



Unaweza ukaona ni kwa hali ya juu kiasi gani Wakristo wa mwanzo walimheshimu Yesu. Walimwabudu Kristo kama Mungu anayeishi. Maelezo mazuri zaidi kwa ajili ya kuabudu kwao kulichangiwa sana na kufufuka na mwili kwa Yesu, waliyemwamini ameshinda kifo kama Bwana wa Maisha.

Je, Unabii uliotimia na Kufufuka kunathibitisha nini?

Utabiri kuhusu masihi ambazo zilitimilika katika maisha ya Yesu zinadhihirisha kwamba alikuwa ni Masihi aliyetabiriwa. Muda mrefu kabla ya kuzaliwa Yesu, marabi wa Kiyahudi walikubaliana kwamba unabii wote unaelekezwa kwa Masihi. Ukweli kwamba unabii wote wa undani kuhusiana na Masihi ulitimia miaka mamia kadhaa baada ya kutabiriwa kunadhihirisha kwamba Mungu aliuvuvia unabii wote, kwamba Mungu aliongoza kuzaliwa kwa Yesu, na kwamba Mungu alimtuma Yesu kama Masihi Myahudi!

► Kwa nini Kufufuka ni muhimu sana katika imani ya Kikristo?

Kufufuka ni msingi mkuu wa imani ya Kikristo kwa sababu inathibitisha kwamba Yesu ni yeye yule aliyesewa kwamba ndiye – Mwana wa Mungu, Mungu katika mwili. Mungu peke yake anayo nguvu ya kufufua wafu, na Mungu hawezি akamfufua mwongo. Baadaye

⁶² Image: "CE30928 Moneda", taken by Angel M. Felicísimo on Feb 7, 2016, retrieved from <https://www.flickr.com/photos/elgolem/24386520264>, licensed under CC BY 2.0, cropped and desaturated from the original.


⁶³ Image: "ICTHUS", retrieved from <https://commons.wikimedia.org/wiki/File:ICTHUS.gif>, public domain.

tutaonesha kwamba Yesu alisema ndiye Mungu. Kufufuka kunadhihirisha ukweli wa madai ya Yesu.

Kufufuka kunatoa uhalali kwa madai ya Yesu kwamba kifo chake "kitakuwa fidia kwa wengi."⁶⁴ Kufufuka kunaonesha kwamba Yesu anayo mamlaka juu ya kifo. Kwa sababu ya hiyo, Yesu anao uwezo wa kutoa maisha kwa wafuasi wake kama alivyoahidi.

Elimu ya Kuitetea Imani katika Vitendo – Ushuhuda wa Simoni Greenleaf

Simoni Greenleaf (1783-1853) alikuwa mmoja wa waasisii wa Shule ya Sheria ya Harvard. Kwa miongo mingi, *Treatise on the Law of Evidence (Tasnifu yake kuhusu Sheria ya Ushahidi)* ilionekana ni kitabu bora zaidi katika ushahidi wa kisheria.⁶⁵



Greenleaf alikuwa pia ni Myahudi aliyemkana Mungu. Aliamini kwamba kufufuka kwa Yesu Kristo ni utapeli. Wakati mwanafunzi alipompa changamoto ya kujifunza ushahidi, Profesa Greenleaf alikusudia kuthibitisha kwamba Kufufuka ni hadithi za kutunga za kusimulia. Badala yake, alikuja kukubali kwamba Kufufuka ni ukweli wa historia.

Kwa sababu alitambua nguvu ya ushahidi uliopo wa Kufufuka, Greenleaf alikuja kuwa Mkristo aliyejitoa kabisa. Maandiko yake yaliwavutia watu ambao wakati wa leo ni watetezi wakubwa wa imani – wakiwemo Josh McDonell na Lee Strobel, ambao tumejifunza habari zao katika kozi hii.

Baada ya kujifunza ushahidi wa Kufufuka, Greenleaf aliandika, "**Kama ushahidi wa kufufuka utawekwa katika chumba chochote cha mashitaka duniani kinachotenda haki bila upendeleo, itaamuliwa kwamba ni ukweli wa kihistoria – Yesu alifufuka kutoka kwa wafu!**"

Kitabu maarufu cha Greenleaf kiliitwa *The Testimony of the Evangelists: The Gospels Examined by the Rules of Evidence (Ushuhuda wa Wainjilisti: Injili Zikipimwa kwa Sheria za Ushahidi)*. Katika kitabu hiki, Greenleaf alitumia sheria za ushahidi wa kisheria ambazo zinatumika katika mahakama za kisheria. Alihitimisha kwamba mahakama yejote ya kisheria yenye kutenda haki itatambua Injili kama za ushahidi wa kisheria. Mwanazuoni huyu nguli wa sheria wa mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, alitambua kwamba uchunguzi wa ushahidi wa kihistoria unaonyesha kwamba kufufuka kwa Yesu Kristo kulikuwa Dhahiri, na siyo habari za kubuniwa.

⁶⁴ Mathayo 20:28

⁶⁵ Image: "Simon Greenleaf", retrieved from https://commons.wikimedia.org/wiki/File:Simon_Greenleaf.jpg, public domain.

Hitimisho

"Lee," Jia alijibu, "ninaelewa wasiwas wako wa kuamini katika Ufufuo. Inaonekana kama haiwezekani! Lakini unapuuzia ushahidi wa kihistoria kuhusu ukweli wa taarifa hii. Siyo kweli kwamba watu wa ulimwengu wa kale hawakutegemea watu waliokufa kurudi tena kutoka kaburini? Ndiyo, baadhi yao waliamini katika mizimu – lakini waliamini kwamba mizimu ni watu waliokufa. Hakuna aliyeamini kwa uhakika kwamba ni mtu anarudi kutoka kaburini.

"Watu wa ulimwengu wa zamani, hawangeweza kujua kuhusu sayansi ya kisasa, lakini walijua kwamba *watu waliokufa hubakia wamekufa*. Wanafunzi walishrushwa na kufufuka. Hakuna aliyetegemea kumwona Yesu akiwa hai. Waliamini tu pale walipokabiliana na wimbi la ushahidi kwamba, 'Hayuko hapa, amefufuka.'⁶⁶

"Mtume Paulo, Mwisraeli aliyeigana dhidi ya imani ya Kikristo, alikuja kuwa mwamini baada ya kukutana na Bwana mfufuka. Kumbuka, Paulo aliandka barua zake wakati ambapo mamia ya watu waliokuwa mashuhuda wa kifo chake walikuwa bado wanaishi. Kama ushuhuda wa Paulo ungekuwa wa uongo, wangelijua! Lakini Paulo aliandika bila kuwepo hofu ya kuhitilafiana:

...Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alimtokea Kefa; tena na wale Thenashara; baadaye aliwatokea ndugu zaidi ya mia tano pamoja; katika hao wengi wanaishi hata sasa, ila baadhi yao wamelala; baadaye akamtokea Yakobo; tena na mitume wote; na mwisho wa watu wote, alinitokea mimi, kama ni mtu aliyezaliwa si kwa wakati wake.⁶⁷

"Lee, Paulo alijua kwamba Yesu Kristo alifufuka kutoka kaburini. Yesu ni Mwana wa Mungu aliyejufa kwa ajili ya dhambi zetu na aliyeonesha uwezo wake juu ya nguvu za kifo kwa Kufufuka. Na sisi tunamwamini, tunaweza kushiriki katika ushindi wake ulio juu ya kifo. Tunaweza kuwa na uzima wa milele!"

"...watu wanaojiita wa kisasa hujidhania kuwa wao ni wa kwanza katika historia kugundua kwamba watu waliokufa huendelea kubakia waliokufa. Lakini mitume walijua kwamba watu waliokufa huendelea kubakia waliokufa. Masihi waliye kufa huendelea kubakia wamekufa. Kila mtu anajua hivyo. Ndiyo, wanatambua kuna ufufuo wakati wa nyakati za mwisho, lakini siyo sasa...Pasaka ilikuwa ni kitu cha kushtukiza... Huu ndio msingi wa Kanisa, wa imani ya Kikristo, wa maisha ya Kikristo, na tumaini, na upendo na kicheko na ushuhuda. Pasaka siyo kwamba ni jambo lisilowezekana tu, ni kwamba haiwezekani. *Lakini ilitokea.*"
- Nukuu kutoka Mahubiri ya Pasaka na N.T. Wright, Aprili 11, 2009

⁶⁶ Mathayo 28:6

⁶⁷ 1 Wakorintho 15:3-8

Kazi za kufanya Somo la 7

(1) Elimu ya kuitetea imani na Kichwa: Mtihani kwa ajili ya somo hili utakuwa tofauti na masomo yaliyopita. Badala ya kuandika majibu kutoka na maswali yaliyoulizwa, utawasilisha majibu kwenye mdahalo wa darasa. Kiongozi wa darasa atajifanya kwamba ye ye ni mkosoaji ambaye anakataa ukweli wa Kufufuka. Utatoa ushahidi wa Kufufuka ambaao umejifunza katika somo hili.

Kwa mfano – kama “mkosoaji” anasema kwamba Yesu kwa uhakika hakuwahi kufa juu ya msalaba, utatoa sababu ambazo tunaweza kuwa na uhakika kwamba Yesu alikuwa amekufa. Kama mkosoaji atasema kwamba maelezo ya kufufuka yalibuniwa na wanafunzi, unaweza ukajilekeza kwenye ushuhuda wa wanawake kama sababu ya kukubaliana na maelezo hayo. Unapojiandaa kwa ajili ya mdahalo huu, panga taarifa zako kutoka katika somo hili katika njia ambayo itakusaidia kujibu maswali ya wakosoaji wanayoweza kuwa nayo kuhusiana na Kufufuka.

(2) Elimu ya kuitetea imani na Moyo: Katika Warumi 1:4, Paulo anasema kwamba kufufuka kunadhihirisha kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Kisha katika Warumi 6, Paulo anaonyesha kwamba sisi “tunaokufa katika Kristo” wameunganika naye katika ufufuo wake. Hii ina maana kubwa sana katika maisha yetu ya Ukristo kila siku. Kwa sasa tumekuwa “wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu.” (Romans 6:11).

Fikiria kuhusu maisha yako ya Ukristo ya kila siku. Je, unapigana na majoribu ya mara kwa mara katika maeneo fulani fulani? Kama ndivyo, tafakari juu ya ukweli ulioko atika Warumi 6. Umekufa katika dhambi, na uko hai kwa Mungu. Kwa sababu ya ufufuo, unaweza ukaishi kila siku katika ushindi dhidi ya dhambi. Wiki hii, chukua muda wako kumshukuru Mungu kila siku kwa ushindi endelevu dhidi ya dhambi.

(3) Elimu ya kuitetea imani na Mikono: Mwishoni mwa Somo la 5, ulimwuliza asiyeamini akuruhusu umshirikishe kuhusu maumbo yanayounga mkono imani ya Kikristo. Zungumza na huyu mtu tena na mshirikishe taarifa uliyoipata kutoka katika somo hili. Waulize kama unaweza kushirikishana nao ushahidi kuhusu ukweli wa Kufufuka. Kabla ya kikao chako, omba Mungu aandae miyo yao kwa ajili ya kupokea ukweli. Toa taarifa kuhusu mazungumzo yenu katika kipindi cha darasa kitakachofuata.

Somo la 7: Mdahalo

- (1) Orodhesha unabii tatu maalumu za Masihi ambazo Yesu alizikamilisha katika maisha yake.
- (2) Kutimia kwa unabii mwingi maalumu za Masihi kunaonesha nini kuhusiana na chanzo cha unabii?
- (3) Orodhesha hoja tatu za wakosoajia wanazozitoa kuhusu kaburi kuwa wazi. Katika kila hoja, toa sababu moja tu kuonyesha kwamba hoja hiyo ina mapungufu.
- (4) Kuna nini cha muhimu kuhusiana na kumbukumbu ya wanawake waliokuwa mionganoni mwa mashahidi wa kwanza kwenye Ufufuko?
- (5) Kuna nini cha muhimu kuhusu ibada ya kuabudu ya Wakristo wa mwanzo wakiabudu katika kila siku ya kwanza ya wiki na kusherehekea Pasaka kila mwaka?
- (6) Nukuu kutoka kichwani 1 Wakorintho 15:3-6.

Somo la 8

Madai ya Yesu kuwa Yeye ni Mungu

Jambo la kukumbuka

MUHIMU SANA: kabla ya kuanza somo la 8, fanya mdahalo uliotolewa mwishoni mwa somo la 7. Kutegemea ukubwa wa darasa lako, mdahalo huu unaweza kuchukua kipindi chote. Tafadhalii usiharakishe katika zoezi hili. Huu ni wakati wako wa kujihakikisha kwamba unaweza kutumia taarifa iliyoko katika somo la 7.

Utangulizi

"Jia," Lee alisema kwa mashaka, "Nimekuwa nikifiria sana kuhusu mazungumzo yetu. Kama kweli Yesu alifufuka kutoka kwa wafu, hiyo ni vizuri sana! Ni lazima nikiri kwamba unao ushahidi mzuri wa Ufufuo kama historia ya ukweli na siyo hadithi za kutunga na kusimuliwa. Hayo yate yanavutia. Naamini sitakuwa nimekukwaza kama bado nitaendelea kukuuliza swali lingine."

"Hapana," Jia alijibu. "sio kwamba nataka kushinda hoja. Ninachojaribu ni kukushirikisha jambo muhimu katika maisha yangu. Swali lako ni nini?"

"Kila kitu ulichokisema kinaleta maana. Lakini hiyo itathibitishaje kwamba Yesu ni Mungu? Mtu maarufu sana? Hakika! Mwalimu mashuhuri? Hakika! Inawezekana mkubwa kuliko Buddha. Lakini, ni Mungu? Kwa nini usikubali tu kwamba alikuwa mwalimu mashuhuri? Kwa nini ni lazima useme kwamba Yesu alikuwa Mungu?"

► Utamjibuje Lee? Tutajuaje kwamba Yesu alikuwa Mungu?

Je, Yesu alidai kuwa Yeye ni Mungu?

Kenneth Copeland ni mwalimu maarufu sana katika harakati ya injili ya mafanikio. Kwa mujibu wa Copeland, Kristo alikuja kwake kwa njia ya maono akamwambia:

Usitaabike wakati watu wanapokushusha na kusema vibaya juu yako. Walisema hivyo kwangu. Je, hawatazungumza vivyo hivyo kuhusu wewe? Kwa kiwango kile unachoendelea kufanana na mimi, ndivyo watakavyozidi kufikiria zaidi juu yako. Walinisulubisha kwa kuwa nilisema kwamba mimi ni Mungu. Lakini sikusema kwamba mimi ni Mungu; nilisema tu kwamba nilitembea pamoja naye na kwamba alikuwa ndani yangu.⁶⁸

⁶⁸ Kenneth Copeland, quoted in Hank Hanegraaff, *Christianity in Crisis*, (Oregon: Harvest House, 1993), 137-138

Copeland anasema kwamba Yesu hakusema kwamba yeye ni Mungu. Watu wengine wengi walikubaliana na Copeland; wanasema kwamba Yesu hakuwahi kusema kwamba yeye ni Mungu. Je! hii ni kweli? Au je, Yesu alidai kuwa Mungu?

► Utamjibuje Kenneth Copeland? Je! Yesu alidai kuwa Mungu?

Kama Yesu alidai kwamba yeye ni Mungu, alikuwa ni kiongozi pekee wa dini kubwa kuliko zote duniani kutoa madai haya. Mohammedi hakuwahi kujinasibu kwamba yeye ni Mungu; Buddha hakuwahi kujinasibu kuwa Mungu. Kama Yesu alijinasibu kuwa Mungu, hii inaitenga dini ya Kikristo mbali na dini nyingine kubwa duniani. Tutayaangalia madai ya Yesu katika sehemu mbili- madai yake wakati wa huduma na madai yake wakati wa mateso yake.

Yesu alisema nini wakati wa Huduma Yake?

Yesu alisema kuwa yeye ni "MIMI NIPO" wa Agano la Kale.

Yesu alisema, "...Yeye Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO."⁶⁹ Wakati umati wa Wayahudi waliposikia maneno hayo, walijua kwamba Yesu alikuwa analenga kujifunua kwa Yehova kwenye kichaka kilichokuwa kinawaka moto. Musa aliuliza, "Niwaambie nani aliyenituma?" Mungu akajibu, "Ndivyo utakavyowaambia wana wa Israeli, 'MIMI NIKO amenituma kwenu.'"⁷⁰ Wakati Yesu aliposema, "MIMI NIKO," wasikilizaji wake walijua kwamba alikuwa anajinasibu kwamba yeye ni Yehova.

Yesu alisema yeye ni mmoja pamoja na Mungu Baba.

Yesu alisema, "Mimi na Baba tu Umoja." Wakati aliposema haya, Wayahudi walichukua mawe ya kumpiga. Kwa nini? Kwa sababu walitambua kwamba anajnasibu yeye ni Mungu. Walisema, "wewe uliye mwanadamu wajifanya mwenyewe u Mungu. "⁷¹ Hawakudiriki kumpiga mawe kwa sababu alikuwa mwalimu mwenye hadhi; hawakudiriki kumpiga mawe kwa ajili ya kazi zake njema; walijaribu kumpiga mawe kwa sababu alijifanya mwenyewe kuwa ni Mungu.

Wakati Kenneth Copeland anaposema, "Yesu hakuwahi kujinasibu kwamba yeye ni Mungu," inaonyesha kwamba Copeland haelewi mafundisho ya Yesu kama vile wasikilizaji wa Yesu wa Kiyahudi walivyokuwa wanamwelewa! Hata maadui wa Yesu walitambua kwamba alikuwa anasema kwamba ni Mungu.

Buddha alisisitiza kwamba atawaelekeza watu wake "kwanye njia." Lakni Yesu hakuwahi kusema, "Nitaonyesha njia." Badala yake Yesu alisema, "Mimi ndimi njia."⁷² Hata kama utakataa dai la Yesu la kuwa Mungu, hupaswi kukataa kwamba alisema maelezo hayo. Yesu alidai kuwa Mungu.

⁶⁹ Yohana 8:58

⁷⁰ Kutoka 3:14

⁷¹ Yohana 10:30, 33

⁷² Yohana 14:6

Yesu alisema anazo sifa za Kimungu.

► Soma kila mstari ulioko hapa na orodhesha orodha ya hizo sifa za kimungu Yesu anazodai kuwa nazo.

Mathayo 18:20 _____

Yohana 17:5, 24 _____

Yesu alijinasibu kuwa na sifa za Mungu, au tabia za Mungu. Alijinasibu kuwa anapatikana mahali pote kwa wakati mmoja; alijinasibu kuwa yeye ni wa milele. Hizi ni sifa ambazo zinahusika na Mungu wa kweli tu. Wakati Yesu alipotoa kauli hizi, wasikilizaji wake walijuwa alikuwa anadai kwamba anazo sifa ambazo zinahusika na Mungu peke yake.

Yesu alisema kuwa anao uweza wa kutenda mambo ya kiungu.

Yesu alijinasibu kuwa na **nguvu za kusamehe dhambi**. Katika Marko 2 Yesu alimwambia yule mwenye kupooza, "Mwanangu, dhambi zako zimesamehewa." Wasikilizaji wake wa Kiyahudi walilalamika, "Nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa Mungu mwenyewe?" Katika kujibu, Yesu alifanya jambo jingine la kuthibitisha kwamba alikuwa na mamlaka ya kusamehe dhambi. Alimponya mwenye kupooza.⁷³ Uponyaji ule ulikuwa ni ushuhuda wa uwezo wa kiungu wa Yesu

Yesu alijinasibu kuwa ana **uwezo wa kuwapa uzima wa milele kwa wale wote watakaomwamini yeye**. Yesu aliwaambia wasikilizaji wake kwamba alikuwa "ameshuka duniani kutoka mbinguni." Alisema, "kila amtazamaye Mwana na kumwamini yeye, awe na uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho."⁷⁴

Wakati Wayahudi walipomwuliza Yesu "awaeleze waziwazi" yeye ni nani, alisema, "Naliwaambia, lakini ninyi hamsadiki," Lakini kwa wale watakaomwamini, "nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe."⁷⁵ Ni Mungu peke yake mwenye uwezo wa kutoa uzima wa milele. Kwa kuahidi uzima wa milele, Yesu alijinasibu kuwa Mungu.

Yesu alisema nini katika Kesi yake?

Wakati wa kuendelea kwa kesi yake, alidai kuwa yeye ni Mungu. Baada ya mashahidi kutoa ushahidi wao, Kuhani Mkuu alimwuliza Yesu, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wake Mtukufu?" Yesu akasema, "Mimi ndiye, nanyi mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija na mawingu ya mbinguni."

Kuhani Mkuu alijua mara moja kwamba Yesu anadai uungu. Kuhani Mkuu "akararua nguo zake" akasema,... "Mmesikia kufuru yake."⁷⁶

⁷³ Marko 2:1-12

⁷⁴ Yohana 6:40

⁷⁵ Yohana 10:24-28

⁷⁶ Marko 14:61-64

Jibu la Yesu lilikuwa katika sehemu tatu:

- “Wewe ni Kristo?” “*Mimi ndiye.*”
- “Wewe ndiwe Mwana wake Mtukufu?” “*Mimi ndiye.*”
- “*Mtamwona Mwana wa Adamu...*”

“Wewe ni Kristo?” Yesu alidai kuwa ni Masihi.

Neno “Kristo” ni tafsiri ya neno la Kiyunani kwa “Masihi”. Kwa kujinasibu kwamba yeye ni Masihi, Yesu alijinasibu pia kuwa ni Mungu. Yeremia alitabiri siku ambayo jina la Masihi litaitwa “Bwana (Yehova) ni haki yetu.”⁷⁷ Isaya alitabiri kwamba Masihi ataitwa “Mungu mwenye nguvu.”⁷⁸ Wakati Yesu aliposhuhudia, ‘Mimi ni Kristo’ alikuwa anasemea nyadhifa hizi (“Bwana ni haki yetu” na “Mungu mwenye nguvu.”)

“Wewe ndiwe Mwana wake Mtukufu?” Yesu alidai kuwa Mwana wa Mungu.

Mara nyingi Yesu alikuwa akimtaja Mungu kama “Baba.” Je! Yesu alikuwa anajinasibu kuwa Mwana wa Mungu kwa maana ya kwamba sisi sote ni wana wa Mungu? Hapana. Yesu alijinasibu kuwa Mwana pekee wa Mungu.

Yesu alisema, “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee.”⁷⁹ Kwa Yesu kuwa Mwana wa Mungu inamaanisha kwamba ana aina ya uhusiano wa pekee na Baba. Yesu alisema pia kwamba yeye ni Mungu Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba.⁸⁰ Huu ulikuwa ni uhusiano maalumu sana wa Baba na Mwana.

Yesu alisema kwamba Yeye na Baba ni wamoja.⁸¹ Kwa kweli, Yesu alisema kwamba tunapaswa kumuenzi Mwana kama tunavyofanya kwa Baba.⁸² Wakati Yesu alipodai kuwa Mwana wa Mungu, alikuwa anamaanisha kuwa mmoja katika asili na Mungu aliye Baba. Inamaanisha kwamba yeye ni Mungu Mwana, mwenye asili moja na Baba. Hii ndiyo sababu viongozi wa Kiyahudi walikasirika kwa Yesu kuthibitisha kwamba alikuwa Mwana wa Mungu.

“Mtamwona Mwana wa Adamu.” Yesu alidai kuwa Mwana wa Mtu.

Katika kujibu swal la Kuhani Mkuu, Yesu alisema, “Mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa Nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni.” Hii ilikuwa ni kurejea kwenye kitabu cha Danieli katika Agano la Kale.

Danieli alisema, “Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu.”⁸³ Neno “Mwana wa Adamu” kilikuwa

⁷⁷ Yeremia 23:6

⁷⁸ Isaya 9:6

⁷⁹ Yohana 3:16

⁸⁰ Yohana 1:18

⁸¹ Yohana 10:30

⁸² Yohana 5:23

⁸³ Danieli 7:13, Toleo la King James

ni cheo cha Masihi. Wakati Kuhani Mkuu aliposikia jibu la Yesu, alijua kwamba Yesu alikuwa anajinasibu ni Masihi.


Hitimisho

Yesu hakuhukumiwa kwa aliyoyatenda; hakusulubiwa kwa kuponya watu au kwa kuwafundisha watu kuwapenda jirani yao. Yesu alisulubiwa kwa kile alichosema yeye ni nani. Wale watu waliomsikia Yesu akisema walijua kwamba alikuwa anajinasibu kuwa Mungu. Wale waliosema, "Kamwe Yesu hajawahi kujinasibu kwamba ni Mungu" hawaelewi maneno ya Yesu kama na vile Wayahudi walivyokuwa wanamwelewa walipokuwa wanamsikia wakati wa huduma yake duniani.

Yesu kwa uhakika alijinasibu kuwa ni Mungu. Na aliyathibitisha maneno yake yote kwa matendo yake. Siyo tu kwamba alimponya yule aliyekuwa na mwenye kupooza kuonyesha kwamba alikuwa na uwezo wa kumsamehe dhambi; bali pia alifanya miujiza mingine mingi, kuonyesha uwezo wake juu ya mambo ya asili na hata kifo chenyewe. Alimfufua Lazaro kutoka kwa wafu, akijiita mwenyewe kwamba ni "Ufufuo na Uzima." Kipekee kufufuka kwa Yesu kunathibitisha kwamba alikuwa ni yeye aliyejiita kama alivyo, aliyekuwa ni Mungu katika mwili.

Elimu ya Kuitetea Imani katika Vitendo – Kuongoka kwa Chuck Colson

Chuck Colson (1931-2012) alikuwa ni mmoja wa watendakazi wa Rais Richard Nixon katika Ikulu ya Raisi wa Marekani (*Jumba Jeupe.*)⁸⁴ Hata hivyo, Bw. Colson akaanza kujitambua kwamba maisha yake yalikuwa matupu. Alipokuwa ofisini kwake Ikulu, siku moja akajiuliza mwenyewe, "Maisha ni kitu gani? Ni lazima kuna kitu cha ziada katika maisha kuliko hivi nilivyo." Siku hiyo, Chuck Colson akajitambua kwamba hajui maana halisi ya ukweli wa maisha.



Mwaka 1972, baada ya kuacha utumishi katika Ikulu ya Raisi wa Marekani, Chuck Colson alikutana kwenye kikao na Tom Filipo, raisi wa kampuni moja kubwa. Colson akagundua kwamba Tom anaonekana mwenye Amani zaidi kuliko wakati uliopita. Alipomwuliza sababu za kuwa hivyo, alimwambia alikuwa ameyatoa maisha yake kwa Kristo.

Miaka miwili baadaye, dunia ilimgeuka kinyume kabisa Chuck Colson. Kwa sababu ya mambo aliyoyafanya alipokuwa mfanyakazi wa serikali, Colson alijijua kwamba ni lazima atafungwa gerezani. Akiwa katikati ya msukosuko huu, alimtembelea tena Tom Filipo. Filipo alimshirikisha Injili Bwana Chuck Colson. Akiwa anaendesha gari kurejea nyumbani usiku ule, Colson alilisimamisha gari lake pembedi na akaanza kuomba kwamba Mungu amsamehe dhambi zake.

⁸⁴ Image: "Chuck Colson", Nixon Presidential Library, retrieved from https://commons.wikimedia.org/wiki/File:Chuck_Colson.jpg, public domain.

Baada ya kumaliza kifungo chake gerezani, Chuck Colson aliendelea kumtumikia Mungu kwa uaminifu. Kwa kweli alijitoa maisha yake kuhudumia watu waliokuwa wamefungwa magerezani. Alihudumu kwenye huduma hii takribani miaka arobaini. Alitembea karibu dunia nzima akitembelea wafungwa kwenye magareza mabaya sana duniani; alianzisha Ushirika wa wafungwa wa Magereza, shirika linaloendelea kuwafikia wafungwa kwa Injili.

Mwaka 1984, Chuck Colson alitoa hotuba kwenye kongamano la Kitaifa la Watangazaji wa mambo ya kidini ambako alithibitisha ushahidi kuhusu ukweli wa Vitabu vya Injili. Katika hotuba yake, Bwana Colson alisema kwamba *Watergate* ilimshawishi kwamba Kufufuka kulitokeaa kweli kama Vitab vya injili vinavyotaarifu. Hii ni sehemu ya hotuba ya Bw. Colson:

Kuna ushahidi gani wa kufufuka kwa Yesu? Maelezo ya mitume walioshuhudia kwa macho. Mitume wote kumi na moja pamoja na Paulo walikwenda kwenye dunia iliyojulikana ya wakati ule kwa miaka 40 wakitangaza kwamba Yesu amefufuka kutoka kwa wafu. Kamwe, ingawaje walipitishwa kwenye mateso, vipigo, kufungwa jela, na hatimaye, wote isipokuwa mmoja, kifo cha mashahidi wafia imani – hawakuukana ufufuo wa ukweli wa Yesu Kristo.

Haya yote yana nini cha kufanya na Watergate? Ehrlichman, Haldeman, Mitchell, na mimi mwenyewe (viongozi katika Ikulu ya Nixon) tulimwamini Raisi kwa shauku kubwa. Tulikuwa katika mamlaka yetu na uwezo na marupurupu makubwa yasiyokuwa na kipimo. Hata pamoja na marupurupu ya ofisi yenye nguvu sana duniani, tishio la kwenda jela lilikuwa na nguvu sana, kiasi kwamba mmoja baada ya mwingine, wale waliohusika, waliachana na viongozi wao ili kujinrusu wasiadhibiwe kwa kuhusika katika uhalifu.

Hali hii inaungaje mkono ukweli wa kufufuka? Kirahisi ni hivi: Watergate inaonyesha asili ya mwanadamu. Kamwe hakuna anayeweza kunifanya niamini kwamba viumbu vya kibinadamu vya kawaida kumi na moja watavumilia kupigwa, kufungwa gerezani, na kifo bila kukataa kwamba Yesu Kristo alifufuka kutoka kwa wafu.

Ni kukutana tu na Mungu anayeishi kulikoweza kuwaweka katika kutoyumba. Vinginevyo, mtume Petro angeweza kumkataa Yesu ili kuokoa maisha yake mwenyewe. Alishafanya hivyo mara tatu.

Ushahidi ni mkubwa sana. Watu wale walishikamana na ule ushuhuda kwa sababu walimwona Kristo aliyeokuwa amefufuka kutoka kwa wafu. Na kama alikuwa amefufuliwa, hiyo inathibitisha uungu wake.⁸⁵

⁸⁵ Hii imenekuliwa kutoka katika hotuba iliyotolewa na Chuck Colson kwenye kongamano la Kitaifa la Watangazaji wa Kikristo Februari, 1984.

Uamuzi: Je! Yesu ni Mungu?

Njia nyingine ya kushughulikia madai kuhusiana na Kristo ni kufikiria njia mbadala. Agano jipya humwonyesha Yesu kama mtu aliyejinasibu kwamba ni Mungu. Tufanyeje na jambo hili? Kuna chaguzi tano, na mojawapo tu ndiyo inaweza kuwa sahihi: Aidha Yesu alikuwa ni Hadithi, ni Guru, ni Mwongo, ni Kichaa (*Majinuni*) au Bwana.

Je! Yesu alikuwa ni Hadithi?

Je! Yesu atakuwa ilikuwa ni hadithi? Baadhi ya wakosoaji husema kwamba Yesu hakuwahi kuwepo, au kwamba Yesu wa historia hakuwahi kusema au kutenda mambo yanayodaiwa katika Agano Jipya.

- Je! Itawezekana kwamba Agano Jipya haiaminiki au kwamba Vitabu vya Injili vilikuwa ni hadithi?

Taarifa za Yesu haziwezi zikawa ni hadithi. Tumeona kwamba Agano Jipya kihistoria inaaminika. Kuaminika kwa Agano Jipya kunathibishwa na kipimo cha Bibliografia, kipimo cha Ushahidi wa Ndani, na kipimo cha Ushahidi wa Nje. Agano Jipya hutoa picha halisi ya Yesu – alikuwa nani, alifanya nini, na alisema nini. Yesu hakuwa ni hadithi.

Je! Yesu alikuwa ni Guru?

Je! Yesu atakuwa alikuwa ni guru au ni mchaji wa Mashariki? Baadhi ya wakosoaji husema kwamba Yesu alikuwa ni sawa na waalimu wa theolojia ya Kihindu. Wanasema kwamba Yesu alifundisha kwamba sisi wote ni miungu.

- Je! Itawezekana kwamba Yesu alikuwa ni guru wa Mashariki aliyeamini kwamba kila mwanadamu ni mungu?

Yesu alikuwa ni Myahudi aliyezwa kikamilifu kabisa katika utamaduni wa Mungu mmoja.⁸⁶ Alikuwa ni mwalimu wa maandiko ya Kiyahudi. Hakuna Myahudi atakayetokea kusema kwamba sisi wote ni miungu. Kila mtoto wa Kiyahudi amekariri *Shema*: "Sikiza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja."⁸⁷

Mafundisho ya Yesu hayakuwa ya uchaji wa Kimashariki, bali mafundisho ya rabi wa Kiyahudi anayeamini katika Muumbaji mmoja aliye bora.

Je! Yesu alikuwa ni Mwongo?

Je! Yesu atakuwa alikuwa ni mwongo? Baadhi ya wakosoaji wanasema kwamba Yesu alikuwa anajitambua kwamba hana uungu. Wanasema kwamba aliwandanganya wafiasi wake. Wanasema kwamba alikuwa kama Jim Jones, Mmarekani aliyekuwa kiongozi wa ibada za madhehebu ya mafundiso potofu aliyewaongoza watu 900 kujiua huko Guyana; au

⁸⁶ Monotheistic inamaanisha kuamini katika Mungu alie mmoja tu.

⁸⁷ Kumbukumbu la Torati 6:4

Shoko Asahara, kiongozi mwingine wa aina hiyo wa Japani aliyewaongoza wafuasi wake kufia kwenye shambulio la gesi ya sarin kwenye njia ya chini kwa chini huko Tokyo.

► Je! Itawezekana kwamba Yesu alikuwa ni Mwongo aliyewadanganya wafuasi wake?

Petro Kreeft alisema kwamba Yesu hangeweza kuwa mwongo kwa sababu ya tabia yake. Hakuwa mchoyo, alikuwa na upendo, anayejali, mwenye huruma, na mwenye shauku katika kufundisha ukweli.⁸⁸ Hata wapinzani wake hawakuwa na lolote la kusema kinyume chake. Wakati wa kuendelea kwa kesi yake, ilibidi watafute mashahidi wa uongo.

Kreeft alisema kwamba Yesu hangeweza kuwa mwongo kwa sababu hakuwa na sababu ya kumfanya aseme uongo. Waongo hudanganya kwa sababu za ubinafsi, kupenda fedha, umaarufu, starehe au madaraka. Yesu aliachana na vitu vyote vizuri vya ulimwengu huu pamoja maisha yaliyokuwemo ndani yake. Badala yake, kujinasibu kwa Yesu kuwa Mungu kulimletea chuki, kukataliwa, kutolewana, mateso, maumivu makali na kifo.⁸⁹

Yesu hangeweza kuwa mwongo kwa sababu ya Ufufuo. Kama tutaiamini Biblia kwamba kihistoria inaaminika, ni lazima tukubali Kufufuka kuwa ni jambo la kweli. Ni Mungu peke yake anayeweza kufufua aliyekufa, na Mungu hangeweza akamfufua Yesu kutoka kwa wafu kama angekuwa mwongo.

Je! Yesu alikuwa ni Kichaa (*Mtu punguani*)?

Baadhi ya watu watasema kwamba Yesu hakudanganya, lakini kwa makosa aliamini kwamba yeye ni Mwana wa Mungu, Katika nukuu ya hapo juu, C.S.Lewis alionyesha kwamba mwanadamu wa kawaida anayeamini kwamba yeye ni Mungu, mtu huyo ni mwenda wazimu.

► Kwa kuangalia maisha ya Yesu kama inavyooneshwa kwenye Vitabu vya Injili, Je! Itawezekana kwamba Yesu alikuwa ni mtu punguani ambaye kimakosa alijinasibu kwamba alikuwa Mungu?

"Ninajaribu kumzuia mtu ye yeyote anayesema ujinga ambao watu mara nyingi husema kwamba: Niko tayari kumkubali Yesu kama mwalimu mkuu wa maadili, lakini sikubaliani na kujinasibu kwake kuwa ni Mungu.

Hicho ni kitu kimoja ambacho hatupaswi kukisema. Mtu ambaye alikuwa mtu wa kawaida tu na akasema mambo ambayo Yesu aliyasema hawezi akawa mwalimu mkuu wa maadili. Aidha atakuwa ni kichaa au la sivyo atakuwa Shetani wa Kuzimu. Ni lazima ufanye chaguo lako. Aidha mtu huyu alikuwa, au ni Mwana wa Mungu, au vinginevyo mwenye wazimu au kitu kingine kibaya zaidi. Unaweza kumfunga kama mpumbavu, unaweza kumtemea makohozi na kumuua kama pepo, au unaweza kuanguka miguuni pake na kumwita Bwana na Mungu; lakini tusije tukajiunga na upuuzi wowote wa yeye kuwa mwalimu mkuu. Hakuacha hilo wazi kwetu. Na hakukusudia kufanya hivyo."

- C.S. Lewis, *Mere Christianity (Ukristo tu)*

⁸⁸ Peter Kreeft, *Handbook on Christian Apologetics*, (IL: InterVarsity Press, 1994), 160

⁸⁹ Ibid.

Ni mtu ambaye ana ugonjwa wa akili tu anayeweza kuamini kwamba yeye ndiye Mwenyezi Mungu Muumba. Fikiria kwamba umekutana na mtu barabarani anayesema kwa kujiamini kabisa, "Mimi ni Napoleoni" au ni "Alexanda Mkuu." Utajua kwamba huyu mtu alikuwa mgonjwa wa akili.

Kama Yesu angekuwa ni mtu wa kawaida aliyeamini kwamba alikuwa Mungu, angekuwa ni mgonjwa wa akili. Lakini wanasaikolojia wanasema kwamba Yesu hakuwahi kuwa na alama ya ugonjwa wa kuchanganyikiwa. Alikuwa mkamilifu katika ujumla wa nafsi yake.

Mafundisho ya Yesu yalionyesha hekima yake kwa vitendo. Kitendo chake cha kuwajali wale waliokuwa kwenye mateso kilionyesha upendo kwa wengine ambao huwezi kutegemea kuupata kwa mtu ambaye ana ugonjwa wa akili. Kwa uhakika Yesu hakuwa mtu punguani.

Je! Yesu alikuwa ni Bwana?

Kama Yesu hakuwa ni hadithi, hakuwa guru, hakuwa mwongo, au hakuwa mtu punguani, uchaguzi wa mwisho utakaokuwa umebakia ni kwamba alikuwa ni yeye kabisa kama alivyokuwa amejisema mwenyewe; Yesu alikuwa ni Bwana. Kama wanafunzi wake baada ya kufufuka, ni lazima tumwabudu Yesu kama Bwana na Mungu!

Hitimisho letu kutokana na kuangalia hizi chaguzi tano unaendana na hoja ya ujumla ya Ukristo tuliojifunza hapo awali. Kwa kuwa Agano Jipyä kihistoria ni sahihi, tunazo sababu za kutosha za kuamini kwamba Yesu alifufuka kutoka katika wafu na kutimiza dazani za unabii zilizohusiana na Masihi. Haya mambo mawili yanaonesha kwamba Yesu ni yeye yule aliyejinasibu kuwa – Mwana wa Mungu, na Mungu aliyejekuwa katika mwili.

Katika somo hili, tumeona kwamba Yesu ni Mungu kama alivyojinasibu kuwa. Kwa kuwa Yesu ni Mungu, ni lazima tumkubali kama mamlaka isiyoweza kukosea. Yeye anaaminika kwa kila hali. Kwa hiyo ni lazima tukubaliane na madai yake ya kuwa yeye ndiye peke yake njia ya kwenda kwa Mungu. Ni lazima pia tukubaliane na madai yake kwamba, Biblia (*Neno la Mungu*) inatoka kwa Mungu, Ukristo ni wa kweli. Ni kwa jinsi tunajibu ukweli huu ndio jambo la muhimu sana.

Hitimisho

"Lee," Jia alisema, "Tuko katika mahali muhimu sana. Tumeona ushahidi wa uwepo wa Mungu; tumeona ushahidi wa uumbaji; tumeona ushahidi wa kuaminika kwa Agano Jipy;a; tumeona ushahidi kwamba Yesu ni yeye yule kama alivyojinasibu aliquwa.

"Lee, katika mazungumzo yetu yote, tumeona kwamba:

- Agano Jipyka kihistoria linaaminika na ni la kutegemewa.
 - Yesu alifufuka kutoka katika wafu na kutimiza dazani za unabii zilizohusiana na Masihi.
 - Kufufuka kwa Yesu na kutimilika kwa unabii kunaonesha kwamba Yesu ni yeye yule aliyejinasibu kuwa – Masihi, Mwana wa Mungu, na Mungu aliyejina katika mwili.

- Akiwa ni Mwana wa Mungu, Yesu ni mamlaka isiyoweza kukosea.
- Yesu Kristo alifundisha kwamba Biblia ni Neno la Mungu na kwamba yeye ndiye peke yake njia ya kwenda kwa Mungu.

"Kwa kuwa yote haya ni kweli, kuna hitimisho moja tu la uhakika. Kama Yesu alikuwa Mungu, tunapaswa tuamini alichosema: Biblia ni Neno la Mungu, na Yesu ndiye njia peke ya kwenda kwa Mungu. Kwa hiyo, Ukristo ni wa kweli.

"Lee, swalilangu ni hili, 'Je! Utaamini?' Uko tayari kusalimisha maisha yako kwenye mamlaka ya Yesu, Mwana pekee wa Mungu?"

Kwa machozi katika macho yake, Lee alijibu, "Jia, Je, unakumbuka uliponiambia kuhusu "Thomasi mwenye mashaka?" Hivyo ndivyo mimi nilivyo; ninahitaji ushahidi kwa wengi. Lakini wiki iliyopita, nilisoma zaidi kuhusu Tomaso katika Biblia yako. Baada ya kuuona ushahidi, Tomaso alisema, "Bwana wangu na Mungu wangu!"⁹⁰ Macho ya Tomaso yalifumbuliwa, aliuona ushahidi, na akaamini.

"Jia, nimeuona ushahidi – na ninaamini. Nilipokuwa nasoma habari za Tomaso, Mungu alifungua macho yangu katika kuuona ukweli wa BiBlia. Nilikuwa kipofu, lakini sasa ninaona! Niko tayari kuyasalimisha maisha yangu kwa Yesu. Uko tayari kuomba pamoja nami?"

Kazi za kufanya Somo la 8

(1) Elimu ya kuitetea imani na Kichwa: Utaanza kipindi kinachofuata kwa mtihani kutokana na maswali ya tafakuri yaliyoko katika Somo la 8. Jifunze maswali haya kwa uangalifu kwa maandalizi ya mtihani

(2) Elimu ya kuitetea imani na Moyo: Watu wengi wanaodai kwamba wao ni Wakristo husema, "Mimi nimeamini," lakini hizo ni fikra za akili zao tu zinzoujua ukweli lakini siyo watifi kwa Yesu. Katika kitabu cha Yohana, neno "Ninaamini" lina maana ya kutii kwa hiari. Kama hatutatii, basi hutaamini. Je! Unaamini? Je! Unaishi kwa utii? Kama sivyo, jiachilie sasa kwa ukamilifu na kwa utii kabisa kwa Mungu.

(3) Elimu ya kuitetea imani na Mikono: Zungumza na asiyeamini kuhusu Yesu kujinasibu kwamba yeye ni Mungu. Kabla hujawaonyesha yale Yesu aliyosema, uliza, "Unafikiri nini kuhusu Yesu? Kama hakuwa Mungu, unadhani alikuwa nani? Waonyeshe kwamba uchaguzi mmoja tu wenye maana ni kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu (Mungu Mwana), kama alivyosema. Toa taarifa kuhusu mazungumzo yenu katika kipindi cha darasa kitakachofuata.

Mtihani wa Somo la 8

(1) Orodhesha kauli nne za wakati wa huduma yake kuonyesha kwamba Yesu alijiamini kwamba ni Mungu.

⁹⁰ Yohana 20:28

- (2) Orodhesha kauli tatu za wakati wa kuendelea kwa kesi yake kuonyesha kwamba Yesu alijiamini kwamba ni Mungu.
- (3) Je, ni chaguzi ngapi tano za kuzingatia kwenye madai ya Yesu ya kujinasibu kwamba yeye ni Mungu?
- (4) Kwa kifupi elezea tatizo la kila kipengele katika chaguzi nne za mwanzo.
- (5) Andika Kauli sita na hitimisho kwa ajili ya hoja ya Ujumla ya Ukristo.
- (6) Nukuu kutoka kichwani Yohana 20:30-31.

Somo la 9

Upekee wa Ukristo katika Dini Nyingi

Utangulizi

Katika Maonyesho ya Dunia ya Chicago mwaka 1893, Bunge la Dini mbalimbali liliruhusu uwakilishi wa wajumbe kutoka kila dini kubwa za dunia kutoa mada. Wanenaji kutoka kila dini walijaribu kuishawishi hadhira kwamba dini zao zilikuwa bora na za maana zaidi kuliko za wengine.

Mwakilishi wa mwisho kunena alikuwa Mchungaji Yusufu Cook, aliyekuwa akiwakilisha imani ya Kikristo. Kabla ya Cook kunena, msemaji wa dini ya Hindu akaushambulia Ukristo kama "dini iliyo mbaya kuliko dini nyingine zote" kwa sababu inawaita watu "watenda dhambi."

Badala ya kushambulia dini nyingine yeyote, Yusufu Cook alianza kwa kumwelezea Bi. Macbeth kutoka kitabu cha Shakespeare. Alielezea jinsi Bi. Macbeth, kutokana na vivu na matamanio, alivyomshawishi mumewe kumwua mfalme Dankani wakati alipokwenda kumtembelea katika kasri lake.

Baada ya kitambo kidogo, Bi. Macbeth alipatwa na maumivu makali ya kujisikia mwenye hatia. Wakati wa mchana, alikuwa na tamaa ya makuu na mjasiri. Lakini usiku, Bi. Macbeth ataamka mara kadhaa kwenda kuosha mikono huku akilia, "Nina doa." Je! Kwa kuosha mikono atatakasika?

Yusufu Cook alimwuliza mwakilishi wa kila dini, "Je! kuna chochote katika dini yenu kinachowenza kuondoa damu ya hatia iliyoko kwenye mikono ya Bi. Macbeth?" Hakuna hata mmoja aliyeongea. Hakuna dini yenye uwezo wa kuosha damu kutoka katika mikono ya Bi. Macbeth?" Hakuna aliyeongea. Hakuna dini yenye uwezo wa kuosha damu kutoka katika mikono ya Bi Macbeth. Kisha Mchungaji Cook akageukia kwenye hadhira na kuhitimisha, 'Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, inatutakasa kutokana na dhambi zetu!"

Katika somo hili, tutaona kwamba Ukristo uko tofauti na dini nyingine zote. Tofauti iliyopo kati ya injili na dini nyingine ni hii: tunaamini kwamba alikuja duniani katika sura ya kibinadamu ya Mwanae, Yesu, kutoa njia ya msamaha kwa ajili ya dhambi zetu na kuturejesha tena katika sura na mfano wake.

Je! Ukristo ndio Imani Pekee ya Ukweli?

Swali la kawaida ambalo Wakristo wanakumbana nalo kila wakati ni, "Dini zote si ziko sawa? Ni njia mbalimbali za kuelekea kwenye lengo moja. Ili mradi unapata njia unayoiona inakufaa, ni sawa."

- Utamjibuje Baniani anayesema, "Ukristo na Ubani ya ni njia mbili tofauti za kuelekea kwenye lengo moja?"

Mjadala unaofuata utatusaidia kuona vyema ni nini kinachoutenga Ukristo na mitizamo mingine yote ya dunia.

Kuna imani za aina tano tofauti kuhusiana na uwepo na asili ya Mungu: **Imani kwamba hakuna Mungu**; Imani kuwa Mungu yumo ndani ya kila kitu na kuwa kila kitu ni Mungu; Mungu anautegema ulimwengu aweze kuwepo; Imani ya kuabudu miungu wengi; na Imani kwamba kuna Mungu mmoja tu.

Imani kwamba hakuna Mungu: Inafundisha kwamba hakuna Mungu. Inakanusha kwamba hakuna chochote zaidi ya ulimwengu wa kawaida.

Imani kuwa Mungu yumo ndani ya kila kitu na kuwa kila kitu ni Mungu: Inafundisha kwamba kuna uwezo wa mungu, lakini huyu mungu hana tofauti na ulimwengu. Mungu siyo kiumbe binafsi aliyeumba ulimwengu. Yeye ni Roho au Akili anayefanana na dunia. Uhindu (*Ubaniani*) ni mfano wa dini hii.

Imani kuwa Mungu anautegema ulimwengu aweze kuwepo: Inafundisha kwamba Mungu ni tofauti na ulimwengu lakini anautegemea ulimwengu ili aweze kuwepo. Kuna ushirikiano tegemezi kati ya Mungu na ulimwengu.

Imani ya kuabudu miungu wengi: Inafundisha kwamba kuna miungu wengi. Wamormoni ni mfano wa dini inayoabudu miungu wengi. Hata hivyo, Biblia inafundisha kwamba kuna Mungu mmoja tu.

Bwana, Mfalme wa Israeli, Mkombozi wako, Bwana wa majeshi, asema hivi; Mimi ni wa kwanza, na mimi ni wa mwisho; zaidi yangu mimi hapana Mungu.”⁹¹

Kabla yangu hakuumbwa Mungu awaye yote, wala baada yangu mimi hatakuwapo mwingine.⁹²

Katika mitazamo ya kidunia ya dini zilizotajwa hapa, hakuna hata moja inayoonesha njia ya kumuunganisha mwanadamu na Mungu. Imani hizi zinahitilafiana na Biblia na kwa falsafa na kwa ushahidi wa kisayansi. Ushahidi tuliojifunza katika kozi hii unaelekezwa kwa Mungu aliyevuka mipaka ya uwezo wa binadamu, aliye huru, aliye wa milele, asiyekuwa na mwili kama mwanadamu, na Mungu mwenye hekima aliyeumba ulimwengu na ambaye ana mwingiliano na wanadamu.

Imani ya kumwamini Mungu mmoja tu (**Monotheism**) inafundisha kwamba kuna Mungu mmoja tu aliye tofauti na dunia, wa milele, binafsi na aliye na uweza wa kiungu. Dini tatu kubwa zinazoamini katika Mungu mmoja tu ni za Kiyahudi, Kiislamu na Kikristo. Dini hizi zinafundisha kwamba Mungu aliingilia kati katika ulimwengu ili atuletee wokovu wetu.

Dini ya Kiyahudi (**Judaism**), iliyozishwa na Mungu kupitia Abrahamu na Musa, ilikamilishwa na Kristo. Isipokuwa kwa Wayahudi (Wakristo) wa Kimasihi, dini ya Kiyahudi

⁹¹ Isaya 44:6

⁹² Isaya 43:10

ya wakati wa sasa imemkataa Yesu kama mkamilishaji wa unabii zilizohusiana na Masihi. Mfumo wa Wayahudi wa utoaji dhabihu unaelekezwa kwa Yesu kama dhabihu ya mwisho kwa ajili ya dhambi zetu. Wayahudi wa wakati wa sasa hawana msingi katika dhana ya msamaha kama watamkataa Yesu. Kwa wakati wa sasa hata hawatoi tena dhabihu.

Dini ya Kiislamu (**Islam**) ilianzishwa kwenye karne ya saba katika Makka na Madina. Mohammedi alianzisha dini ya uongo kutokana na kusambaa kila mahali kwa dini za Kiyahudi na Kikristo. Kuna mambo mengi ya imani ya kufanana katika dini hizi kwa sababu zina msingi mmoja wa kuanzishwa kwake, lakini kuanzia mwanzo, Uislamu umewaongoza watu nje kabisa na ukweli wa uungu wa Yesu, kifo chake na kufufuka kwake.

Uislamu hauna msingi wa kutosha wa msamaha kwa sababu hauna mbadala wa upatanisho. Katika Uislamu, mtu anaweza kusamehewa tu endapo matendo yake mema yakipimwa yatazidi mabaya. Hata hivyo, tunajua kwamba hakuna kiwango chochote cha mema, hata kama tungelikuwa na chochote, kinachoweza kusimama kwa niaba ya dhambi zetu kinyume na Mungu asiyekuwa na mwisho wa utakatifu.

Ni Ukristo tu (**Christianity**) ulio na njia ya msamaha wa dhambi. Tulikuwa na hitaji la mpatanishi atakayekuwa daraja kwa ajili ya pengo lililokuwepo kati ya mwanadamu na Mungu. Dhambi ilitutenga na Mungu, lakini mpatanishi ambaye alikuwa ni Mungu na mwanadamu kwa wakati mmoja aliweza kuleta upatanisho wa Mungu na binadamu kwa maisha na kifo cha Yesu na suluhu.⁹³ Kama Mungu, Yesu alimwakilisha Mungu kwa mwanadamu. Kama mwanadamu, Yesu alimwakilisha mwanadamu kwa Mungu. Alikuwa ni mpatanishi wa kiungu-mwanadamu, ambaye katika kifo chake na kufufuka kwake, aliwaleta Mungu na mwanadamu pamoja.

Yesu ilibidi kwa pamoja awe Mungu na Mwanadamu ili kukamilisha kile alichokifanya. Dhabihu ya kifo ilikuwa ni lazima kwa ajili wa upatanisho wa dhambi. Ni katika mwili tu Yesu angeweza akafa. Na peke yake kama Mungu, Yesu angeweza kuwa dhabihu nzuri sana na toshelevu kwa ajili ya dhambi zetu kwa Mungu asiye na mwisho. Pia, Yesu alihitaji kuwa wa Mungu ili kusambaratisha kifo na dhambi kwa nguvu ya kufufuka kwake.

Kifo cha upatanisho na kufufuka kwa Yesu aliyekuwa Mungu-mwanadamu ndiko kunakotofautisha kati ya Ukristo na dini nyingine. Ni Ukristo peke yake unaoonesha njia kwa ajili ya mwanadamu kusamehewa dhambi zake na kupatanishwa na Mungu kwa njia ya imani. Ni Ukristo peke yake ulioonesha njia ya kumrejesha mwanadamu kwenye sura na mfano wa Mungu. Ndiyo maana Yesu alisema kwamba yeye ndiye Njia, na Kweli, na Uzima, na kwamba hakuna mtu atakayekuja kwa Baba, ila kwa njia ya yeye..⁹⁴

⁹³ 1 Timotheo 2:5; 2 Wakorintho 5:18-21

⁹⁴ Yohana 14:6

Je, Imani ya Utatu Mtakatifu ni muhimu kwa Imani ya Kikristo?

Kama Yesu ni Mungu, je, haimaanishi kwamba kuna Mungu wengi? Hapana. Imani ya Utatu Mtakatifu wa Mungu inafundisha kwamba kuna Nafsi tatu ndani ya kiumbe mmoja wa kiungu aitwaye Mungu. Hizi nafsi tatu ni Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Kuna sababu nyingi za kuitetea imani ya Utatu Mtakatifu dhidi ya wale wote wanaoipinga.

Imani ya Utatu Mtakatifu (Mungu mmoja aliyedhihirishwa katika nafsi tatu) ni sifa ya kutofautisha Ukristo. Imani hii inatofautisha Ukristo na imani ya Kiyahudi na ya Kiislamu, dini nyingine kubwa mbili zilizotajwa hapa zinazoamini katika Mungu mmoja.

Uislamu unaikataa imani ya Utatu Mtakatifu, ingawaje Waislamu wanaamini katika Mungu mmoja binafsi mwenye uwezo unaozidi wa binadamu. Waislamu wanasema kwamba Mungu hawezi akawa na mtoto, kwa hiyo wanamkataa Yesu kwamba siyo mtoto wa Mungu, au Mungu Mwana. Sehemu ya tatizo ni kwamba Waislamu wanaamini kwamba kupata mtoto kunahusisha asili ya kukutana kimwili na kufanya tendo la ndoa kati ya baba na mama. Hiyo siyo imani ya Kikristo ya Uwana wa Yesu. Hakuna wakati wowote ambao mwana hakuwahi kuwa mwana. Uwana wa Yesu siyo wa kimwili; Uwana unahusisha uhusiano maalumu kabisa ambao Yesu amekuwa nao na Baba yake tangu milele. Yesu alikuwa Mwana hata kabla ya mimba yake kutoka kwa Roho Mtakatifu, na kuzaliwa na bikira Mariamu ili aishi mionganoni mwetu kama mwanadamu.

Baadhi ya wasiokuwa Wakristo hufikiri kwamba Wakristo ni waumini wa miungu mitatu.⁹⁵ Lakini hivi sivyo ilivyo. Wakristo ni waumini wa imani ya Mungu mmoja tu. Tunaamini kwamba yuko Mungu mmoja tu, lakini kuna nafsi tatu zinazokaa ndani ya huyo Mungu mmoja. Hizi nafsi tatu hushirikishana asili moja. Hawa siyo miungu inayotofautina.

Ushahidi wa Kibiblia kuhusu Utatu Mtakatifu

Hapa kuna shauri la kibiblia la imani ya Kikristo kwamba kuna Mungu mmoja ambaye amejifunua mwenyewe kama Nafsi tatu: Baba, Mwana, na Roho mtakatifu. Kauli zifuatazo zinafundishwa kwenye Biblia. Hizi zinafanya msingi wa imani ya Utatu Mtakatifu.

Kigezo mantiki A: Kuna Mungu mmoja tu.

"Sikiza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja."⁹⁶

"Mimi ni Mungu, wala hapana mwingine; mimi ni Mungu, wala hapana aliye kama mimi."⁹⁷

⁹⁵ *Tri-theist* ni watu wanaoamini katika miungu mitatu tofauti.

⁹⁶ Kumbukumbu la Torati 6:4

⁹⁷ Isaya 46:9

Kigezo mantiki B: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu wanatambuliwa na Maandiko kama Mungu.

“...na Mungu Baba....”⁹⁸

“...Neno alikuwa Mungu.... Naye Neno alifanyika mwili.”⁹⁹

“...kwa nini Shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo Roho Mtakatifu,... Hukumwambia uongo mwanadamu, bali Mungu.”¹⁰⁰

Kigezo mantiki C: Hizi Nafsi tatu yanahusiana zenyewe na kwa dunia kama Nafsi tofauti.

Kwenye ubatizo wa Yesu:¹⁰¹

- Mwana alibatizwa,
- Roho Mtakatifu alishuka kama hua
- Baba alizungumza kutoka mbinguni, akasema, “Wewe ni Mwanangu mpendwa, nipendezwaye naye.”

Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu siyo nafsi zinazofanana; kila nafsi ikifanya majukumu tofauti na mwingine kwa wakati mmoja.

Kukaribia mwisho wa huduma yake, Yesu alisema atamwomba Baba atutumie “msaidizi mwingine” – Roho Mtakatifu.¹⁰² Kuna Nafsi tatu tofauti zinazohusika katika ombi hili. .

Hitimisho: Mungu mmoja wa kweli wa Biblia alijidhihirisha mwenyewe kuwepo katika Nafsi tatu tofauti: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Mungu ni mmoja kwa asili, lakini katika Nafsi tatu.

Ingawaje neno *Utatu Mtakatifu* halione kani katika Biblia, imani ya Utatu Mtakatifu ina msingi wake katika taarifa za Maandiko. Biblia inaonyesha kwa ukamilifu uwepo wa Nafsi tatu tofauti. Kila Nafsi inatambulika kama Mungu mmoja wa ulimwengu huu.

Huu siyo mkanganyiko kwa sababu Wakristo hawasemi kwamba Mungu kwa pamoja ni nafsi moja na nafsi nyingine tatu. Wakristo hawasemi kwamba Mungu kwa pamoja ni Mungu mmoja na miungu wengine watatu. Badala yake, Wakristo wanasema Mungu ni mmoja kwa asili katika nafsi tatu.

⁹⁸ Wagalatia 1:1

⁹⁹ Yohana 1:1, 14


¹⁰⁰ Matendo ya Mitume 5:3-4

¹⁰¹ Marko 1:10-11

¹⁰² Yohana 15:26

Mfano wa Utatu Mtakatifu

Ulimwengu ni moja ya mfano mzuri wa Utatu Mtakatifu. Ulimwengu wote kwa pamoja una vipengele vitatu tu muhimu: - nafasi, muda na mata. Kama utaondoa hapo kimoja katika hivi vitatu, hutakuwa na ulimwengu tena.



Nafasi inakuwa na *urefu*, *upana*, na *kimo* – vitu vitatu ndani ya kimoja. Kama ingekuwa ni kuondoa kimojawapo cha vipimo hivi vitatu, hutakuwa na nafasi tena.

Muda unakuwa na uliopita, uliopo, na ujao – vitu vitatu ndani ya kimoja. Kama ingekuwa ni kuondoa kimojawapo ya vipengere hivi, hutakuwa na muda tena.

Mata ina nguvu iliyo kwenye mwendo unaotengeneza tukio (*phenomena*) - vitu vitatu ndani ya kimoja. Bila nguvu, hakuwezi kuwepo na mwendo au *tukio*. Bila mwendo, hakuwezi kuwepo na nguvu au *tukio*. Kama hakuna *tukio*, ni kwa sababu hakuna nguvu au mwendo.¹⁰³

Suala la “vitu vitatu ndani ya kimoja” ni sehemu ya asili kamili ya ulimwengu. Je! Inawezekana kwamba Mungu aliutengeneza ulimwengu ili kuakisi hali ya Utatu? Naamini kwamba Mungu aliacha alama zake za vidole kwenye uumbaji. Kama vile ulimwengu mmoja unavyokuwa na nafasi, muda, na mata, Mungu mmoja naye anakuwa na Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.


Mchoro wa asili wa Utatu Mtakatifu

Imani ya Kibiblia kuhusiana na Utatu Mtakatifu imefundishwa na Kanisa tangu wakati wa mitume. Kulia ni mchoro ambao kanisa limetumia kuelezea Utatu Mtakatifu.



Imani ya Utatu Mtakatifu ni Muhimu sana kwa Imani ya Kikristo

Baadhi ya watu wanasema kwamba siyo muhimu kuamini imani ya Utatu Mtakatifu, na kwamba zina makosa. Imani ya Utatu Mtakatifu ni msingi wa mafundisho makuu muhimu ya Injili. Kwa mfano, wanaokataa Utatu Mtakatifu wa Mungu, wao hukataa kwamba Yesu ni Mungu. Lakini kama Yesu siyo Mungu, kifo chake hakikuleta ukombozi.

ULIMWENGU WOTE



MUDA



¹⁰³ Kwa maelezo zaidi, soma Nathan Wood, *Trinity in the Universe* (MI: Kregel Publications, 1984).

Kama tutakataa kwamba Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wanatofautiana, tutakuwa tunakataa tabia za Mungu za nafsi na mahusiano. Kwa mfano, Mungu hangekuwa wa upendo tangu umilele kama ilikuwa angojee hadi alipoumba ili aweze kumpenda kila mtu. Lakini kama Mungu ni zaidi ya nafsi moja, Nafsi hizi zinaweza kupendana kwa umilele wote.

Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni Nafsi zinazoishi kwa mahusiano na kila mmoja.

Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu siyo mashirika yasiyokuwa watu. Kila mmoja ana utu na wanaishi katika uhusiano binafsi na mwingine. Tunawaita Nafsi kwa sababu wanaishi katika uhusiano na mwingine. Kila mmoja katika Utatu Mtakatifu anaweza kujirejea kama "Mimi" na kwa mwingine kama "Wewe." Ingawaje Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ni Mungu mmoja, wako katika Nafsi tofauti kila mmoja akimpenda mwenzake, akitoa kwa mwingine, akiwasiliana na mwingine, na akiishi kwa ajili ya mwingine. Ni Nafsi za kweli.

Imani ya Utatu Mtakatifu inagusa utu na mahusiano ya mwanadamu.

Utatu Mtakatifu ndio chanzo cha utu wetu. Mungu alitufanya katika mfano wake. Kama ilivyo kwa Utatu Mtakatifu, tuna uwezo wa kuwasiliana sisi kwa sisi, na sisi na Mungu. Tuna akili, utashi na mihemuko ambayo hutupa sisi uwezo huu.

Utatu Mtakatifu hugusa jinsi tunavyowasiliana na mwingine, pia na Mungu. Kwa kuwa hizi Nafsi za Utatu Mtakatifu zinakaa katika kuoneshana upendo zenyewe kwa kila mmoja, tunapaswa tuishi kwa kuoneshana upendo sisi kwa sisi na kwa watu wengine. Hiyo ndio njia ambayo Mungu ametuumba nayo. Tumeumbwa kwa mfano wa Mungu. Tumeumbwa tuwapende wengine kama washiriki wa Utatu Mtakatifu wanavyopendana wenyewe.

► Je! Unaweza kuelezea Imani ya Utatu Mtakatifu kwa Muislamu anayeamini kwamba Wakristo wanaamini miungu mitatu?

Ni kwa jinsi gani Wakristo wajibu kuhusu Imani Katika mizimu (animism)?

Katika Afrika, wasioamini wengi wana heshima kubwa na hata hofu kwa maroho (*mizimu*). Watu hawa mara nyingi huwaauliza Wakristo, "Kwa nini nimwamini Mungu ambaye simwoni wakati familia yangu wameshakutana na roho za wahenga wetu? Tumeona nguvu zao. Tunaona kwamba wanaishi. Kwa nini tumwabudu Mungu ambaye haonekani?"

Ikiwa inaitwa "Imani katika mizimu" au "Dini ya Kikabilia" au "Dini ya Asili", mtizamo huu unazua changamoto kubwa sana kwa Elimu ya Wakristo ya kuitetea imani. Unapojaribu kufanya huduma ya Uinjilisti mionganoni mwa wabudu mizimu, usitarajie kuulizwa maswali kama, kuna ushahidi gani wa nyaraka kuhusiana na Biblia? Au "Kuna hoja gani ya sayansi ya dunia (kosmolojia) kuhusu uwepo wa Mungu?"

Randall McElwain wakati mmoja aliuliza kikundi cha wachungaji wa Kiafrika, "Ni kwa jinsi gani mnawathibitishia watu wasioamini kuhusu uwepo wa Mungu?" Walijibu kwa kucheka. "Kila mtu katika Afrika ni makini sana kujua kwamba kuna Mungu! Ni Wamarekani na watu wa Magharibi tu wanaofikiri kwamba Mungu hayupo. Watu wetu hawaaulizi 'Je! Mungu yupo?' Badala yake wanaauliza, 'Je! ni Mungu gani mwenye nguvu zaidi?'"

Ni kwa jinsi gani mtetea imani wa Kikristo ataweza kujibu hoja za wanaoamini mizimu? Tutaangalia kupidia maswali manne:

1. Mizimu ni nini?
2. Kuna tofauti gani kati ya mizimu na Ukristo?
3. Je! mizimu na Ukristo vinaweza kuchanganywa pamoja?
4. Ni kwa jinsi gani tunaweza kuwasilisha Injili kwa waamini mizimu?

Imani katika mizimu ni nini?

Imani katika mizimu ni mtazamo katika nguvu za asili na roho za mababu (mizimu) kuwa ni vitu hai vyenye utambulisho tofauti. "Mizimu" hutafuta mahali pa kuishi kama vile wanyama, mimea, na miamba. "Mizimu ya watu wa zamani" ni watu katika familia lakini waliokufa. Mara nyingi wanapewa heshima kama wanajamii wa familia husika.

Kwa mujibu wa dini nyingi za kikabila, hizi roho zina ufinyu katika utendaji. Uwezo mkubwa walio nao unatokana na asili ya miili isiyoonekana waliyo nayo. Mara nyingi hawatabiriki na wanaweza wakasababisa madhara makubwa kwa wanadamu. Wanaweza kufanya kazi bila kuonekana kwa sababu hawana miili ya kuonekana, lakini nguvu zao zina ukomo. Kwa sababu ya hiyo, zinawezakudhibitiwa na mganga wa kienyeji, au kiongozi wa kiroho. Mara nyingine wanaweza kudhitiwa na maneno ya kiuganga au hirizi.

Taratibu nyingi za mizimu zinaelekezwa katika kutuliza na kubembeleza kwenye ulimwengu wa roho, Aidha ni fedha zilizochomwa moto kama sadaka kwa watu waliokufa zamani, au dhabihu kwa maroho (mizimu). Imani ya katika mizimu hujaribu kutuliza na kubembeleza ulimwengu wa maroho.

Kuna Tofauti gani kati ya Imani ya mizimu na Ukristo?

Hofu badala ya Upendo

Labda tofauti kubwa iliyoko kati ya Imani katika mizimu na Ukristo ni uhusiano uliopo kati ya Mungu na mwanadamu. Kwenye Imani ya mizimu, uhusiano kati ya mwanadamu na maroho ya asili au mizimu, ni hofu. Wenyewe Imani hiyo mara nyingi huishi wakiwa katika hofu endelevu kutokana na kile ambacho mizimu ya wahenga wao inaweza kuwatendea. Hakuna kushirikiana salamu au mahusiano. Malengo ya watu wengi wenye Imani ya mizimu ni kutoa heshima kamili kwa hii mizimu ili kuuepukana na matatizo. Mitambiko na maombi hufanyika ili kukidhi mahitaji ya haya maroho. Wachawi na wenye waganga wa asili huwa wanalipwa kuthibiti ulimwengu wa maroho.

Kwa tofauti, Wakristo wanamwabudu Mungu ambaye anafuatilia uhusiano wa upendo wake na mwanadamu. Mungu alitembea katika Bustani ya Edeni akiwa na Adamu na Hawa. Mungu alimtuma mwanae kuishi pamoja nasi na kufa kwa ajili ya kuwa fidia ya dhambi

zetu. Kristo tayari alishaituliza ghadhabu ya Mungu. Kwa dhambi zetu, tulileta laana ya Mungu, lakini Mungu alitoa upatanisho kuititia zawadi ya Mwana wake wa pekee.¹⁰⁴

Kwa kuwa Yesu tayari ameshalipia gharama ya dhambi zetu, uhusiano wetu na Mungu sasa ni ule wa upendo, na siyo hofu. Kama tutaitikia mwito wake wa ukombozi wa bure, Mungu ameahidi kwamba tataridhi umilele pamoja naye. Hatuhitajiki kuishi kwenye hofu. Tunaweza kuishi kwenye uhusiano wa upendo.

Kuishi kwa majaaliwa badala ya matumaini

Wenye imani ya mizimu hukiona kifo kama chanzo cha hofu kuu. Hakuna ahadi ya maisha baada ya kaburi. Hakuna ahadi ya kuungana tena na familia. Hakuna matumaini ya Mungu mwenye huruma.

Kwa tofauti, Wakristo huutazamia uzima wa milele pamoja na Mungu wao mwenye upendo. Kwa Mkristo, maisha ni kusonga mbele kwenye furaha isiyokuwa na mwisho.

Maroho ya mbali badala ya Mungu aliye karibu.

Tofauti nyingine kati ya wenye imani ya mizimu na Wakristo ni msisitizo wao wa kutegemea mizimu badala ya Mungu. Hata wale wenye imani ya mizimu wanaotambua Mungu aliye mkuu, hutoa msisitizo zaidi kwa mizimu badala ya Mungu.

Kwa ulinganifu, Wakristo wanapaswa kuweka umakini wao kwa Mungu na siyo kwa ulimwengu wa maroho. Biblia inashuhudia kuhusu uhalisia wa ulimwengu wa maroho. Hata hivyo, Biblia inatoa maelezo machache kuhusiana na ulimwengu huu wa maroho. Biblia haijatufundisha chochote jinsi ya kuwasiliana na maroho (aidha mazuri au mabaya). Haijasema lolote ni kwa jinsi gani tunaweza kutumia nguvu za maroho yaliyo ili kutusaidia. Kwa nini? Kwa sababu Mungu peke yake ndiye chanzo cha nguvu zetu na maarifa yetu.

Je, Imani katika mizimu na Ukristo vinaweza kuchanganywa pamoja?

Baadhi ya Wakristo wamesema, "Ndio, Ukristo ni dini ya kweli. Hata hivyo, tunaweza kuuchanganya Ukristo na dini za asilia za mizimu." Uchanganyaji wa Ukristo wa kweli na dini nyingine unaitwa **usawazishaji wa Imani (syncretism)**.

Baadhi ya "makanisa huru" katika Afrika wameunganisha ujumbe wa Ukristo na dini za kikabilo. Mara nyingi hii ilianza na jaribio la nia njema la kuiweka injili kwa mazingira ya Waafrika. Baadhi ya wachungaji wa Kiafrika walitambua kushindwa kwa wamisionari wengi wa kimaghari kuhasilisha injili katika Afrika bila ya kuingiza "masuala" yote ya utamaduni wa magharibi. Wachungaji hawa walitaka Wakristo wa Kiafrika kuimba nyimbo za Kiafrika, kuvaa nguo za Kiafrika, na kuabudu katika hali na utaratibu halisi wa Kiafrika.

Ingawaje juhudhi hizi zote zilianza kwa nia njema, lakini makanisa mengi yameiga hizi desturi ambazo ni kinyume kabisa na injili. Katika huu "Ukristo Uliosawazishwa," Mungu yuko mbali

¹⁰⁴ Yohana 3:16

kama maroho yalivyo mbali.. Waliokufa zamani wanaonekana kama wapatanishi kati ya waabuduji na Mungu. Kuna msisitizo mdogo sana kuhusiana na kifo cha Yesu cha upatanisho. Badala yake, wachungaji wanasisitiza nguvu juu ya ulimwengu wa maroho, uponyaji wa miujiza, na tafsiri ya ndoto.¹⁰⁵

Kama dini zote ni sawa, usawazishaji ungekubalika. Hata hivyo, kama tulivyokuwa tumeona awali, kuna njia moja tu ya kwenda kwa Mungu. Wanadamu wanaweza kumwendea Mungu kwa njia moja tu kupitia Yesu Kristo. Njia nyingine zote ni feki. Haziongozi njia ya kwenda kwa Mungu. Hatuwezi kufuata njia feki na njia sahihi kwa wakati mmoja.

Jaribu kufikiria kwamba mimi nimekupa kikombe cha kimiminika. Nikakuambia, "Hiki kikombe kina aina mbili za vinywaji vilivyochanganya pamoja. Mojawapo ya kinywaji kwenye kikombe ni cha afya sana. Kinywaji kingine ni sumu kali sana inayoweza kukuua. Nilivichanganya ili uweze kupata vinywaji vyote viwili kwa pamoja." Je! Utakunywa kinywaji kilichoko kwenye kikombe? Kwa hakika hapana. Kinywaji chenye sumu kimeharibu kabisa kinywaji chenye afya.

Kwa njia hiyo hiyo, haiwezekani kumwabudu Mungu na dini za uongo kwa wakati mmoja. Paulo alisema, "Hamwezi kunywea kikombe cha Bwana na kikombe cha mashetani. Hamwezi kushirikiana katika meza ya Bwana na katika meza ya mashetani."¹⁰⁶

Katika Agano la Kale, baadhi ya watu katika Israeli walitaka kumwabudu Yehova wakati huo huo wakiabudu mungu wa uongo Baal. Elia akawaauliza, "Mtasita-sita katikati ya mawazo mawili hata lini? Bwana akiwa ndiye Mungu, mfuateni; bali ikiwa Baali ni Mungu, haya! Mfuateni yeye."¹⁰⁷

Katika imani zetu, katika taratibu zetu za kuabudu, na katika mfumo wetu wa maisha, tunaweza kumfuata Kristo au tunaweza kuifuata miungu ya uongo. Hatuwezi kufanya vyote kwa pamoja.

Ni kwa jinsi gani tunaweza kuwakilisha Injili kwa wanaoamini katika mizimu?

Kwa kuwa kipengele chenye nguvu kwa waamini mizimu ni hofu, **Wakristo wanapaswa kuonyesha nguvu ya Mungu dhidi ya hofu**. Kwa kuonyesha upendo wa Mungu na kwa uangalifu kushiriki habari njema za injili, Mkristo anaweza kuwasaidia waamini mizimu kuishinda hofu yao dhidi ya mizimu. Mpaka hapo hofu itakaposhindwa, waamini mizimu wengi watakuwa na wasiwasi wa kuitikia injili. Wakristo wanapaswa waoneshe, upendo wao kwa majirani zao waamini mizimu kuptilia imani yao ya uhakika katika Mungu wao mwema, kwamba upendo kwa ajili ya Mungu huitupa hofu nje. Yohana aliandika, "Katika pendo hamna hofu; lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu, kwa maana hofu ina adhabu; na mwenye hofu hakukamilishwa katika pendo."¹⁰⁸

¹⁰⁵ Winfried Corduan. *Neighboring Faiths*. (IL: Intervarsity Press, 1998), 156

¹⁰⁶ 1 Wakorintho 10:21

¹⁰⁷ 1 Wafalme 18:21

¹⁰⁸ 1 Yohana 4:18

Yesu Kristo hutukomboa katika hofu.

John Seamands alielezea habari za kabile la Ibani nchini Malaysia. Kabile hili la waabudu mizimu waliishi kwenye hofu endelevu ya ndoto, panya, na aina fulani ya ndege. Wakati kundi la Wakristo wa Kichina walipokwenda Malaysia baada ya Maasi ya Mpiganaji ngumi, Waibani walishangazwa kwamba hawa Wakristo walitembea kuititia katika msitu huo bila hofu. Wakauliza, "Je! hamna wasiwasi na maroho ya uovu?" Wakristo wa Kichina waliwajibu, "Hapana! Mungu wetu yuko hai. Anatupenda sisi na ana nguvu kuliko nguvu nyingine zote." Leo hii, kuna maelfu ya Wakristo Waibani. Ushuhuda wao wa kwanza kila wakati ni, "Yesu Kristo amenikomboa mimi kutokana na hofu."¹⁰⁹

Kwa kuwa injili si ya mifumo ya maisha ya Magharibi, **Wakristo wasifikiri kwamba injili ni sawa na utamaduni wa Magharibi.** Mwanzoni mwa karne ya ishirini, baadhi ya wamisionari walijaribu kuanzisha "Uingereza Ndogo" ndani ya nchi nyingine. Watu katika suti na tai zao za Kimagharibi waliimba nyimbo za kimagharibi wakati wakiwa wamekaa kwenye viti katika mtindo wa kanisa la kimagharibi lililo na kinara. Tunapaswa tuiweke injili katika njia ambayo itawasilishwa kwa ukamilifu kwa walengwa wetu wote.

Mwisho, kwa kuwa mfumo wa usawazishaji mara nyingi umeidhoofisha injili, **Wakristo wanapaswa kuwasilisha injili kwa usahihi na uwazi.** Ni lazima tuwatambulisse waamini mizimu kwa Mungu wetu ambaye anawapenda na anataka awe na mahusiano nao. Ni lazima tuwatambulisse waamini mizimu kwa Yesu Kristo ambaye alikufa kwa ajili ya kufanya upatanisho wa dhambi zetu na ambaye alifufuka kutoka kaburini akiwa na ushindi juu ya kifo.

Hatupaswi kuweka mbadala wa ujumbe wa msingi wa maisha ya Yesu, kifo cha upatanisho, na kufufuka katika kutaka kuwavutia waamini mizimu na matendo ya ishara na miujiza, au mbinu za kufanya maombi ili "kumlazimisha" Mungu afanye yale tunayoomba. Mungu wetu siyo mzimu wa kikabila wa kuchezea; ni mwenye mamlaka juu ya ulimwengu wote. Tutakapofundisha kwamba Mungu anaweza kuchezewa kuititia mbinu za maombi na "matambiko ya imani" tunamleta awe kwenye kiwango cha chini cha mungu wa kabilu. Elimu ya kuitetea imani kwa wanaoamini mizimu kamwe isishushe kiwango cha injili hadi kuwa dhaifu kwa ajili ya kuwavutia wasikilizaji.

Yesu Kristo ana nguvu kuliko maroho ya uovu.

Wanaoamini mizimu wanaosikia injili kwa mara ya kwanza mara mara watalinganisha uwezo wa nguvu alizo nazo Mungu wa Wakristo na nguvu za mizimu yao ya kikabila. Elimu ya kuitetea imani yenye nguvu kwa mwamini wa mizimu itamdhiihirishia uwezo wa Mungu. Wakati hatupaswi kumchezea Mungu ili afanye kama tunavyotaka katika mipango yetu,

¹⁰⁹ Maelezo mengi yaliyoko katika sehemu hii yamenekuliwa kutoka kwa John T. Seamands, *Tell It Well*, (Kansas City: Beacon Hill Press, 1981).

tunatakiwa tuwe wepesi kuishi ili kuruhusu Roho wake afanye kazi kupitia kwetu katika kudhihirisha uwezo wa Mungu.

Mmishenari mmoja kwa ajili ya Wafilipino alimtembelea dada mmoja ambaye alidhoofishwa na ugonjwa wa ajabu. Huyu dada alitoka katika kabilia ambalo ndilo kwanza limetoka katika kuisikia injili kwa mara ya kwanza. Kila mtu katika kjiji kile alijua kwamba ugonjwa wa huyu msichana ni matokeo ya nguvu za giza. Shetani alikuwa anakipiga kile kijiji kwa sababu watu walikuwa wamekubaliana na mafundisho ya Injili.

Mmishenari alisema, "Ninajihisi kusikia uwepo wa nguvu ya uharibifu." Yule Mmishenari na Wachungaji wa Kifilipino wakamwombea yule dada kwa jina la Yesu Kristo. Waliimba nyimbo zilizohusiana na uwezo wa jina la Yesu na uwezo wa damu yake iliyomwagika. Msichana alifunguka saa hiyo hiyo. Uponyaji wake ulikuwa ni ushuhuda mkubwa mno kwa kabilia hili la waamini mizimu. Waliona kwamba Mungu ni mwenye uwezo zaidi kuliko mizimu yao ya kikabila. Kuanzia hapo hawakuogopa tena mizimu.

Itakuwaje kwa wale ambao kamwe hawajawahi kuisikia Injili?

Biblia inafundisha kwamba Yesu ndiye njia pekee ya kuingia mbinguni. Kauli hii inazua swalii gumu sana. Inakuwaje kwa mtu anayekufa bila ya kuisikia Injili? Je! Kuna matumaini yeyote kuhusiana na mtu huyu? Je, kulikuwa na uwezekano wa wao kuokolewa?

Ninaamini kwamba jibu ni *ndiyo*. *Kulikuwa na uwezekano wa wao kuokolewa*. Jibu langu haliegemei moja kwa moja kwenye Biblia, lakini litakuwa kwenye seti za kweli za Biblia ambazo kwa njia nyingine zinafanania na swalii. Mungu ni mwenye haki na mwenye upendo ambaye hataki hata mtu mmoja apotee. Alimpangia kila mmoja katika dunia njia ya wokovu, na Roho Mtakatifu yuko duniani akimvuta kila mtu kwa Kristo kwa njia mbalimbali. Ninaamini kwamba kama mtu ambaye hajawahi kuiona Biblia akikubaliana na ufunuo wa ujumla wa uumbaji na dhamira ya ndani kwa kumsihi Mungu kutoka moyoni, Mungu atamfunulia taarifa ya kutosha ya wokovu. Taarifa zinaweza kutoka kwa mmishenari, malaika, ndoto, au ufunuo wa moja kwa moja kutoka kwa Mungu.

Ufunuo huu unaweza kuwa wenyewe mipaka. Hakuna fundisho la Biblia kwamba ujumbe wote wa kihistoria wa injili ni muhimu ili kuweza kuamini katika Kristo kwa ajili ya wokovu. Imani inayookoa inaweza kuegemea kwenye uelewa wenyewe mipaka wa maudhui ya imani.

Lengo la imani ya huyu mtu bado ni Kristo, ingawaje inaweze kana asiweze bado kujua jina la Yesu au imani ya Utatu Mtakatifu. Mwamini huyu anaweza tu kirahisi akaelewa kwamba Mungu Muumbaji kwa namna fulani ametoa njia ya kupunguza pengo kati ya mwanadamu na Mungu. Bila ya kuwepo na ufunuo kamili wa injili, mtafutaji huyu anaweza akaiweka imani yake ndani ya Mmoja Aliyetumwa ili kupunguza pengo hilo.

Hii haimaanishi kwamba watu wanaweza kuamini chochote wakitakacho. Kupitia neema ya Mungu, mtafutaji itambidi aisahau miungu ya uongo inayomzunguka, atambue kwamba hawezu kujisaidia mwenyewe, na amtafute kwa imani Mungu wa kweli Muumbaji. Mtafutaji

anapokuja kujifunza zaidi kuhusu Kristo, ni lazima akumbatie kweli za injili. Hawezi akakataa imani za msingi za Kikristo.

Imani ya neema iliyotangulia ni muhimu katika kujibu swali hili. Neema iliyotangulia inafafanuliwa kama “neema inayotangulia kabla ya kukombolewa.” Biblia inafundisha kwamba neema imetolewa kwa kila mtu katika dunia. Paulo aliandika, “Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa.”¹¹⁰ Neema iliyotangulia ni kwa ulimwengu wote, lakini pia inaweza ikakubalika au ikakataliwa.

Kama Neema ya Mungu inaleta wokovu kwa “watu wote,” hii inamaanisha kwamba Mungu atatoa njia kwa hiyo Neema. Kama mtu mmoja ataitikia kwa kukubaliana na hiyo neema, haijalishi yuko mbali kiasi gani kutoka kwa ushawishi wa wamishenari, Mungu atampa mwanga na neema Zaidi.

Neema hii inaweza kumpa mtafutaji kuifanyia kazi imani ndani ya Yesu. Neema hii inatenda kazi hata kama mtafutaji hajawahi kusikia ujumbe kamili wa injili au kama Mungu atafunua ukweli kupitia malaika au ndoto. Mungu atamwokoa mtu yeyote anayemtafuta Mungu mmoja wa kweli wa uumbaji kwa moyo wake wote.¹¹¹

Hakuna hata mtu mmoja atakayesimama mbele za Mungu na kwa ukweli wote aseme kwamba ilikuwa vigumu kwake kumtafuta Mungu wa kweli na kuamini katika Yesu. Kama hatutamtafuta Mungu, tutatambua siku ya hukumu kwamba tulikuwa na nafasi ya kumtafuta Mungu wa kweli. Kama kwa ukweli tutamtafuta Mungu kwa moyo wetu wote, tutapewa ukweli wa kutosha wa kumwamini Kristo kwa ajili ya wokovu.

Uinjilisti bado ni muhimu. Ingawaje inawezekana kwa mtu ambaye hajafikiwa kwa uinjilisti kumlilia Mungu kwa ajili ya kuomba huruma, bado ni muhimu kwamba Wakristo wachangamkie kupeleka injili. Kwa kuisikia injili inaleta uwezekano mkubwa kwamba mtu anaweza kuukubali ukweli. Wakristo wanaopeleka injili siyo tu kwamba wanawasilisha ujumbe; wanazungumza kwenye dhamira ya mwenye dhambi. Wanajaribu kuwatia hamasa wenye dhambi kuitoa mioyo yao kwa Mungu.

Kwa kuwa Mungu humvuta kila mtu kuja kwake, kila mtu atakuwa na nafasi ya kutafuta na kuupata ukweli wa Mungu wa kweli. Mwitikio kwa ajili ya Mungu unafanywa kuwa rahisi wakati wakristo wanapoomba kwa ajili ya watu waliopotea na kuwashirikisha injili. Imani ya neema inayotangulia inapaswa kutuhimiza zaidi kwenye uinjilisti, kwani tunajua kwamba Mungu yuko kazini katika kila moyo wa mtu. Kama Mungu ataokoa watu wengine nje ya kazi yetu sisi, ni kwa jinsi gani atafanya zaidi kama tutawajibika kuomba kwa ajili ya waliopotea na kuwashuhudia.

Wamishenari wamekutana na visa vingi ambavyo Mungu ameandaa watu ambao hawajafikiwa na uinjilisti kwa ajili ya injili. Wamishenari wameweza kuunganisha injili na vipengele vya utamaduni wa watu. Hii imefanya kuwa rahisi kwa watu kuelewa na kuikubali

¹¹⁰ Tito 2:11

¹¹¹ Yeremia 29:13

injili. Kusoma zaidi kuhusu hili, soma vitabu vya Don Richardson: *Uzima wa milele ndani ya mioyo yao na Mtoto wa Amani* (*Eternity in Their Hearts and Peace Child*).

► Ni vipengele gani katika mila yenu vinaonyesha neema ya mungu iliyotangulia ikiandaa njia kwa ajili ya injili?

Elimu ya kuitetea imani katika vitendo – Kuongoka kwa Lamin Sanneh

Dr. Lamin Sanneh (1942-2019)¹¹² alikuwa Profesa wa the D. Willis James Missions and World Christianity katika Chuo Kikuu cha Yale, ambako pia alitumika kama Profesa wa Historia. Profesa Sanneh alijifunza Kiarabu na Mafundisho ya Uislamu huko Uingereza na Beirut, Lebanoni. Alifundisha katika vyuo vikuu vya Havard na Yale.

Dr. Sanneh alikuzwa kama Mwislamu mwaminifu katika nchi ya Gambia. Alikuwa anafurahia msisimko wa mfungo wa Ramadhani na nafasi ya kuonesha uaminifu wake kwa dini yake wakati wa kufunga. Kama kijana mdogo, Lamin alikuwa Mwislamu mwaminifu sana aliyezingatia nidhamu ya imani ya Kiislamu.

Akiwa anasoma Kurani, Sanneh mara kwa mara alikuwa anaguswa na kile ambacho Kurani ilikuwa inasema kuhusu Yesu. Inafundisha kwamba Yesu alikuwa ni Mtume na Mjumbe kutoka kwa Mungu, lakini Yesu hakufa msalabani. Sanneth alivutiwa na maisha ya Yesu. Hata hivyo, alikuwa na wasiwasi kwamba huu mvuto unaweza kuja kumtoa kwenye Uislamu. Aliomba kwamba Mungu amlinde kutokana na kuguswa kwake na Yesu!

Hata hivyo, mvuto wa Sanneh kwa Yesu uliendelea kukua kwa nguvu sana. Hakuweza kuepukana na swali hili, "Je! Ni nani alikufa pale msalabani? Kurani inasema kwamba Yesu hakufa, bali Mungu alimweka mtu mwagine afe badala ya Yesu. Sanneh alihitaji kujua, "Ni nani aliywewkwa na Mungu kuwa badala ya Yesu?" Alianza kuwaza, "Labda, Yesu kweli alikufa msalabani. Labda Mungu aliruhusu hili. Kama ni hivyo, je, kwa nini Mungu aliruhusu Yesu afe?"

Dr. Sanneh alianza kujifikiria kuhusu maisha yake mwenyewe. Alikuwa amepatwa na jambo kubwa lililoleta huzuni katika familia yake. Akajiuliza, "Vipi kama Mungu aliruhusu Yesu ateswe kama sehemu ya ulimwengu? Vipi kama Yesu alikufa juu ya msalaba kushinda kifo?" Alianza kutambua kwamba msalaba ulikuwa ni muhimu kama njia ya Mungu ya kuingia katika ulimwengu wetu.

Ilikuwa ni katika kipindi kingine cha baadaye kwamba Dr. Sanneh alipokea nakala ya kitabu cha Biblia. Lakini Roho wa Mungu alikuwa amefungua macho ya Sanneh kwenye hitaji la kupokea wokovu. Wakati Sanneh alipopokea nakaia ya Biblia, alianza kwa kusoma vitabu vya Matendo ya Mitume na Warumi. Alijifuza kwamba Mungu ametoa kuhesabiwa haki siyo kwa kupitia nidhamu yake kali, bali kwa neema kupitia imani. Alianza kuona kwamba ni

¹¹² Imechukuliwa kutoka kwa Lamin Sanneh, "Jesus, More Than a Prophet" in Kelly Monroe, *Finding God at Harvard: Spiritual Journeys of Christian Thinkers*, (MI: Zondervan, 1996).

kwa kupitia neema yake tu kwamba tunawekwa huru kutokana na kushindwa kwetu kumpendeza Mungu aliye mkamilifu.

Profesa Sanneh alikuja kuamini kwa sababu Mungu alimfungua macho yake kwenye hitaji lake la kupata wokovu. Kisha Mungu akatumia Neno kumwonyesha Lamin Sanneh njia ya kwenda kwa Mungu.

Kazi za kufanya Somo la 9

(1) Elimu ya kuitetea imani na Kichwa: Fanya mtihani kutokana na maswali ya tafakuri yaliyoko katika Somo la 9. Jifunze maswali haya kwa uangalifu kwa maandalizi ya mtihani

(2) Elimu ya kuitetea imani na Moyo: Wingi wa taarifa zilizotumiwa kuandika somo hili zinazungumzia maswali ya wanaoamini mizimu na Waislamu. Je! Kuna watu unaowajua walioko aidha katika mojawapo ya dini hizi? Kama ndivyo, kuwapa injili zaidi sana ni kuandaa orodha ya maswali na majibu. Ili kuwa na ufanisi, ushuhuda wetu ni lazima utolewe katika uwezo wa Roho Mtakatifu. Anza kuomba ili kwamba Mungu:

- Akupe nafasi ya kushirikisha injili kwa rafiki yako mwabudu mizimu au Mwislamu.
- Upako wa kushirikisha injili kwa nguvu na usahihi.

(3) Elimu ya kuitetea imani na Mikono: Zungumza na mwabudu mizimu au Mwislamu. Kama unazungumza na mwabudu mizimu, onesha jinsi upendo kamili wa Mungu unavyosababisha hofu kuondoka. Kama unazungumza na Mwislamu, mwoneshe jinsi Mungu alivyo Watatu-katika-Mmoja.

Mtihani wa Somo la 9

(1) Orodhesha imani tano kubwa zinazohusiana na uwepo na asili ya Mungu. Fafanua kila moja.

(2) Kuna tofauti gani kati ya Ukristo na imani nyingine kubwa?

(3) Kuna vigezo mantiki gani vitatu na hitimisho ambavyo vinaonyesha ushahidi wa kibiblia wa imani ya Utatu Mtakatifu?

(4) Ni mambo gani matatu ya ulimwengu yanaonyesha imani ya Utatu Mtakatifu?

(5) Fafanua *Imani katika mizimu*. Ni nini tofauti kubwa iliyopo kati ya Imani katika mizimu na Ukristo?

(6) Fafanua *Usawazishaji*. Kwa nini usawazishaji haukulaliki kwa Wakristo?

(7) Imani ya Neema iliyotangulia ni nini?

(8) Nukuu kutoka kichwani Matendo 4:11-12.

Vianzo Vilivyopendekezwa

Kozi hii ni utangulizi wa kujifunza Elimu ya kuitetea imani. Kama unataka kujifunza zaidi, utafaidika kutokana na vitabu vilivyopendekezwa hapa.

Craig, William Lane. *On Guard*. Colorado Springs: David C. Cook, 2010.

Geisler, Norman and Frank Turek. *I Don't Have Enough Faith to be an Atheist*. Wheaton: Crossway Books, 2004.

Ham, Ken. *The New Answers Book: Over 25 Questions on Creation/Evolution and the Bible*. Green Forest: Master Books, 2006.

Little, Paul. *Know Why You Believe*. Downers Grove: Intervarsity Press, 2008.

McDowell, Josh. *More than a Carpenter*. Wheaton: Tyndale Momentum, 2009.

McDowell, Josh. *The New Evidence That Demands a Verdict*. Nashville: Thomas Nelson, 1999.

McDowell, Sean. *A New Kind of Apologist: Adopting Fresh Strategies; Addressing the Latest Issues; Engaging the Culture*. Eugene: Harvest House, 2016.

Qureshi, Nabeel. *No God but One: Allah or Jesus?* Grand Rapids: Zondervan, 2016.

Palau, Luis. *God Is Relevant: Finding Strength and Help in Today's World*. Colorado Springs: Multnomah, 2010.

Strobel, Lee. *The Case for Christ*. Grand Rapids: Zondervan, 2013.

Strobel, Lee. *The Case for Faith*. Grand Rapids: Zondervan, 2014.

Kumbukumbu ya Kazi Zilizofanywa

Jina la Mwanafunzi _____

Kwenye jedwali iliyopo hapa chini, onyesha ni lini kazi za kufanya ulizopewa zilipomalizilika. Elimu ya kuitetea imani na Kichwa inachukuliwa "imekamilka" pale tu mwanafunzi anapofikia kiwango cha ufaulu wa asilimia 70% au zaidi. Kazi zote za kufanya zilizotolewa zinatakiwa zimalizike kwa ukamilifu ili kuweza kupata Cheti cha ufaulu kutoka Shepherds Global Classroom.

Somo	Elimu ya kuitetea imani na Kichwa	Elimu ya kuitetea imani na Moyo	Elimu ya kuitetea imani na Mikono
1			
2			
3			
4			
5			
6			
7			
8			
9			

Maombi kwa ajili ya kupewa Cheti cha Kufuzu kozi kutoka Shepherds Global Classroom yanaweza kukamilishwa kuititia ukurasa wetu wa wavuti www.shepherdsglobal.org. Vyeti vitatumwa kwa mfumo wa kidigitali kutoka kwa Raisi wa SGC kwenda kwa wakufunzi na wawezeshaji ambao watakamilisha maombi hayo kwa niaba ya mwanafunzi (au wanafunzi).